# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Saba – Tarehe 15 Septemba, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na shughuli za Mkutano wa Nne, Kikao cha Saba. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Maswali ya Kawaida.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitaanza kwa kuwaomba radhi, kama mnavyofahamu kwamba siku ya Alhamis huwa ina ratiba maalum. Kutokana na udhuru ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu anao hatutakuwa naye leo, kwa jinsi hiyo tutaendelea na maswali ya kawaida. Swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima. Mheshimiwa Mbunge uliza swali lako.

Na. 86

### Mpango wa Kuipatia Halmashauri ya Itilima Fedha za Kutosha

**MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Halmashauri ya Itilima ni mpya iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria, lakini mpaka sasa hivi haijapata fedha za kutosha kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya Wilaya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia Halmashauri hiyo fedha za kutosha kwa ajili ya maendeleo yake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ilikuwa imepokea shilingi bilioni 5.04 kati ya shilingi bilioni 8.2 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwa ni asilimia 61.5 ya bajeti yote ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Halmashauri hiyo imetengewa shilingi bilioni 10.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na ongezeko la asilimia 26.8 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016. Upelekaji wa fedha katika Halmashauri za Serikali za Mitaa hufanywa kwa kuzingatia hali ya makusanyo ya Serikali kila mwezi. Hivyo, naomba kutoa wito kwa taasisi za umma na sekta binafsi kuweka mkazo katika kuimarisha makusanyo ya kodi na ushuru mbalimbali ili kujenga uwezo wa Serikali katika kutoa huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silanga, Mbunge wa Itilima, swali la nyongeza.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa bajeti ya 2015/2016 Serikali imeweza kupeleka asilimia 61.5 katika Wilaya ya Itilima; je, kulingana na makusanyo ya Serikali hivi sasa tunavyoona ina kasi kubwa ya kukusanya fedha nyingi, iko tayari kufidia asilimia 38.5 ya fedha ili kukamilisha miradi iliyobakia kwa 2015/2016? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa bajeti ya mwaka 2016/2017 ya Wilaya ya Itilima ina shilingi bilioni 10, hadi sasa Serikali inaweza ikaniambia katika *quarter* hii ya kwanza imepeka kiasi gani? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo swali la pili la ghafla mno sidhani kama Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa na majibu kamili. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema pale awali kwamba katika Wilaya ya Itilima, Halmashauri ya Itilima katika kipindi kilichopita imepelekewa asilimia 61 na hili ni kutokana na hali mbalimbali tulipotoka katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba nikuhakikishie kwamba Serikali itahakikisha kwamba inasukuma juhudi kubwa sana, fedha zinazokusanywa zinapelekwa kwa wananchi ndiyo maana hivi sasa ukiangalia kwamba hata kuna miradi ile ambayo ilikuwa imepitiliza mwaka *especially* miradi ya maji Serikali imekuwa ikitoa nguvu ya kutosha kupeleka fedha katika maeneo hayo lengo kubwa ni kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika bajeti ya mwaka wa fedha mwaka huu kwa mfano, wenzetu wa Itilima bajeti yao ya mwaka sasa hivi ni shilingi bilioni 10.2 lakini nikiri wazi kwamba katika katika hii bajeti ya maendeleo bado hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyoenda isipokuwa ni fedha za *OC* tu ambazo kiujumla wake katika Halmashauri mbalimbali tumepeleka hivi sasa karibuni shiingi bilioni 6.2 na Halmashauri ya Wilaya ya Itilima kwa *OC* ya mwezi wa Julai imepelekwa milioni 39, lakini lengo kubwa la Serikali kuhakikisha fedha iliyokusanywa iweze kupelekwa katika miradi ya maendeleo ili kukidhi yale makisio ya bajeti ya mwaka huu wa fedha yaweze kutekelezeka vizuri.

**SPIKA:** Ahsante! Nitawapa watu wawili, Mheshimiwa Doto Biteko na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii.

Kwa kuwa tatizo la kutokupelekewa fedha kwenye Halmashauri linajitokeza sana hasa Wilaya ya Bukombe na hasa fedha za barabara. Mji wa Bukombe, barabara zake nyingi zimekatika na tunaelekea kwenye msimu wa mvua.

Je, Waziri anawaambia nini wananchi wa Bukombe juu ya barabara hizi ambazo wakati wa msimu wa mvua tuna uhakika hazitapitika kama fedha hazitapelekwa kwa dharura?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli na naomba nikiri wazi kwanza siku zipatazo kama mbili Mheshimiwa Doto Biteko aliniletea *request* katika Halmashauri yake ikionesha miundombinu ya barabara hivi sasa ilivyoharibika kule katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, niseme wazi kwamba sasa hivi lengo letu kubwa ni Kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo yamekuwa korofi kwa sababu makusanyo yanaendelea kukusanywa tutaenda kuyafanyia kazi. Mheshimiwa Doto Biteko, naomba niseme kwamba lengo la Serikali na bahati nzuri hivi sasa unaona jinsi gani Serikali inakusanya misuli yake kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato. Naamini katika bajeti ya mwaka huu tutaipa vipaumbele hasa katika suala zima la miundombinu ya barabara kwa sababu tunajua ndiyo itachochea uchumi wa wananchi wetu kuweza kusafirisha mazao yao kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, kwa hiyo naamini kwamba katika jambo hili tutalipa kipaumbele katika Ofisi yetu ya Rais, TAMISEMI.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikitoa taarifa za makusanyo kila mwezi na imekuwa ikijisifia kwamba makusanyo yameongezeka kwa kiasi kukubwa. Lakini ni ukweli kwamba katika Halmashauri zetu fedha hazifiki na hazipo kabisa.

Je, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa hizo fedha ambazo mmekuwa mkisema mkizikusanya kwa wingi zikafika kwenye Halmashauri zetu nchini kwa sababu kule ndiko kwenye watu, ndiko ambako huduma inatakiwa kutolewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme wazi kwamba Serikali imekuwa na tumekuwa tukitoa taarifa kila mwezi kwamba kwa kipindi cha sasa Serikali katika makusanyo yake imejitahidi kwa kiwango kikubwa sana kukusanya fedha na makusanyo hayo ya fedha lengo lake mnakumbuka mwaka huu tuna bajeti takribani ya shilingi trilioni 29.54 na hii maana yake lazima fedha zikusanywe ili kwamba miradi iweze kutekelezeka.

Kwa hiyo, hayo makusanyo ya fedha yanayoendelea hivi sasa, imani yangu kubwa sasa hivi Serikali inajipanga kuna vipaumbele vingi ndiyo maana katika suala zima la awali kuna ile miradi ya maji ilikuwa inaendelea na wakandarasi wali-*mobilise* vifaa kutoka *site* na ndiyo

maana kwamba katika eneo la kwanza la kipaumbele ukiangalia miradi mingi ya maji ambayo ilikuwa inaendelea, hivi sasa mingi inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda katika sekta ya miundombinu ya barabara, ninyi mnafahamu ni mashahidi, wale wanaotoka kule maeneo ya Tunduru wanakuta barabara kutoka Songea mpaka kule Mtwara kwenda Masasi pale, zamani mitambo ili-*stuck* pale ilikuwa haifanyi kazi, lakini Serikali imepeleka pesa hizi. Sisi watu wa Dodoma na watu wa Manyara wanafahamu, barabara kutoka Dodoma kwenda Manyara pale, hapa katikati kipindi kilichopita, Wabunge walikuwa wanalalamika, kazi ilikuwa imesimama, sasa hivi ukiangalia karibuni zote zinaenda. Serikali inakusanya hizi nguvu na nina amini miradi yote iliyopangwa katika mwaka wa fedha mwaka huu tutahakikisha inatekelezeka kwa sababu ni *commitment* ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kipindi hiki cha bajeti.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli, kwa niaba yake, Mheshimiwa Paresso.

Na. 87

**Mgogoro wa Ardhi Kati ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) na Kijiji cha Lashaine – Monduli**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. JULIUS K. LAIZER)** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na mgogoro wa mipaka kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Kijiji cha Lashaine Wilayani Monduli, lakini mwaka 2011 yalifikiwa makubaliano chini ya Mkuu wa Wilaya kuwa mipaka yenye mgogoro isomwe upya kwa kutumia *GPS* na wananchi wa kijiji cha Lashaine wamekuwa wakisubiri zoezi la kusomwa upya mipaka kwa muda mrefu.

Je, Serikali itakamilisha lini makubaliano haya kwa kutumia *GPS* kusoma mipaka upya ili kumaliza mgogoro huo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Julius Laizer, Mbunge wa Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vinavyozunguka eneo la Jeshi la Monduli vimekuwa na migogoro ya mipaka na Jeshi kwa miaka mingi. Katika kumaliza migogoro hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli ilifanya vikao na makubaliano ya mipaka eneo la Jeshi na kulipima kwa kutumia vifaa vya kisasa yaani *GPS* mwaka 2004. Eneo la Jeshi lilipunguzwa kutoka ukubwa wa hekta 94,000 hadi hekta 86,966 ili kupisha makazi ya raia wa vijiji jirani yaliyokuwa yameingilia eneo la Jeshi kikiwemo Kijiji cha Lashaine.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mpaka wa Jeshi upande wa Kijiji cha Lashaine ni kuzibainisha *beacons* zilizowekwa ili wananchi waweze kuziona kwa wazi kwa mujibu wa ramani iliyosajiliwa yaani *boundary recovery.*

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Laizer kuwa azma yetu ya kufufua mpaka huo bado ipo na tutafanya hivyo tutakapopata fedha za kutekeleza jukumu hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa makubalinao hayo yalifikiwa mwaka 2011 na sasa ni miaka sita, na tatizo hili limeendelea kuwepo; je, ni lini sasa kwa uhakika kabisa Serikali itaenda kumaliza huu mgogoro uliopo kati ya wananchi na eneo hilo la Jeshi?

Swali la pili, kwa kuwa migogoro hii ya mipaka ya Jeshi na maeneo ya wananchi haipo tu Monduli, iko katika maeneo mbalimbali kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, nafahamu kumekuwa na mgogoro huu katika maeneo mengi ambapo Jeshi ina kambi zao. Sasa ni lini kwa uhakika Serikali itatuletea taarifa hapa Bungeni kwamba ina mkakati huu wa kwenda kumaliza matatizo hayo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mgogoro huu ni wa siku nyingi na kwamba sasa hivi wakati umefika upatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka huu wa fedha, bajeti ya Wizara yangu ilitenga shilingi bilioni 12 kwa ajili ya shughuli za uthamini, upimaji na ulipaji wa fidia katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, tukianza kupata fedha hizo hususan tatizo dogo kama hili la kuhuisha tu mipaka litashughulikiwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la kwamba migogoro hii iko mingi na lini taarifa italetwa, nataka nikiri kwamba sehemu nyingi za nchi yetu migogoro baina ya vijiji na Kambi za Jeshi ipo na kama nilivyosema awali tatizo ni fedha za kufanya uthamini kwa yale maeneo ambayo hayajathaminiwa, fedha za kufanya upimaji kwa maeneo yanayohitaji kupimwa na fedha za kulipa fidia kwa maeneo ambayo Jeshi linatakiwa kufidia.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe pia kwamba kuna maeneo mengi ambayo wananchi ndiyo wameingia katika maeneo ya Jeshi. Kwa hiyo, inabidi waelekezwe, waelimishwe wasiwe wanavamia maeneo ya Jeshi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tutakapoanza tu kupokea hizi fedha, kazi zote hizi nilizozitaja zitaanza kufanywa ili tuondoe migogoro hii inayokabili Jeshi letu na wananchi.

**SPIKA:** Swali la nyongeza nilikuona Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Masoud.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, suala la Monduli linafanana na suala la Makambako.

Mheshimiwa Spika, Makambako kuna eneo linaloitwa Kipagamo ambalo miaka ya huko nyuma wananchi waliipa Jeshi kwa ajili ya matumizi ya shabaha. Maeneo hayo sasa tayari

wananchi tumejenga shule na tayari kuna makazi ya watu na matumizi hayo sasa hayatumiki kama ambavyo yalivyokuwa yamekusudiwa huko nyuma kwa sababu pana shule na makazi ya watu.

Je, Serikali haioni sasa iko haja ya kuwarudishia wananchi eneo lile ili liendelee kutumika kwa shule na makazi ya watu na kwa sababu barua tulishaiandika kupitia Serikali ya Kijiji na nilimpa mwenyewe Waziri mkono kwa mkono, je, ni lini sasa Serikali itarudisha eneo hilo hilo liendelee kutumika kwa wananchi? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tafadhali.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba barua hiyo Mheshimiwa Mbunge alinikabidhi na nimeipokea na mimi nilichofanya ni kuipeleka Makao Makuu ya Jeshi ili wanipe maoni juu ya suala hilo. Ikumbukwe tu kwamba maeneo yaliyotolewa kwa ajili ya Jeshi yalipangiwa kazi za Jeshi, kwa hiyo inawezekana kwamba eneo hili sasa hivi halitumiki tena kwa shabaha kutokana na ukaribu wake na makazi ya watu lakini huenda linashughuli nyingine za kijeshi.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa hapo wavute subira tupate maoni ya Jeshi kuhusu eneo hili, ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa na ni imani yangu kwamba maoni hayo nitayapata muda siyo mrefu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali mwaka 2006 (miaka kumi iliyopita), Serikali iliahidi kuyapima, kutathmini na kutoa fidia maeneo kadhaa na ndani ya maelezo hayo maeneo yote mliyaeleza mkaainisha katika kitabu ambacho mlitupatia.

Swali linakuja, inakuwaje leo ndani ya muda wa miaka kumi Serikali haijaona umuhimu, ahadi zenu ambazo mlituambia maeneo hayo mtayapima, kutathmini na kutoa fidia na baadhi ya wameshakufa katika maeneo hayo; je, Serikali ina nia njema kulipa fidia wananchi hao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kwamba tumeorodhesha maeneo yote yenye migogoro na tumeyaorodhesha maelezo ya nini kinachohitaji kufanyika. Yapo maeneo ambayo yanahitaji kwanza kufanyiwa tathmini ya fidia, yapo yanayohitaji kupimwa, yapo yanayohitaji kutolewa fidia lakini yako vilevile kama nilivyosema awali yale ambayo wananchi walivamia na hawastahili kuwa hapo. Na ukweli wa mambo ni kwamba fedha zinazohitajika ni nyingi, kila mwaka tumekuwa tukitenga katika bajeti yetu, fedha kiasi fulani ili kupunguza awamu kwa awamu mpaka tumalize. Kwa bahati mbaya sana kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge ni kwamba fidia ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi wananchi wamejenga na kila nyumba ina thamani yake, kwa hiyo kuweza kulimaliza hili tatizo haraka ni vigumu kwasababu ya uwezo wenyewe wa kifedha. Tunachoweza kuendelea kusema ni kwamba kila mwaka, mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi bilioni 12, zikipatikana tutaanza sehemu moja baada ya nyingine ili kuweza kuondoa hili tatizo la muda mrefu. Mara nyingi nimekuwa nikisimama hapa nikijibu suala la migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na Wananchi lakini ningependa kutoa wito vilevile kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba tusaidiane.

Mheshimiwa Spika, zamani Jeshi lilikuwa lina maeneo makubwa sana. Kwa sababu ya uhaba wa ardhi, wananchi sasa hivi wamekuwa wakivamia maeneo hayo. Kwa hiyo, yale maeneo yote ya Jeshi yaliyovamiwa ambayo wananchi hawastahili kuwa hapo ni vema wakatoka katika maeneo hayo na sisi kama Serikali, wale ambao wanastahili ya kulipwa fidia tutaendelea kuwalipa kadri uwezo utakavyokuwa unaruhusu.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

Na. 88

**Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji (Mgangalenga)**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE** aliuliza:-

Upo mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika Kijiji cha Mpwayungu kwa jina maarufu Mgangalenga wa muda mrefu na Serikali imegharamia fedha nyingi sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha mradi huo ili wananchi waweze kunufaika nao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *scheme* ya umwagiliaji ya Mpwayungu ilijengwa kupitia Mradi Shirikishi wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji *(PIDP)* mwaka 2005/2006. Ujenzi wa *scheme* hii ulihusisha ujenzi wa banio na kuchimba mifereji ya kufikisha maji mashambani. *Scheme* hii ina eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lenye hekta 160. Eneo lililoendelezwa kwa kufikiwa na mifereji ya udongo linafika hekta 140 ambalo ni kwa ajili ya kilimo cha mpunga lakini kwa sasa eneo linalotumika ni chini ya hekta 25. Kwa sasa Serikali inaendelea na juhudi za kuhamasisha wakulima kulitumia eneo hilo ambalo limeshaendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Umwagiliaji itafanya mapitio ya usanifu wa mradi huu katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa nia ya kuongeza ufanisi wake.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu, hata hivyo naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa mzima wa Dodoma hakuna sehemu ambayo tuna mto unaotiririsha maji mwaka mzima, na kwa kuwa mradi ule haukuzingatia uchimbaji wa bwawa kwa maana ya kuyahifadhi maji ili baadaye wananchi waweze kuyatumia kwa kumwagilia.

Je, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini juu ya uchimbwaji wa bwawa ili tuweze kuvuna maji na baadae tuweze kuyatumia na ili ule mradi uweze kuleta ufanisi?

Swali la pili, kwa kuwa kwenye majibu ya Serikali kuna baadhi ya vitu vingi vimeachwa, Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kujionea kwa macho hali ilivyo kwenye mradi huo? Ahsante *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Maji na Umwagiliaji Injinia Isack Kamwelwe majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kweli Mkoa wa Dodoma hauna mito ambayo inatiririsha maji mwaka mzima na ndiyo maana Mheshimiwa Lusinde wewe ni shahidi, kupitia Bunge la Bajeti ambalo limeisha juzi juzi hapa la mwaka huu wa fedha tuliagiza kwamba kila Halmashauri ifanye usanifu wa bwawa moja kila mwaka kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua na pia kukinga maji ya mifereji au mito ili tuwe na maji toshelezi kwa ajili ya matumizi ya binadamu mifugo na kilimo cha umwagiliaji.

Pamoja na hilo Awamu ya Tano kupitia Wizara ya Maji tumeeamua kwamba miradi yote mikubwa ya maji kuanzia sasa tutakuwa tunaweka mabomba mawili, bomba la maji safi ya kunywa pamoja na bomba kwa ajili ya umwagiliaji na kwa kuanza, mradi ambao unakuja ambao utahusisha ujenzi wa Bwawa la Farkwa kwa ajili ya maji ya Dodoma tumesanifu na tumeweka mabomba mawili, moja kwa ajili ya maji masafi ya binadamu na maji ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili umeuliza kama niko tayari kuongozana na wewe kwenda kwenye eneo lako kwa sababu sasa hivi ni kipindi cha Bunge, Mheshimiwa Spika kwa ruksa yako niko tayari, lakini baada ya Bunge basi itabidi nipewe ruhusa na Waziri wangu wa Maji na Umwagiliaji.

**SPIKA:** Maswali ya nyongeza Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Lubeleje. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Jimbo la Rombo kama yalivyo Majimbo mengine tuna shida kubwa sana ya maji, shida yetu hasa inatokana na kampuni ambayo inasambaza maji katika Jimbo letu *Kili Water* kuwa na ukata mkubwa baada ya *GTZ* waliokuwa wafadhili wake kujiondoa. Halmashauri tangu awamu iliyopita imeleta maombi katika Wizara ya Maji ili tuweze kuanzishiwa mamlaka kwa sababu mamlaka ina uwezo wa kukopa kuanzisha vyanzo vipya vya maji ili iweze kusimamia vizuri hali ya maji katika Jimbo letu. Hivi majuzi nimemkumbusha Waziri kuhusu hitaji hilo.

Sasa nataka nijue, je, Serikali ni lini watatusaidia kwa kushirikiana na TAMISEMI ili tuweze kuwa na mamlaka ya maji katika Wilaya ya Rombo itakayoweza kusimamia vizuri usambazaji wa maji yaliyopo na kuanzisha vyanzo vipya vya maji?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwenye Sera yetu ya Maji ya mwaka 2002 miradi ya maji ni shirikishi kati ya Serikali na wananchi, Serikali inajenga wananchi wanaiendesha kwa mfumo wa kutengeneza hizi mamlaka ndogo ndogo na mamlaka kubwa.

Kwa hiyo, zipo taratibu naomba nimhakikishie Mheshimiwa Selasini kwamba tutakwenda kuliangalia ombi lake *viability* ya Halmashauri yake kuweza kuendesha huo mradi badala ya *Kili water*. Kwa hiyo, hilo tunalichukua na tutakwenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Wilaya ya Mpwapa na Kongwa kuna mabonde mazuri sana ya maji na yanatiririsha maji mwaka mzima. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga *scheme* ya umwagiliaji katika vijiji vya Godegode, Nzovu, Bori, Msagali, Tambi, Mang'weta, Chamkoroma, Mseta na maeneo mengine ili *scheme* hii iweze kusaidia kilimo cha umwagiliaji na kusaidia kuondoa tatizo la njaa, katika maeneo hayo?*(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Maji, Injinia Lwenge.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, mapendekezo yake ya kutaka *scheme* hizo za Godegode na zingine mara nyingi tunaziandaa wakati tunatayarisha bajeti, kwa mwaka huu katika mapendekezo ambayo tulikuwa tumeyapitisha kwenye bajeti kwanza ni kuendeleza na kukamilisha *scheme* ambazo tayari zilikuwa zinaendelea na zina makandarasi, tukasema awamu hii tutaendelea kwanza tufanye usanifu katika miradi mingine itakayofuata baada ya kukamilisha hii ambayo inaendelea. Kwa hiyo Mheshimiwa, Godegode kwanza tuangalie zile *scheme* ambazo tayari tunazikamilisha halafu tutaanzisha na hizo zingine mpya. Tutazifanyia usanifu Tume ya Umwagiliaji ndiyo kazi kubwa itakayofanya mwaka huu wa fedha katika kuhakikisha maeneo mengi ambayo yanaweza kufanyiwa umwagiliaji tuweze kuyafanyia kazi.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa Wizara hiyo. Mheshimiwa Lubeleje.

**TAARIFA**

**MHE. GEORGE LUBELEJE**: Mheshimiwa Spika, samahani kidogo kuweka kumbukumbu sawa, mimi ni Mheshimiwa Lubeleje siyo Mheshimiwa Godegode. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Alikuwa anamaanisha maeneo ya Godegode ndani ya Wilaya ya Mpwapwa kuna eneo linaitwa Godegode. Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje kuweka sawasawa. Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo swali linalofuata.

Na. 89

**Kusuasua kwa Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia - Tunduru**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza:-

Miradi ya Maji ya Benki ya Dunia nchini imekuwa ikisuasua sana na hata ile iliyokamilika maji yamekuwa yakitoka wakati wa mvua tu.

Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi inayosuasua ikiwemo ile ya Wilaya ya Tunduru?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza programu ya maendeleo ya sekta ya maji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo. Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi katika Jimbo la Tunduru kama ilivyo pia katika maeneo mengine nchini ilitokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha pamoja na kutopatikana kwa vyanzo vya maji vya uhakika katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo Sekta ya Maji, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilipanga kutekeleza jumla ya miradi kumi na moja, kati ya hiyo, miradi minne ya vijiji vya Nandembo, Nalasi, Lukumbule na Amani ujenzi wake unaendelea na miradi minne katika vijiji vya Majimaji, Muhuwesi, Nakapanya na Mchoteka haikupata vyanzo. Aidha, mradi wa Mbesa umesimama baada ya Halmashauri kuvunja mkataba wa mkandarasi kutokana na kutokishi taratibu za kimkataba na tayari taratibu zinaendelea kumpata mkandarasi mwingine.

Mheshimiwa Spika, miradi yote ambayo haikupata vyanzo itapewa kipaumbele katika Awamu ya Pili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliyoanza mwezi Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha miradi hiyo inakamilika, mwezi Agosti, 2016 Wizara imetuma kiasi cha shilingi milioni 147.4 kwa Halmashauri ya Tunduru na Serikali itaendelea kutuma fedha kwa kadri zitakavyopatikana. Upungufu wa maji kwenye miradi iliyokamilika hususan wakati wa kiangazi umesababishwa na mabadiliko ya tabianchi pamoja na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kibinadamu. Wizara inashauri tuendelee kuihamasisha jamii katika uhifadhi wa mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani swali la nyongeza.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kukamilisha kwa miradi ya maji ya vijiji vya Nandembo, Nalasi, Lukumbule na Amani; je, Serikali haioni kwamba kuchelewa kukamilisha miradi hiyo kutaongeza gharama ya miradi?

Swali la pili, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji amesema vijiji vya Majimaji, Muhesi, Nakapanya na Mchoteka utekelezaji wake haukufanikiwa kutokana na kukosa vyanzo. Je, Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha vyanzo vinapatikana na

utekelezaji huu unaanza mara moja kwa sababu jambo hili ni la muda mrefu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji na Umwagiliaji Mhandisi Isack Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza amezungumzia Serikali haioni kwamba kuchelewa utekelezaji wa miradi kuna ongeza gharama; ni kweli ukichelewa utekelezaji wa mradi gharama inaongezeka kwa sababu kuna mabadiliko ya bei ambayo yanatokana na vifaa vya ujenzi, lakini pili wale wakandarasi wanaojenga wameajiri watu wao ile gharama ya mishahara muda unakuwa mrefu, kwa hiyo ni kweli kabisa kwamba kuchelewa kunaongeza gharama ya miradi. Kuchelewa kwa miradi kunatokana na matatizo ambayo yanajitokeza katika mkataba siyo kwamba ni suala ambalo linapangwa na binadamu basi tu ni kwamba, kwa mfano tunachelewa kwa sababu katika utekelezaji wa hii miradi tunasaidiana na wadau ambao ni marafiki zetu ambao wanatusaidia katika utekelezaji wa miradi sasa hela ikichelewa kupatikana basi kwa vyovyote vile lazima mradi uchelewe.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine tuna-*design* mradi kumetokea mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa na binadamu vyanzo vinakosa maji kwa vyovyote mradi ule lazima utachelewa.

Swali lake la pili amezungumzia suala la vyanzo, ni kwamba Serikali kwa sasa tayari kwa miradi ambayo haikupata vyanzo *study* zinaendelea kuhakikisha kwamba miradi hiyo inapata vyanzo na lazima vyanzo vipatikane ili tuweze kukamilisha utekelezaji wa hiyo miradi.

**SPIKA:** Wheshimiwa Wabunge, ninawaona lakini tuendelee na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano swali linaulizwa na Mheshimiwa Miza Bakari Haji.

Na. 90

**Barabara Zinazojengwa Chini ya Kiwango**

**MHE. MIZA B. HAJI** aliuliza:-

Kumekuwepo na kutoridhishwa kwa wananchi kutokana na barabara zetu kutengenezwa chini ya kiwango hali ambayo inapelekea barabara hizo kufanyiwa matengenezo mara kwa mara.

(a) Je, Serikali inaweza kugundua ni barabara ngapi nchini zilizotengenezwa chini ya kiwango?

(b) Je, ni hatua gani zilizochukuliwa kwa waliosababisha tatizo hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Miza hili jina hata Dodoma lipo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Miza Bakari Haji Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Spika, Serikali inaweza kugundua kama barabara imejengwa chini ya kiwango kwani ukaguzi wa ujenzi wa miradi ya barabara unatekelezwa wakati wote wa ujenzi na hata baada ya mradi kukamilika kabla ya muda wa ukaguzi wa mwisho kupita. Aidha, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara nne za Mbagala Rangi Tatu - Bendera Tatu, Sekenke - Shelui, Kyamyorwa - Buzirayombo na Nangurukuru – Mbwemkulu ulipokamilika yalijitokeza matatizo mbalimbali kabla ya muda uliotarajiwa yalijitokana na mapungufu kwenye ubora kama mashimo madogo madogo katika maeneo kadhaa ya barabara na kuharibika kwa tabaka mbili za juu.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida ujenzi wa barabara hutekelezwa kwa kuzingatia mikataba kati ya *TANROADS* na mkandarasi, na kati ya *TANROADS* na mhandisi msimamizi. Viwango vinavyotakiwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara vimetajwa katika mikataba husika. Endapo kunatokea tatizo lolote kuhusu ubora wa kazi, kwa mfano barabara kujengwa chini ya kiwango, vipengele vya mikataba husika hutumika kabaini nani aliyesababisha mapungufu hayo kati ya mkandarasi, mhandisi msimamizi au mwajiri na hatimaye kuwajibika. Kutokana na mapungufu hayo niliyoyataja juu katika barabara hizo nne, hatua zilichukuliwa kulinganana vipengele vya mikataba husika na makandarasi wa miradi hiyo walirekebisha mapungufu hayo kwa gharama zao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine inayosababisha uharibifu wa barabara ni wingi wa magari makubwa ya mizigo hususan magari makubwa ya mizigo yanayotumia *excel* zenye tairi moja yaani *super single tyre*. Hivyo kwa kuwa Sheria ya Uthibiti wa Uzito wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeweka kiwango kidogo cha uzito wa tani 8.5 kwenye *excel* zenye tairi moja *(super single),* Wizara inafanya utaratibu wa kuona ni jinsi gani itafanya mabadiliko ya Kanuni za Usalama Barabarani za mwaka 2001 ziweze kuona na sheria hiyo kwenye kipengele cha *super single*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miza Bakari Haji swali la nyongeza.

**MHE. MIZA BAKARI HAJI**: Mheshimiwa Spika, asante na mimi nina swali moja la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani mbadala ya kuwaepuka Wakandarasi wa aina hii ambao wanaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi na hasara kubwa kwa Taifa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali fupi la nyongeza, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Miza Bakari Haji kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuifuatilia kwa ukaribu sana sekta hii ya ujenzi, naomba nimhakikishie kwamba Serikali yetu iko makini kuhakikisha inafuatilia utekelezaji wa mikataba. Kwa sasa tunahakikisha mikataba yote inaziba mianya yote ya kumpa mtu unafuu wa kuja kuharibu baadaye na akaja akadai analindwa na mikataba. Kwa hiyo, tuna hakikisha mikataba tunaiweka sawasawa na tutakapogundua yeyote ambaye uwezo wake, tatizo siyo mikataba tatizo ni uwezo wake huwa tunamzuia hapati miradi tena mingine.

**SPIKA:** Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Gekul.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Sambamba na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ninaomba awahakikishie wananchi wa Sikonge ambao wamekuwa hawaridhiki na matengenezo ya barabara ya

Sikonge - Mibono hadi Kipili ambayo wakandarasi wamekuwa wakitengeneza kipande cha Sikonge hadi Mibono na kuacha kipande cha Mibono hadi Kipili bila matengenezoya aina yoyote kiasi ambacho haipitiki kila mwaka. Kwa sababu mwaka huu imepangiwa shilingi milioni 892 anawahakikishiaje wananchi wa Sikonge kwamba mwaka huu itatengenezwa kwa kiwango bora mpaka mwisho wa barabara ya Kipili?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wananchi wa Sikonge kwamba fedha hizo zilizotengwa ni kwa ajili ya pamoja na kipande cha Mibono hadi Kipili na tutahakikisha tunasimamia ili barabara hiyo itengenezwe kwa kiwango kizuri kama ambavyo imetengenezwa eneo la Sikonge hadi Mibono.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa miongoni mwa sababu ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezitaja, ambazo zinasababisha uharibifu wa barabara, magari na wakandarasi wasio waaminifu, sababu kubwa mwaka huu iliyosababisha barabara zetu kuharibika ni mvua za masika ambazo hazikutegemewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa kauli humu ndani katika Bunge la Bajeti kwamba *TANROADS* watoe fedha katika Halmashauri zetu kwa sababu ni dharura, wasaidie Halmashauri kujenga hizo barabara. Naomba nifahamu hii kauli ya Serikali imetekelezwa kwa kiwango gani, hususan katika Mkoa wangu wa Manyara na Jimbo la Babati Mjini maana hizo barabara hazijatengenezwa kabisa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kwa uelewa wangu kauli ambazo tulikuwa tunazitoa kati ya mwezi wa nne na mwezi wa sita kuhusu kuwataka *Regional Managers* wote wa *TANROADS* kuhakikisha wanarudisha mawasiliano katika barabara zilizokatika yalitekelezwa. Kwa kuwa anahitaji takwimu, naomba anipe muda nichunguze katika eneo lake kama kulitokea tatizo lolote, ili tuweze kulirekebisha.

Na. 91

**Ujenzi wa Barabara ya Nangomba - Nanyumbu**

**MHE. WILLIAM D. NKURUA** aliuliza:-

Ujenzi wa barabara za lami hufuata Ilani ya Chama Tawala na matamko ya viongozi. Katika ziara yake Wilayani Nanyumbu, Rais wa Awamu ya Nne aliahidi ujenzi wa barabara ya Nangomba hadi Nanyumbu kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Dua Nkurua, Mbunge wa Nanyumbu, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nangomba – Nanyumbu uliofanywa na Kampuni za *UWP – Consulting PTY* kutoka Afrika Kusini na *UWP Consulting Company Limited* ya Tanzania ili kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha ili kuanza ujenzi wa barabara hii. Aidha, *TANROADS* Mkoa wa Mtwara inaendelea na itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi tena ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa barabara hii ya kutoka Nangomba kwenda Nanyumbu imetolewa majibu ambayo yanatia moyo na sina mashaka kabisa na ahadi zinazotolewa na Serikali ya Awamu ya Tano; lakini kwa kuwa barabara hii inaunga barabara kubwa inayotoka Songea mpaka Mtwara, kwa jina maarufu inaitwa *Mtwara Corridor.* Barabara hii kutoka Songea mpaka pale ilipo mizani, Mnazi Mmoja ni zaidi ya kilometa 500.

Je, kwa kuwa Mangaka pana pacha ya kuelekea Msumbiji, Serikali haioni umuhimu wa kuweka pale mizani ili kuweza kudhibiti magari yote yaelekeayo Msumbiji na *Mbamba Bay* ili kulinda barabara zetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** Mheshimiwa Spika, nimepata taarifa hiyo kwamba kuna mchezo unafanywa na wasafirishaji wanaotumia magari makubwa kusafirisha bidhaa kutoka Songea kwenda Mtwara kwa sababu hakuna mizani kati ya Songea hadi Mangaka, hivyo wanabeba mizigo mikubwa, wanapofika Mangaka au kukaribia Masasi huwa wanapunguza mizigo kwa sababu mbele watakutana na mizani.

Mheshimiwa Spika, nimepata hiyo taarifa na ninaomba kuchukua nafasi hii kuwaagiza *TANROADS* wahakikishe wanaangalia mahali gani waanze kuweka mizani ya kutembea ili tuanze kudhibiti wakati kituo maalum cha kuweka mizani kitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwa sasa sehemu mbalimbali za vipande hivi vya barabara kati ya Mtambaswala, Mangaka hadi Songea havijakamilika. Inawezekana kwamba mahitaji hayo ya kuweka mizani yatafanyika baada ya kukamilika kwa wakandarasi wote katika barabara hiyo ya *Mtwara Corridor.* Ninaomba kazi hiyo ya kuweka mizani inayotembea *(mobile)* ifanyike haraka ili kuweza kuhakikisha kwamba barabara zetu hazianzi kuharibika kabla kazi haijakamilika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Mwita Waitara, atafuatia Mheshimiwa Shabani Shekilindi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa fursa niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa shida ya Nanyumbu na maeneo yaliyotajwa ni sawa na shida iliyopo Jimbo la Ukonga Dar es Salaam, ningependa kujua kauli ya Serikali kwamba barabara ya kuoka Banana – Kitunda – Kivule – Msongola ambayo imeahidiwa takribani ni awamu ya tatu, kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, pamoja na Majimbo yote Mkoa wa Dar es Salaam ikizingatiwa kwamba Wabunge wengi humu ndani wanakaa Dar es Salaam na Majimbo yao yana hali mbaya sana ya barabara hasa wakati wa mvua.

Ni lini barabara hiyo itakamilika? Nakushukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Banana – Kitunda – Kivule na kuendelea ni kati ya barabara ambazo zipo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 hadi 2020 kama ilivyo barabara ya Kongwa – Mbande ambayo Serikali imedhamiria kuijenga kwa kiwango cha lami katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mwita Waitara barabara hii kama sehemu ya *ring roads* za Dar es Salaam na kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tutaijenga kwa kiwango cha lami kama tulivyoahidi. Suala la lini, naomba sana katika masuala ya ujenzi wa barabara ni miradi mikubwa siyo rahisi sana kutoa tarehe.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne alipofika Lushoto alituahidi kilometa nne za barabara ya lami.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi hiyo iliyotolewa na Rais Mstaafu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, hicho kiwango cha kilometa nne ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne, na kama ambavyo nimekuwa nikisema kila wakati, dhamana tuliyopewa ni kuhakikisha tunatekeleza ahadi zote za viongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba kazi hii itafanyika katika kipindi hiki cha miaka mitano, kama ambavyo tumeongea huko nyuma na ninamsifu sana Mheshimiwa Shekilindi kwa kufuatilia, tutalitekeleza kama ambavyo nimekwambia huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumjibu Mheshimiwa Shekilindi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata la Wizara hiyo hiyo ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na linaulizwa na Mheshimiwa Asha Abdulla Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba swali langu namba 92 kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar na wale ambao wanaopenda kudumisha Muungano lijibiwe.

Na. 92

**Gharama za Nauli Dar es Salaam – Zanzibar**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Gharama za usafiri wa vyombo vya baharini na angani kwa safari za Zanzibar na Dar es Salaam ni za juu sana licha ya bei ya mafuta kupungua.

Je, Serikali inachukua hatua gani kusaidia wananchi hao kudhibiti nauli hizi za meli na ndege kwa kushirikiana na mamlaka husika toka pande zote mbili za Muungano?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo nyeti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuunguza nauli Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)* ina jukumu la kujenga ushindani katika sekta ndogo ya usafiri wa ndege na hi ni kwa mujibu wa Ibara ya 25 ya Sheria ya Usafiri wa Anga *(Civil Aviation Act [Revised Edition 2006])*. Panapokuwa na ushindani katika njia moja nauli hutokana na soko. Aidha, mamlaka huingilia kati kisheria kuweka kiwango kikomo pale tu inapotokea kuna ukiritimba na wananchi wanaumia.

Mheshimiwa Spika, mamlaka imejitahidi kuhusu ushindani kati ya Dar es Salaam na Zanzibar ambapo zaidi ya makampuni kumi ya ndege yanatoa huduma katika njia hiyo kwa nauli kati ya shilingi 140,000 na shilingi 278,000 kwenda na kurudi pamoja na kodi endapo msafiri atanunua tiketi mapema zaidi kabla ya safari. Kwa mfano, tarehe 4 Aprili, 2016 nauli ya juu kwa kampuni kumi za ndege zilizokuwa zinatoa huduma katika njia hiyo ilikuwa shilingi 139,000 na ya chini ilikuwa shilingi 75,000 ambapo wastani wa nauli kwa makampuni yote kumi kwenda tu pamoja na kodi ilikuwa shilingi 88,700.

Mheshimiwa Spika, utaona kuwa wastani wa bei ya nauli ya kwenda Zanzibar pamoja na kodi ni wa chini na unaendana na gharama halisi za uendeshaji na faida kidogo kwa mtoa huduma ukilinganisha na sehemu ambazo hakuna ushindani kabisa au hakuna ushindani mkubwa kama ilivyo Songwe na Mwanza. Hivyo, nashauri kwa mtu anayehitaji kusafiri afanye mipango ya safari yake mapema ili kupata unafuu wa nauli, maana kadri anavyonunua tiketi yake mapema kabla ya safari, ndivyo nauli inavyokuwa chini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya usafiri wa bahari kwa safari za Zanzibar na Dar es Salaam, kwa sasa kuna jumla ya vyombo sita vya majini vinavyotoa huduma hiyo. Vyombo hivyo vyote vimesajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Bahari Zanzibar *(Zanzibar Maritime Authority)*. Hivyo, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* imekwishafanya mawasiliano na *ZMA* ili viwango hivyo vya nauli za vyombo vya majini baina ya Dar es Salaam na Zanzibar vitathiminiwe kwa kuzingatia taratibu za mamlaka ya usajili wa vyombo hivyo.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu na kwa kuwa mimi ni msema kweli daima napenda niseme sijaridhika na majibu hayo; na kwa kuwa, Serikali yetu hii ya Awamu ya Tano imejikita zaidi kuwaondolea dhiki wanyonge na wanyonge wa Zanzibar pamoja na Tanzania Bara bado wanapata dhiki katika suala hili, nipende kusema na kumwambia Waziri kwamba ni kwa kiasi gani Serikali itaongeza udhibiti wa mamlaka husika kwa kuhakikisha kwamba bei hizi zinapungua na wananchi wanapata nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa haiingii akilini Mhesimiwa Waziri anaposema kwamba mtu anayetaka kufanya safari afanye *booking* siku nne au siku ngapi hizo zote anazoziona yeye; kwa kuwa safari nyingine ni za dharura sana. Kwa mfano, watu wanapokuja huku Bara ni kwa ajili ya kupata tiba katika Hospitali ya Rufaa, pengine Muhimbili, pengine Kituo cha *Cancer*

*Ocean Road* na mambo mengine ya dharura mtu anapoumwa unapomwambia akafanye *booking* ya siku nne ili apate nafuu ya ndege nafikiri hiyo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, Mheshimiwa Waziri bado atilie mkazo katika mamlaka hizi pamoja na hivyo vyombo vya pwani, bado nauli hii bado ni kubwa sana kwa wanyonge…

**SPIKA:** Sasa swali Mheshimiwa.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nataka majibu ya maswali yangu hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba kukubaliana na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma na ninamhakikishia kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwamba tutafute muda twende wote Zanzibar tukakutane na *Zanzibar Maritime Authority,* ili tukalijadili hilo kwa undani, hatimaye mamlaka hizo mbili za Muungano, mamlaka iliyoko upande wa Zanzibar na mamlaka iliyoko upande wa Tanzania Bara ziweze kutekeleza majukumu yake kama ambavyo Mheshimiwa Asha Abdullah Juma amependekeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha na Mheshimiwa Ngonyani itabidi mpate kibali cha Spika kabla ya kuondoka pamoja. Nimekuona Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. *(Kicheko)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, bado hayajaridhisha. Nchini kwetu safari za ndani ni ghali kuliko safari za kwenda nje ya nchi. Hii imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wetu. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kushirikiana na mamlaka hiyo ili kuweka kiwango maalum kisizidi hiyo bei kwa ajili ya kurahisisha usafiri kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, tuliamua na kupitia Bunge hili kwamba turuhusu ushindani na ndivyo tulivyofanya. Kupanga viwango kwa mamlaka zetu maana yake ni kutoka katika kile tulichoamua awali na mimi sina matatizo kama Bunge hili na Serikali kwa ujumla itaamua.

Kwa maoni yangu ni vema ngoja tuimarishe Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania* na mnafahamu tumeanza kuliimarisha, litaingiza ushindani mkubwa na mimi nina uhakika hao sasa hivi ambao wamepanga viwango vya juu watalazimika kuvishusha ama kuondoka katika biashara hiyo na kuliacha shirika letu likitamba. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Na mimi siridhiki kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya ushindani yanayosemwa kwanza hajawekewa mazingira mazuri ya ushindani na nauli kwa tunaosafiri kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam mara kwa mara, nauli kwa mfano za Shirika la *FastJet,* wanapoaihirisha safari wewe abiria hawakulipi na ukichelewa ndege unalipa zaidi ya nauli.

Je, *TCAA* na Mheshimiwa Waziri wanalijua hili na kama wanalijua wana mpango gani wa kuliondoa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali inaelekea lipo nyeti sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna majibu ya nyongeza kutoka Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, alivyoliweka ndivyo hivyo lilivyo. Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(IATA)* na sisi kama nchi mwanachama tunao wajibu wa kufuata taratibu za Kimataifa za usafiri wa anga. Moja ya taratibu zilizopo katika *IATA* ni kwamba ushindani ndiyo utatawala bei za tiketi katika usaifirishaji wa anga. Lakini ushindani huo umewekewa masharti, ikitokezea kwamba *route* iliyokuwa na ushindani sasa ushindani huo umekwisha kumetokeza *monopoly* ya msafirishaji mmoja; sheria za *IATA* na kwa maana hiyo sheria zetu za usafiri wa anga zinairuhusu mamlaka ya usimamizi wa usafiri wa anga kuweka ukomo wa bei kwa huyo msafirishaji ambaye anayo *monopoly* wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie *case* ya *Fast Jet* na *route* za Mwanza au Songwe. Ni kweli kwamba hizi *route* ya Dar es Salaam – Mwanza imekuwa inaendeshwa kwa ushindani kwa sababu zipo *scheduled flights* za kampuni zaidi ya moja. *Precision Air* bado wameendelea kuwa wana-*operate* kati ya Dar es Salaam na Mwanza ingawa siyo kwa *frequency* kubwa kama ilivyo ya *FastJet.* Na jambo hili limesababishia sana usumbufu kule mamlaka ya usimamizi wa usafiri wa anga kwa sababu linawafanya washindwe kuingia saa kwenye hiyo hatua ya kuwawekea ukomo *FastJet* wa nauli kwa sababu bado *route* inaonekana ina ushindani, kwamba *Precision Air* wapo wana-*operate* kwenye hiyo *route*.

Mheshimiwa Spika, lakini ikifika mahali kwamba *Precision Air* wamesimamisha kabisa safari zao za Dar es Salaam kwenda Mwanza basi mamlaka ya usimamizi wa usafiri wa anga itakuwa ina uwezo wa kisheria sasa wa kuweka ukomo wa bei kwa msafirishaji aliyebaki kwenye *route* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na pili usafiri wa ndani wa kawaida kimataifa bado huwa hauwezi kulinganishwa na usafiri wa nje kwa maana ya kuangalia umbali, hii ni *practice* ya dunia nzima ndivyo ilivyo, sio Tanzania pekee tu.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa Dar es Salaam – Dodoma; Dar es Salaam – Dodoma ndege zinazokuja ni ndege ndogo na hizi ndege ili iweze kuja na kurudi kwa faida lazima bei *per seat* iwe ni kubwa kidogo kuliko ndege kubwa zaidi ambayo ingefanya *route* ya namna hii. Ndiyo maana sasa hivi upanuzi huu wa uwanja wa Dodoma ndege za *size* kubwa zikianza kuja kwa vyovyote vile bei za kusafiri kutoka Dar es Salaam kuja hapa Dodoma kwa ndege zitashuka sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kutokana na unyeti wa swali hili, Mheshimiwa Flatei una swali la nyongeza?

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naona amejibu kama nilivyokuwa nafikiri.

**SPIKA:** Ahsante sana, nashukuru tuendelee na Wizara sasa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Joseph Haule, Mbunge wa Mikumi.

Na. 93

**Migogoro ya Wakulima na Wafugaji**

**MHE. JOSEPH L. HAULE** aliuliza:-

Kilio kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji kimekuwa ni cha muda mrefu sana kwa Wilaya ya Kilosa, lakini pia Jimbo la Mikumi, Kata za Tindiga, Kilangali na Mabwegere jambo linalosababisha wakulima kushindwa kwenda mashambani.

Je, ni lini Serikali itakomesha migogoro hiyo isiyo na tija kwa ustawi wa Taifa letu?

**NAIBU WAZIRI KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji katika Kata za Tindiga na Kilangali, inatokana na wakulima kukinga maji ya Mto Miyombo kwa ajili ya umwagiliaji na hivyo kusababisha yasitiririke na kuikosesha mifugo maji. Aidha, mipaka ya vijiji vya Kiduhi na Kilangali haijawekwa bayana kiasi cha kufanya mifugo kushindwa kupita kwenda kwenye maji. Chanzo cha mgogoro wa kijiji cha wafugaji cha Mabwegere ni vijiji jirani kutotambua mipaka ya kijiji hicho.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya maji kwa mifugo katika Kata za Tindiga na Kilangali kwa kuanzia katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imetenga fedha kwa ajili ya kuchimba lambo katika kijiji cha Kiduhi, Kata ya Kilangali.

Mheshimiwa Spika, jitihada mbalimbali zimefanyika katika kushughulikia migogoro ya Mabwegere hadi kuhusisha mahakama. Kwa sasa suala hili linashughulikiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambapo Waziri mwenye dhamana kwa mamlaka aliyonayo kisheria amemteua Jaji wa Mahakama Kuu ili kufanya uchunguzi wa mgogoro wa Kijiji cha Mabwegere.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo la migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi iliandaa mkutano wa Wakuu wa Mikoa mwezi Julai 2016, kwa lengo la kupokea taarifa ya utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kutenga maeneo ya malisho ya mifugo ikiwemo itakayotolewa kwenye mapori ya akiba na hifadhi. Baadhi ya maazimio yaliyofikiwa ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kufanya tathmini ya umiliki wa Ranchi za Taifa kwa lengo la kubaini maeneo ambayo hayatumiki kikamilifu ili wapewe wafugaji. Pia Wizara ya Maliasili na Utalii kufanya tathmini ya Mapori ya Akiba na Hifadhi yaliyopoteza sifa ili yatumike kwa shughuli nyingine ikiwemo ufugaji, hii ni pamoja na kutambua kuwa mapori mengi tengefu ni ardhi za vijiji kwa mujibu wa sheria na hivyo kuendelea kuwa maeneo ya malisho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Jay swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninasikitika sana kwa majibu ya Naibu Waziri anaposema kwamba wafugaji hawapati maji kwa sababu wakulima wamekuwa wakikinga hayo maji, nadhani wana upungufu wa *research*. Inaonesha kwamba mto Mkondoa na mto Miyombo inafika mpaka sehemu ambazo wafugaji wapo na tatizo lao kubwa siyo maji, tatizo lao kubwa ni malisho. Ndiyo maana wameonekana sehemu za Malangali wakilisha katika sehemu za mashamba ya watu na sehemu ambazo watu wamehifadhi mazao yao.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Tindiga pamekuwa siyo mahali salama kwa watu kuishi na kwa kilimo kwa sababu wafugaji wameonekana ku-*take over* maeneo yale na hapa nnavyozungumza na wewe pamekuwa na mauaji kila mwezi; tarehe 8 Juni ameuawa kijana anaitwa Ally Mbarouk Makakala na juzi tarehe 6 Septemba wameuawa watu wawili Elia Emmanuel Mbwane na Ramadhani John Mashimba.

Je, Serikali inawahakikishiaje usalama wa wakulima wa pale Tindiga lakini pia inawahakikishiaje usalama wananchi wa Tanzania ambapo suala la migogoro ya wakulima na wafugaji limeonekana kuwa kero kubwa sana hapa nchini? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Mkuu wa Mkoa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilikuja Tindiga na kutoa baadhi ya maagizo ambayo mpaka sasa hayajafanyiwa kazi na kupelekea vifo vya hao watu wawili vilivyotokea juzi.

Je, Naibu Waziri pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani wapo tayari kuambatana pamoja na mimi kuelekea Tindiga kuona hali halisi ya mauaji na hali ya kutotulia katika Jimbo la Mikumi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo zito, Naibu Waziri Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge haridhiki na maelezo yangu nafikiri bado tuna fursa ya kuangalia suala hilo ili tuweze kupata maelezo mengine na ninamuahidi kwamba tukitoka hapa nitakaa naye tuone namna gani tunaweza tukapata taarifa ambazo zitatusaidia kuboresha hiyo ambayo tunayo ili tuweze kufanya yale ambayo ni ya muhimu kwa ajili ya kushughulikia mgogoro huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu mauaji ambayo yametokea Mheshimiwa Mbunge amewasiliana na sisi. Tunafahamu kwamba ni sehemu ya changamoto kubwa tuliyonayo nchi nzima ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Ndiyo maana kama nilivyoeleza katika swali la awali Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara zingine ikiwepo Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maliasili na TAMISEMI tayari kuna timu ya Wizara hizo inafanya *ground work* kuja na mapendekezo ambayo yatatusaidia kuondoa migogoro tuliyo nayo. Kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Mbunge akiwa na subira na katika muda ambao siyo mrefu tutafikia muafaka wa namna ya kusuluhisha matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba maagizo ya Kamati ya Ulinzi na Usalama hayajatekelezwa. Vilevile nipo tayari nikitoka hapa kuwasiliana na Mheshimiwa *DC* wa kule kujua ni kwa nini maagizo yale hayajatekelezwa, ikibidi kama anavyopendekeza mimi mwenyewe sitasita kuandamana naye kwenda Jimboni kwake kuangalia hali hii. Pamoja na kwamba tayari nafahamu aliyekuwa wakati huo Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba tayari alishafika kwenye eneo hilo. Serikali hatutaki hii migogoro iendelee na pale panapotakiwa tufanye jambo lolote la kunusuru na kusuluhisha tutafanya hivyo. Kwa hiyo,

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo shida kwenda Jimboni kwake kuangalia hii hali. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mwigulu Nchemba.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu sahihi aliyoyatoa. Niseme tu na mahali pote wasikie kwamba hakuna shamba lolote ambalo linafanana na thamani ya maisha ya mwanadamu, wala hakuna kundi lolote la mifugo ambalo linafanana na maisha ya mwanadamu. Kwa hiyo, hakuna mgogoro wowote ule ambao unaleta uhalali wa kuua mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia kigezo hiki nitoe maelekezo katika Mkoa husika na Wilaya husika kuwasaka wowote wale waliohusika na mauaji hayo na sehemu yoyote ile ambako watatumia vigezo vya mgogoro kuua watu, wakamatwe na wafikishwe kwenye mkono wa sheria. Kama watatumia kigezo cha *mob* nielekeze katika Kijiji husika ambacho watapoteza maisha ya mwanadamu, wakamate vijana wote wenye nguvu ambao wanaweza wakawa wawefanya hivyo ili kuweza kupekua na kuweza kupata wale waliofanya kazi hiyo. Kama Magereza hayatoshi wawaachie huru vibaka wote walioiba simu na vitu vidogo vidogo, wakamate wale wanaoua watu wawekwe ndani ili tuweze kukomesha utaratibu wa watu kuua wananchi wasiokuwa na hatia na kuwasababishia matatizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hivi baada ya majibu haya mazuri muhimu kweli bado mna maswali ya nyongeza? Mheshimiwa Saddiq Muradi nimekuona, swali moja la nyongeza na swali la mwisho kutoka Mtwara kule.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa Wilaya ya Mvomero kuna migogoro mikubwa sana ya wakulima na wafugaji zaidi ya Wilaya ya Kilosa na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero imefanya mikakati mbalimbali kupunguza migogoro hii na zipo juhudi kubwa sana zilifanyika na aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alifika mara mbili na aliahidi kutupatia fedha kwa ajili ya kujenga majosho na malambo; fedha ambazo hadi leo hazijapatikana. Majosho na malambo yale yatasaidia ng'ombe wale kwenda kupata maji katika maeneo ambayo yapo nje ya mashamba ya watu.

Je, Serikali ipo tayari kutimiza ahadi hiyo ya Waziri ili tuweze kupata fedha za kujenga malambo na majosho Mvomero? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alitoa ahadi kuhusu miundombinu hiyo ya malambo na majosho. Nipende tu kusema kwamba alifanya hivyo kama Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi na hakufaya kama binafsi. Kwa hiyo, ahadi aliyoitoa bado ipo kwenye Wizara yangu hajahama nayo. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu itaendelea kuwasiliana na Halmashauri ya Mvomero ili kuhakikisha kwamba ahadi yetu hiyo ya Wizara inatekelezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerome Bwanausi, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba migogoro hii ya wakulima na wafugaji inasambaa karibu maeneo mengi hapa nchini ikiwa ni pamoja na katika Jimbo la Lulindi katika Vijiji vya Sindano, Maparawe, Mapili pamoja na Manyuli.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuja kule kusaidiana na kusuluhisha matatizo yaliyopo kati ya mpaka wa Tanzania na Msumbiji hususani katika eneo la kando kando mwa Mto Ruvuma ambako wananchi wengi ndio hulima lakini tayari kuna uvamizi mkubwa wa wafugaji ambao sasa upotevu wa amani umeanza kuwepo katika eneo hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, changamoto za migogoro ya wafugaji na wakulima na migogoro ya ardhi ya aina mbalimbali ni kweli kwamba ipo karibia kila kona ya nchi yetu. Kwa hiyo, pamoja na kwamba tupo tayari kwenda kila Jimbo katika kila kona ya kuangalia namna gani ya kutatua, Wizara na Serikali kwa ujumla inafikiria kutafuta suluhu ya jumla; suluhu ambayo itasaidia katika maeneo yote badala ya kila wakati labda Waziri na Naibu Waziri kukimbia kila mgogoro unapotokea. Kwa sababu mnafahamu Waheshimiwa Wabunge kwamba nchi yetu ni kubwa inawezekana tukashindwa kufika kote kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nimeshafika Lulindi kwa Mheshimiwa Bwanausi lakini nilienda kushughulikia kero nyingine kabisa ya korosho. Kwa hiyo, bado ni Tanzania yetu hiyo hiyo kama inaelekea kwamba utatuzi wa jumla hautaweza kushughulikia kero aliyoileta Mheshimiwa Mbunge, nipo tayari kwenda kule na labda itakuwa vilevile ni fursa ya kwenda kumalizia viporo vya korosho nilivyoviacha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea sasa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mbunge wa Kasulu Mjini, kwa niaba yake aliyejiandaa.

Na. 94

**Upungufu wa Maafisa Ardhi na Maafisa Mipango Miji Nchini**

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITILE (K.n.y MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** aliuliza:-

Miji mingi nchini inakabiliwa sana na uhaba wa Maafisa Ardhi na Maafisa Mipango Miji.

(a) Je, ni kwa nini Serikali isianzishe utaratibu wa kuajiri Maafisa hawa moja kwa moja wanapohitimu Vyuo Vikuu?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isichukue jukumu la kununua vifaa vya kupimia ardhi kama vile darubini, *GPS* na kadhalika na kuvisambaza kwenye Miji yetu ikiwemo Mji wa Kasulu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna upungufu mkubwa wa wataalam katika sekta ya ardhi na tafiti zinaonesha kwamba hadi kufikia Machi, 2016 idadi ya wataalam wa sekta ya ardhi kwa maana ya Maafisa Ardhi, Mipango Miji na Wapima Ardhi, Wathamini na Mafundi Sanifu katika Halmashauri 161 ilikuwa ni 1,087 ukilinganisha na mahitaji ya wataalam 3,040. Idadi hii ni sawa na asilimia 36 ya mahitaji kamili ya watumishi hao. Tafsiri ya mapungufu haya imekuwa ikionekana katika kiwango kidogo cha upangaji, upimaji na umilikishwaji wa ardhi iliyopimwa mijini na vijijini.

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kuajiri maafisa moja kwa moja wanapohitimu Vyuo Vikuu, Serikali imekuwa ikichukua jitihada mbalimbali ili kukabiliana na tatizo hilo. Mathalani katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2016/2017 Wizara yangu imeomba kibali cha kuajiri watumishi wapya 252 katika sekta ya ardhi. Kama kibali hicho cha kuajiri kitapatikana basi nina uhakika pengo litapungua ingawa ni kwa kiasi kidogo.

Hata hivyo nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuliona hili na nimwahidi kuwa Serikali imechukua wazo lake na pia itaendelea kulifanyia kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa vifaa vya upimaji, Wizara yangu tayari imetenga kiasi cha shilingi bilioni nane katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kununua vifaa vya upimaji ambavyo vitasambazwa katika ofisi zetu za Kanda na hata hivyo Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji ndizo zenye dhamana ya kusimamia upimaji wa ardhi kwenye maeneo yao, hivyo zinapaswa kutenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya upimaji. Aidha, katika kukabiliana na upungufu wa vifaa vya upimaji, Wizara imekuwa ikinunua vifaa vya kupimia ardhi na kuvisambaza kwenye Halmashauri kila fedha zinapopatikana.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya kutia moyo ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa migogoro ya ardhi katika Halmashauri zetu na hasa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imekuwa mingi sana, je, Serikali ina mpango gani wa kuziwezesha ofisi za Kanda ku-*speed up* utoaji wa hati ili kupunguza migogoro ya ardhi? *(Makofi)*

Sehemu ya pili, moja kati ya vitu vinavyosababisha migogoro mikubwa sana ya ardhi, hasa mijini ni uwepo wa baadhi ya watumishi wa Idara ya Ardhi wasiokuwa waaminifu katika Halmashauri zetu, watumishi hawa wamekuwa wakikaa muda mrefu sana sehemu moja ya kituo cha kazi. Je, Serikali ina mpango wowote wa kuwabadilisha mara kwa mara ili kujenga mahusiano mazuri kati ya wananchi na watumishi hao wa Idara ya Ardhi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Nditiye ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi ya Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikiwezesha Ofisi za Kanda na tuna Kanda nane na zote zinafanya kazi hiyo ya usajili kama alivyosema, pengine labda kama kuna eneo ambalo lina upungufu na kazi

hazifanyiki vizuri tungeomba kufahamu, kwa sababu ninavyofahamu mimi Kanda zote nane zinafanya kazi ya usajili na ndiyo maana tumefanya hivyo ili kurahisisha usajili katika maeneo hayo. Kwa hiyo, kama kuna sehemu kuna tatizo basi ni vizuri tukafahamu maaana lengo la Serikali ni kurahisisha na kupunguza ule muda wa kusubiri, kwa sababu sasa hivi ndani ya mwezi mmoja tunasema hati inakuwa imeshasajiliwa. Lakini kama lengo letu halifikiwi maana yake kuna tatizo mahali fulani, sasa nitashukuru sana Mheshimiwa Mbunge kama atatuambia kwamba pengine kanda hiyo ambayo anatoka yeye hakuna ufanisi mzuri katika suala zima la usajili.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anasema uwepo wa watumishi wasio waaminifu na wa kukaa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni azma ya Serikali kuona kwamba watumishi wanapokuwa katika maeneo wanafanya kazi zao kwa uadilifu na weledi mkubwa kama ambavyo dhamana hiyo wamepewa. Lakini pale inapotokea pengine mtumishi amekaa eneo moja muda mrefu na amekuwa mzoefu kawa kama ni mwanakijiji katika eneo lile au ni mwanamji wa pale na ameshindwa kufanya kazi aliyoifanya, basi tutawasiliana na Wizara husika ili tuweze kuona nini cha kufanya. Kwa sababu kumhamisha pale kama ameshindwa kufanya kazi na kumpeleka eneo lingine unakuwa hujamsaidia, kama ana tatizo kubwa basi tujue tatizo lake ni nini ili hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa. Pengine kuwahamisha tu inaweza ikawa siyo *solution,* lakini kikubwa ni kujua madhaifu yake ni nini ili tuweze kuona hatua za kinidhamu kuweza kumchukulia mtumishi kama huyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa David Silinde.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA**: Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru kwa nafasi, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa utendaji mbovu na kutokuwajibika kwa watendaji wa ardhi waliopo kwenye Halmashauri kunachangiwa pia na muundo mzima kwamba watendaji wale hawapata *order* wala maelekezo kutoka kwenye Serikali Kuu kwa maana ya kwenye Wizara, na hasa wanapokosea inakuwa ni vigumu kwa Waziri kutoka juu kumchukulia hatua kwa sababu anasikiliza sana kwenye Halmashauri.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa, kwa unyeti wa Wizara hii na kuondoa migogoro ndani ya nchi yetu kuhakikisha kwamba watendaji wote wa ardhi wanapokea *order* kutoka juu na hata wanapokosea waweze kuchukuliwa hatua kutoka juu ili kuondoa migogoro ndani ya nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, utendaji mbovu wa watumishi hasa kwenye sekta ya ardhi nadhani siyo suala tu pia la kujua kwamba anapokea *order* kutoka mamlaka ipi. Ni kweli katika ule mlolongo uliopo pengine unaweza ukaliona hivyo, lakini nia ya Serikali kugatua madaraka na kusogeza huduma katika Halmashauri zetu ilikuwa ni nia njema na dhamira ya dhati ya kutaka kuona kwamba huduma zile zinafanyika kwa wakati mahali ambapo watu wanahitaji.

Mheshimiwa Spika, lakini hili kama limekuwa ni tatizo, nadhani suala la msingi ni ndani ya Serikali kuweza kuona namna ya kuweza kudhibiti udhaifu huu au utendaji huu mbovu uliopo ili tuweze kujua kwamba hapa kinachotakiwa kufanyika, kama mtumishi ambaye anafanya

utendaji wake katika viwango visivyostahili na akitarajia tu kabisa kwamba mamlaka yenye sauti kwake ni mamlaka fulani, hilo halimfanyi yeye asamehewe katika kosa alilolifanya.

Kwa hiyo tunachosema, ugatuaji wa madaraka ilikuwa ni kusogeza huduma, lakini kama suala la kitaaluma au suala la kitendaji linaonekana lina ugumu katika namna ya kudhibiti watendaji hawa, nadhani ni suala la kuongea kati ya Wizara zote mbili husika tukajua ni jinsi gani watu hawa tutaweza kuwasimamia vizuri zaidi ili wafanye kazi zao kwa weledi.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Pamoja na uhaba wa Maafisa wa Ardhi na uhaba wa fedha, lakini zoezi la kupima ardhi nchini limekuwa likisuasua na mahitaji ya wananchi kujenga yamekuwa yakiongezeka, kwa hiyo ukiangalia katika hali ya kawaida wananchi wengi wamekuwa wakijenga katika maeneo ambayo hayajapimwa, sasa nataka kauli ya Serikali, ipi ni kauli ya Serikali juu ya wananchi wote wanaojenga katika maeneo ambayo hayajapimwa na Serikali bado inasuasua kwenye kupima maeneo hayo ya ardhi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kasi ya wananchi kujenga ni kubwa kuliko *speed* ya Serikali katika kupima maeneo, na ni maeneo mengi ambayo kwa sasa yamekaliwa katika mpangilio usio sahihi na ndiyo maana Wizara imeliona hili na tukaja na programu ile ya miaka mitano ya kuhakikisha kwamba wale ambao wamekuwa na *speed* kali kuliko Serikali tunajaribu kurasimisha maeneo yao ili wakae katika utaratibu mzuri waweze kutambuliwa na Serikali iweze pia kupata kodi zake kupitia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kuona hili pia tunalifanyia kazi, Serikali imesajili makampuni, ina makampuni karibu 55 ambayo yanafanya kazi ya upimaji katika maeneo, na upimaji wao wanaofanya wanafanya kulingana na mipango iliyoko katika maeneo hayo kwa maana ya ile mipango miji kwenye yale maeneo, *masterplan* zao ambazo wameziweka pale.

Kwa hiyo kikubwa tunachosema, kasi ya wananchi ni kubwa, Serikali ina *speed* ndogo na eneo lililopimwa ni dogo, kwa hiyo tunaomba Halmashauri zilizotayari ziyatumie haya makampuni ambayo tumeyabainisha katika suala zima la upimaji, na nilisema pia wakati najibu swali hili tarehe tisa, nikasema orodha tayari tunayo, Halmashauri yoyote iliyo tayari tuwasiliane ili tuwape ile orodha waweze kufanya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, lengo letu ni kuhakikisha Miji imekaa vizuri na imepangika na tunawaomba wananchi, tunawasihi wasianze kuvamia maeneo ovyo sasa hivi kwa sababu kadri tunavyozidi kuweka mikakati ndivyo jinsi ambavyo wao watakuwa katika hatua nzuri ya kuweza kupangiwa maeneo yao, kwa hiyo wasikimbie sana kwa sababu tayari kama Wizara tunaamua kufanya kazi hii kwa weledi mkubwa.

Na. 95

**Shamba la Mkongo – Hale**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI** aliuliza:-

Shamba la Mkonge la Hale Mwakinyumbi lilimilikiwa na *Chavda Ltd.* lakini Serikali ililitoa shamba hilo kwa wananchi wa Hale kwa matumizi yao lakini hulimwa huku wakiwa na wasiwasi kila wakati.

Je, kwa nini Serikali isiwakabidhi rasmi wananchi wa Hale shamba hilo ili wawe na utulivu wanapoendelea na shughuli zao za kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali namba 95 la Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Mwakinyumbi ni shamba linalomilikiwa na Kampuni ya *Mwakinyumbi Sisal Estates Ltd.* ya *M/s Chavda.* Bwana Chavda alinunua shamba hili kwa Mamlaka ya Mkonge Tanzania wakati wa awamu ya kwanza ya ubinafsishaji wa mashamba ya mkonge mwaka 1985 na 1988.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ubinafsishaji sehemu ya shamba hili lilitolewa kwa wananchi wa vijiji vya Mwakinyumbi Stesheni na Hale kwa ajili ya makazi na kilimo cha mazao ya chakula. Shamba hili limeacha kuzalisha tangu mwaka 1994 baada ya kutelekezwa na mmiliki.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 20 Julai, 2016 nilifanya ziara Mkoani Tanga na katika ziara hiyo nilitembelea mashamba ya Mwakinyumbi, Magunga, Magoma na Kwashemshi yaliyopo katika Wilaya ya Korogwe. Katika kulikagua shamba la Mwakinyumbi, tulibaini kuwa shamba hili limevamiwa na wananchi na taasisi mbalimbali kwa shughuli za kilimo na uchimbaji kokoto.

Mheshimiwa Spika, tayari Wizara yangu ilishatoa maelekezo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kuanza utaratibu wa ubatilisho wa miliki hiyo. Hata hivyo, katika kutekeleza maelekezo haya mnamo tarehe 5 Agosti Halmashauri ilituma ilani ya siku 90 ya kusudio la kufuta miliki ya shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, ili wananchi wa Korogwe waweze kukabidhiwa sehemu ya shamba hilo rasmi kupitia Halmashauri yao, taratibu za ubatilisho lazima zikamilishwe. Ninatoa rai kwa wananchi wa Korogwe kuwa na subira wakati Serikali inashughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, nitoe rai pia kwa Halmashauri zote nchini kuendelea kuainisha mashamba pori na viwanja vilivyotelekezwa ili mchakato wa kisheria wa kufuta milki zake ufanyike kwa wakati na kuondoa migogoro inayozidi kushamiri siku hadi siku.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana yenye matumaini kwa wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini, pia nimpongeze kwa safari alizofanya katika Jimbo langu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Naibu Waziri umefika na kuliona shamba hili ambalo limetelekezwa zaidi ya miaka 22, ni kwa nini sasa Serikali isiwakabidhi wananchi wakalitumia kwa shughuli zao mbadala? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa mashamba mengi yamechukuliwa mikopo kwenye mabenki na sasa hivi yametelekezwa, nini kauli ya Serikali kwa yale mashamba ambayo yalichukuliwa mikopo, hayaendelezwi na yametelekezwa mpaka muda huu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anataka kufahamu ni lini Serikali itakabidhi sasa wananchi hao mashamba hayo ambayo yametelekezwa muda mrefu ili waweze kuyatumia.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, ni kwamba utaratibu ili uweze kumnyang'anya mtu huyu ni lazima ule utaratibu wa kisheria ufwatwe, na ndiyo maana nimesema katika hatua za awali ambazo Serikali imechukua ni kutoa *notice* kwa hawa ambao wametelekeza mashamba na siyo huyo mmoja tu, yapo mashamba zaidi ya 22 ambapo baada ya ziara yangu wamepewa *notice*.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba taratibu za Serikali zinaendelea, muda ule ukishakwisha ni jukumu la Halmashauri husika kuweza kupendekeza kwa Mheshimiwa Waziri ili na yeye aweze kumshauri Rais kubatilisha, ni lazima ule mchakato wa kisheria utimizwe. Kwa sababu wenzetu wa Korogwe wameshaanza nina imani litafikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anasema mashamba mengi yamekuwa mapori lakini pia inafahamika kwamba mengine yamechukuliwa mikopo mabenki na nini sasa Serikali inasema nini.

Mheshimiwa Spika, niseme haya yamekuja kuahamika na kuthibitika rasmi baada ya Wizara yangu kuanza kutoa ilani kwa wale ambao wameyatelekeza mashamba yao, lakini kama Serikali tunachofanya sasa ni kuhakikisha tunafanya kazi sambamba na mabenki ili fedha za umma zisipotee, kwa sababu dhamana za hati zile zimewekwa na zimechukuliwa mikopo, lakini pengine mikopo ili haikwenda kunufaisha katika yale maeneo.

Kwa hiyo, jukumu letu sisi tunalofanya, pamoja na ilani zinazotolewa katika mashamba haya, lakini bado kama Serikali tunafanya kazi kwa karibu sana na mabenki ili kuhakikisha kwamba kama zile dhamana walizokuwa wameweka pengine zinakwenda kubatilishwa sasa tujue ni namna gani yale mabenki yataweza kupata pesa zake. Kwa hiyo hili tunalifanya kwa uangalifu ili kuona kwamba pesa za Umma hazipotei lakini pia haki ya wananchi au ya wamiliki wale pia inakwenda sambamba kisheria ili tusijikute kwamba tumekwenda nje ya utaratibu. *(Makofi)*

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa suala la mashamba ya mkonge kwa upande wa Korogwe Vijijini inafanana na Korogwe Mjini, na kwa kuwa Korogwe Mjini tayari ilishaingia kwenye mpango kabambe wa *masterplan,* na kwa kuwa mji huu una mashamba ya mkonge nayo ambayo hayaendelezwi na tayari tulishaleta mapendekezo ya kuomba mashamba hayo yafutwe.

Je, Serikali inatuambiaje na hasa ikizingatia kwamba tupo kwenye ule mpango kabambe wa *masterplan* kuhakikisha kwamba mashamba hayo yanafutwa ili maeneo hayo yaweze kutumika katika huu mpango kabambe ambao umeandaliwa?

**SPIKA:** Majibu mafupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hayo mashamba ambayo tayari wao wameleta mapendekezo kwa Waziri ili na yeye aweze kumshauri Rais ayabatilishe ni yale pia katika mchakato ambayo pengine tunasema kwamba kuna maeneo mengine ambapo wamekopea pesa benki.

Kwa hiyo, mchakato unafanyika ili kuweza kujua, na pale pale tunaangalia ile ilani ambapo kama imekwenda sawasawa kisheria, kwa sababu mashamba ni mengi na yote yanahitaji pia umakini katika kuyabatilisha.

Kwa hiyo, tusingependa kutoa ushauri ambao pengine unaweza ukampotosha Mheshimiwa Rais akaja akalaumiwa, tunataka kujiridhisha na masharti yote yaliyopo pale kama yamezingatiwa lakini pia na kuangalia fedha za Umma zisije zikapotea kwa sababu tu hawa watakuwa wamebatilishiwa umiliki wao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hilo tunalifanyia kazi na nimwahidi Mheshimiwa Mbunge tutakwenda kuiangalia orodha ya mashamba ambayo anayasema tuweze kuona yamefikia katika utaratibu gani ili hatua nyingine ziweze kuendelea.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niulize swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyopo huko Korogwe yanafanana sana na matatizo yaliyopo katika Jimbo la Itigi; kuna shamba lililokuwa la Shirika la *Tanganyika Packers* lipo katika eneo la Kitaraka, lilitelekezwa na shirika hili baada ya shirika hili kufilisika mwishoni mwa miaka ya 1980.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa maeneo yale katika vijiji vya Kitaraka, Kaskazi Stesheni, Doroto, Majengo, Tambukareli, Kihanju na Sanjaranda wamelitumia shamba lile kulima na linawasaidia sana kupata mahitaji yao ikiwemo mazao ya chakula pamoja na mazao ya biashara, lakini kuna taarifa kwamba Serikali ina mpango wa kulibinafsisha shamba lile kwa wawekezaji.

Je, ni nini kauli ya Serikali kwamba haitaonesha inaleta mgogoro na wananchi ambao shamba lile sasa linawanufaisha wananchi wengi sana wazawa na wananchi wa nchi hii kuliko kuweka mwekezaji, ni nini kauli ya Serikali juu ya suala hilo?

**SPIKA:** Majibu mafupi ya swali hilo la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokizungumza kwamba wananchi wamekuwa wakilitumia lile shamba na ametaja vijiji vinavyohusika. Naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali ni njema na kama kuna hatua ya kuweka mwekezaji vilevile pia itakuwa ni kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, tunachotaka afahamu ni kwamba Serikali haiko pale kunyang'anya wananchi ardhi na kuwaacha wakiteseka. Kitakachofanyika ni kwamba watakaokuwa wa kwanza kufikiriwa ni wale wananchi walioko pale na kwa sababu shamba lile lilikuwa linamilikiwa na Serikali tangu awali kwa maana hiyo Serikali kulipangia matumizi mengine ni sahihi. Tutakachofanya kabla halijapewa mwekezaji lazima yale maridhiano ya awali katika kukubaliana namna ya kuweza kufanya ile kazi yaweze kukubalika kwa sababu wao pia wanatambua hawako pale kihalali kulingana na umiliki wa shamba lile.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha, naendelea kuwatambulisha sasa wageni, nitaanza na jukwaa la Spika…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane hasa upande wangu wa kulia huku kelele ni nyingi sana.

Wageni tulionao kuanzia na jukwaa la Spika, tunaye mgeni maalum kwa siku ya leo, naye si mwingine bali ni Mkurugenzi mpya wa Idara ya Usalama wa Taifa, Dkt. Modestus Kipilimba. Dkt. Kipilimba tunakukaribisha hapa Bungeni na kwa niaba ya Wabunge wote tunakupongeza sana kwa uteuzi wako wa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa. Tunakutakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yako na sisi kama Bunge tunakuahidi ushirikiano wa kutosha kila pale ushirikiano wetu utakapohitajika, karibu sana Dodoma. Pia niwakaribishe Maafisa uliofuatana nao. *(Makofi)*

Wageni walioko Bungeni ni wengi nitawataja kwa haraka haraka. Wageni 10 wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Mtakatifu *Jordan* kilichoko Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni mmoja wa Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambaye ni Afisa kutoka ofisi ya CHADEMA Taifa. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Selemani Jafo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kutoka Chuo cha Ufundi *VETA,* Mkoani Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Ernest Maranya, Mgunduzi wa kifaa cha elimu ya mfumo wa jua na sayansi ya anga za juu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Bonnah Kaluwa ambao ni Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kutoka Mkoa wa Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Mariam Machicha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni Madiwani wawili, Watendaji watatu na Makada wa CCM kutoka Vwawa, Mkoa wa Songwe wakiongozwa na Ndugu Agripa Mwashambwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Marwa Chacha ambaye ni Diwani wa Kata ya Rung'abure kutoka Serengeti, Mkoa wa Mara, Mheshimiwa Elias Merengo. Karibu sana kutoka Rung'abure. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Musa Ntimizi ambao ni wanafunzi wenzie aliosoma nao *O-level,* Shule ya Sekondari Jitegemee kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Edward Mwalongo ambao ni wataalam wa elimu ya ujasiriamali kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambao ni vijana kutoka Dayosisi ya Kanisa Anglikana lililopo Ngara Mkoa wa Kagera. Naona ninyi ndiyo mmetoka mbali kuliko wageni wote, karibuni sana kutoka kule Ngara. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Zainab Bakar ambao ni familia yake kutoka Pemba, Mkoa wa Kusini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Miza Haji ambao ni watoto wake kutoka Unguja, Mkoa wa Kaskazini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ezekiel Maige ambao ni Viongozi wa Vijana wa Kanisa la *TIFC* kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambaye ni mkulima kutoka Wilaya ya Mbulu, Mkoa wa Manyara. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Hassan Kaunje ambao ni Viongozi wa Wazalishaji wa Chumvi Tanzania kutoka Mkoa wa Lindi. Karibuni sana ndugu zangu kutoka Lindi. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake kule Bagamoyo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 24 kutoka Taasisi ya *Tanzania Role Model* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Tanzania *Role Model. (Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambaye ni Ndugu yake kutoka Ushetu Mkoani Shinyanga. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Aeshi Hilaly ambao ni wawekezaji kutoka nchini Malaysia. *Our guest from Malaysia, wherever you are, you are welcome.* Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya wageni yameishia hapo sasa tunaendelea na matangazo ya kazi za leo. Naomba tuendelee kusikilizana matangazo haya ni muhimu. Waheshimiwa Wabunge tutafakari taratibu, tumezidi sana kupiga kelele humu ndani.

Naomba niwakumbushe leo Alhamisi, tarehe 15 Septemba, 2016 kutakuwa na semina muhimu sana kwa Wabunge wote saa 7.00 mchana Ukumbi wa Msekwa kuhusu dhana ya bima ya afya na utaratibu wa upatikanaji wa huduma za matibabu kwa Wabunge lakini pia uhamasishaji wa mkakati wa ugharamiaji wa huduma za afya kwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, semina hii itafanyika katika ukumbi wa Msekwa kama nilivyosema kuanzia saa 7.00 mchana, Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria. Semina hii ni muhimu sana kwa sababu masuala ya afya ni muhimu sana kwenu kuyaelewa kama Wabunge lakini pia kuelewa ni namna gani ambavyo mambo haya yatahusisha wapiga kura wetu

majimboni kwetu. Kwa hiyo, nawaomba sana saa 7.00 mchana tukitoka hapa twende katika semina hii.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazie kwamba mlipitisha Azimio kwamba mtasamehe posho ya siku moja kwa ajili ya mchango wa wahanga wa tetemeko la ardhi Kagera. Nafurahi kuwajulisha kwamba michango yenu jumla yake imekuwa ni Sh. 85,580,000 na fedha hizo zimekwishawasilishwa kwenye akaunti husika. Nawashukuru sana, tuendelee na moyo huo kila majanga ya namna hii yanapotokea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Mwenyekiti wa ibada kwa Wabunge wote wa Makanisa ya *CCT* anaomba Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni Wanachama wa *CCT* kuhudhuria ibada katika jengo la Pius Msekwa, ghorofa ya pili, leo siku ya Alhamisi mara baada ya Bunge kuahirishwa saa 7.00 mchana.

Matangazo yameishia hapo. Kuna wageni watano wa Mheshimiwa Zainab Bakar ambao ni familia yake kutoka Pemba, Mkoa wa Kusini, sikuwatangaza?

**MBUNGE FULANI:** Uliwatangaza.

**SPIKA:** Niliwatangaza. Kabla hatujaendelea kuna lolote? Hakuna, kwa hiyo…

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mwongozo wa Spika

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 68(7), naomba nisiisome. Napenda tu kusisitizia neno ambalo mara nyingi limekuwa likitumika kimakosa na neno lenyewe ni wahanga. Nilishawahi kulizungumza siku za nyuma, tunaposema wahanga wa tetemeko la ardhi kule Mkoani Kagera hatuwatendei haki kwa sababu hawakujitoa mhanga kwa ajili ya tatizo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitizie hili neno waathirika wa tetemeko la ardhi na siyo wahanga. Wahanga ni pale mtu anapojitoa iwe kwa namna moja au nyingine kwa nia njema kwa lengo la kuokoa wengine au hata kama kwa nia mbaya. Mfano, magaidi wamekuwa wakijitoa mhanga na kwenda kuua watu wengine. Kwa hiyo, yule anayejitoa na kwenda kuwaua wenzake ni mhanga lakini wale wanaokufa katika lile tukio wanakuwa ni waathirika. Kwa hiyo, naomba neno hili litumike ipasavyo ni waathirika na siyo wahanga, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani hilo halina tatizo, ametusaidia kutuweka sawa Kiswahili. Asichokijua Mheshimiwa Amina Mollel ni kwamba sisi wengine tulijifunza Kiswahili tulipoingia darasa la kwanza kabla ya hapo tulikuwa hatujawahi kusikia Kiswahili kabisa. Mimi miaka saba ya mwanzo nilikuwa najua Kigogo tu nilifikiri dunia yote wanaongea Kigogo basi. Kwa hiyo, lugha yoyote ukijifunza ukubwani unaendanayo taratibu kidogo. Tunakushukuru sana kutuongoza Mheshimiwa Amina Mollel katika hilo na wataalam wangu na ninyi mtakuwa mme-*note* ili wakati mwingine tutumie vizuri kati ya neno wahanga na waathirika. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii, naomba nimwite Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ili aweze kuendelea na ratiba yetu.

*Hapa (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna nyongeza ya wageni wa Mheshimiwa Hamida anaitwa Hiteshi Meta mume wake, Jamila Mohamed dada yake na Hafidh Omar Said shemeji yake. *(Makofi)*

Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2016**
***(The Tanzania Agricultural Research Institute Bill, 2016)***
**Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa Mwaka 2016**
***(The Tanzania Fisheries Research Institute Bill, 2016)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, naanza na Mheshimiwa Hasna Mwilima ajiandae Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nishukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hii Miswada miwili kwa maana ya Muswada wa mambo ya uvuvi lakini pia na Muswada wa masuala ya kilimo. Naomba nijikite kwenye huu Muswada wa Uvuvi kwa sababu kwenye Jimbo langu tunalo Ziwa Tanganyika na limekuwa maarufu sana kwa kutoa samaki anayeitwa mgebuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye hii taarifa yake aliyotoa, kwenye mambo muhimu ya Muswada huu kuna kipengele hapa kinasema kuweka utaratibu na kumbana mtafiti anaposhindwa kuwasilisha taarifa ya mwisho ya utafiti. Siku za nyuma tulikuwa na Kampuni ya Wagiriki iitwayo YOROGWE ilifanya kazi ya utafiti na ilikuwa inavua samaki kwa kutumia meli zile kubwa. Ziwa Tanganyika lina kina kirefu sana duniani lakini ninachojaribu kusema…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge na wale mnaotoka basi mtoke kwa utaratibu wa kutokufanya zogo ndani ya Bunge.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kigoma wale ambao wamezungukwa na ziwa hili kwa maana ya Jimbo la Kigoma Kaskazini, Jimbo la Kigoma Kusini na Jimbo la Kigoma Mjini wanashindwa kuvua samaki walio wengi kwa sababu zana zao za uvuvi haziwafai kwenda chini zaidi. Hii Kampuni ya Wagiriki ambayo ilikuwa inatwa YOROGWE wakati inavua Kigoma wale samaki walikuwa hawaishi kwa sababu walikuwa wanatumia zana zenye hadhi ya kuvua samaki kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba tunaweka sheria hii na na-*support* kwamba utafiti wa kina uweze kufanywa, lakini Wizara iwe inahakikisha hawa watu wanapofanya utafiti wawe wanatoa taarifa pia kwenye Halmashauri husika zinazozunguka hilo Ziwa Tanganyika. Kwa mfano, kwenye miaka ya 2000 tumekuwa na wenzetu hawa wa *FAO* ambao waliwahi kufanya utafiti na wakatoa taarifa kwamba Ziwa Tanganyika lina aina ya samaki zaidi ya 250.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuulizane ukizungumzia Ziwa Victoria unazungumzia sato na sangara lakini sangara ametolewa Ziwa Tanganyika. Walifanya utafiti, wakamchukua sangara kutoka Ziwa Tanganyika wakampeleka Ziwa Victoria na hatimaye ndiyo wakampa jina la sangara. Sangara ni jamii ya singa na nonzi kutoka Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ikilitumia vizuri Ziwa Tanganyika kupitia Wizara ya Kilimo na Mifugo tunaweza kuingiza kipato cha Taifa kwa kuvua samaki wengi walioko kwenye ziwa hili. Hata hivyo, kinachoonekana bado Wizara haijajipanga vizuri kutumia mazao haya ya uvuvi kwenye Ziwa Tanganyika ili kuiingizia kipato Serikali yetu. Kwa hiyo, tunapitisha Muswada huu mzuri lakini pia tuweke taratibu za kuwabana watafiti watakaofanya utafiti kwenye maziwa yetu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo maana nikitaja tu samaki tunaowavua kwenye Ziwa Tanganyika kwa kutumia zana zetu hizo hizo ambazo siyo bora, tuna samaki ambaye anaitwa babukubwa, kuhe, nonzi, sangara, singa, kibonde, kavugwe, kuku maji, mibanga, jamani tuna zaidi ya samaki 30 wanavuliwa na wavuvi wa Kigoma kwa kutumia zana ambazo hazina tija. Je, Serikali ikiweka nguvu, ikawapa wavuvi zana ambazo zina tija tutavua samaki wangapi kwenye Ziwa Tanganyika? Tutaingiza shilingi ngapi katika Taifa letu? Sisi tumepakana na Zambia, Burundi na Kongo na mazao haya ya samaki na dagaa tunakwenda kuuza Kongo, Burundi, Rwanda na Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilimsikia mchangiaji mmoja kama sikosei Mheshimiwa Haonga alikuwa anazungumzia namna ambavyo dagaa wa Ziwa Viktoria wanavyopelekwa Kongo. Sasa fikiria mpaka dagaa wa Ziwa Viktoria wanaenda Kongo. Kwa hiyo, ninachojaribu kuomba hapa ndugu zangu ni kwamba tuweke akili yetu yote kwenye mazao ya uvuvi. Nimepitia taarifa ya Kamati nimeona imejikita kwenye Muswada wa Kilimo tu haijajikita kwenye Muswada wa Uvuvi. Sasa nikapata shida, hivi kilimo ndiyo kinaingiza zaidi mapato kushinda zao la uvuvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba katika utafiti huu tusijikite tu kwenye utafiti wa kilimo tujikite pia na kwenye utafiti wa zao la uvuvi. Kwa mfano, sisi watu wa Kigoma tunao mwalo pale Mwakizega. Tumejenga mwalo mzuri na Halmashauri sasa hivi inaendelea kuumalizia japo wavuvi wameshaanza kuutumia ili angalau kupandisha hadhi mazao yao ya dagaa na samaki waweze kupata kipato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachoomba Serikali itupie jicho la huruma kwenye majimbo haya matatu, Jimbo la Kigoma Kusini, Kaskazini na Mjini ili kuwawezesha wavuvi wetu kwa zana zenye ubora zaidi ili waweze kuzitumia kuvua samaki wengi na kuongeza kipato cha Halmashauri zetu lakini pia kipato cha nchi maana tunawatoza ushuru. Kwa mfano, gunia moja la dagaa, wavuvi wanalipa Sh.3,000 mara wavuvi waliopo ni shilingi ngapi, ni pesa nyingi. Hizi ni *own source* zinazoingia kwenye Halmashauri zetu na sisi tunazielekeza kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili nichangie pia kwenye upande wa Muswada wa Kilimo. Niunge mkono taarifa ya Kamati ya kutoa pendekezo lao la uanzishwaji wa Mfuko Maalum wa Utafiti wa Kilimo. Nimekuwa Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba, Newala na Mtwara, Naliendele hawana tu uwezo wa kutafiti zao la korosho bali wanafanya utafiti wa mazao yote, lakini tatizo kubwa hapatengwi pesa za kutosheleza ili hizi tafiti ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aweze kutuambia pendekezo hili la Kamati la kuanzishwa Mfuko Maalum wa Utafiti wa Kilimo amelichukuliaje ili kuwezesha upatikanaji wa fedha zaidi za utafiti. Kwa sababu Naliendele na taasisi zote za utafiti Tanzania zikiweza kutengewa pesa zitafanya kazi kubwa na nzuri ya kufanya utafiti wa mazao mbalimbali nchini ili wakulima wetu waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia pale Kilimanjaro Hai, tunayo *TACRI* ambao ni watafiti la zao la kahawa. Nikiwa pale kama Mkuu wa Wilaya nilichojifunza Serikali haitengi pesa ya kutosha kuipa taasisi hii ya utafiti ya *TACRI*. *TACRI* inategemea ufadhili wa *European Union,* ukiwa pale unakuta unapokea Mabalozi wa *European Union* wanakuja kuangalia uendelezaji wa *TACRI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, hivi hawa *European Union* wakitoa mkono wakasema kwamba hawasaidii tena ile *TACRI* itaendelea? Kwa hiyo, ninachojaribu kuomba taasisi hizi za utafiti zitengewe pesa zisiwe zinatupwa au zinawekwa pembeni. Wizara inapokuja hapa kwenye bajeti ijayo iweze kuona namna ya kuwezesha taasisi zetu hizi za utafiti ili ziweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pale Kigoma tunao hawa *TAFIRI* na wanaendelea na utafiti wao wa kuonesha tuna idadi ngapi ya samaki kati ya wale 250. Hata hivyo, *TAFIRI* hawa wamekuwa wanafanya kazi Kigoma Mjini, tuombe basi Wizara ione namna ya kujenga hata chuo kimoja cha utafiti ndani ya Mkoa wa Kigoma hata kama ni *branch* ya utafiti kwenye zao la uvuvi ili vijana wetu waweze kujifunza zaidi masuala ya uvuvi, waachane na uvuvi haramu na wafanye uvuvi halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, niseme Miswada hii miwili wa Uvuvi na wa Kilimo ni mizuri na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ajiandae Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema na kuwepo katika kikao cha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi kwanza napenda niipongeze Serikali yangu na Wizara husika kwa kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania 2016. Kwa nini nalazimika kuipongeza Serikali na Wizara? Ni kwa sababu nafahamu Muswada huu unalenga kuendeleza, kuongeza na kuboresha uelewa wa wakulima wetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu yamezungumzwa mambo mengi katika kufanya utafiti. Naomba nijikite kwenye suala la utafiti wa mbegu bora. Waheshimiwa Wabunge wengi jana wakati wanachangia wameeleza sana uwepo na mbegu bora za mazao ya chakula na biashara. Mimi mwenyewe nimewahi kutumia mbegu za mahindi ambazo zinaletwa na haya mashirika mbalimbali, cha kushangaza nilipanda kama heka 10 lakini shamba lote mahindi hayakuota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inawezekana jambo hili lilinigusa mimi lakini pia liliwagusa wakulima wetu, mambo kama haya kwa kweli yanakatisha tamaa. Kwa hiyo, binafsi naamini kwa kupitia taasisi hii ambayo itafanya utafiti tutakuwa na mbegu bora. Miongoni mwa vitu ambavyo mimi binafsi nasisitiza ni kupatikana kwa mbegu bora ambazo hazitakatisha tamaa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutokuwa na mbegu bora maana yake tunawafanya wananchi wetu waendelee kutunza mbegu zile kwa teknolojia ambazo zimepitwa na wakati labda kwa kufutika mbegu kwenye moshi ili mwaka mwingine ikasaidie. Kwa karne hii ambayo tunakwenda nayo binafsi naona sio jambo jema. Kwa hiyo, nasisitiza sana katika eneo hili la utafiti tuzingatie upatikanaji wa mbegu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na jambo hilo pia naomba nisisitize suala la uhifadhi wa mazao. Wakulima watalima mashamba, watapanda mbegu na hatimaye watavuna. Katika eneo hili, wakati wakulima wetu wa mazao ya biashara na chakula wanasubiri soko mara nyingi Serikali imekuwa ikiwasisitiza wasiuze mazao yao. Katika kipindi kile ni wajibu wetu sasa kuwaelimisha njia bora ya uhifadhi wa mazao ili viwango na ladha ile isipotee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu nimeshuhudia tumekuwa tukiunda Bodi mbalimbali lakini mara nyingi hatuzisimamii. Mfano mzuri ni Bodi ya Korosho. Hivi karibuni tumefanya kikao cha wadau wa korosho Bagamoyo, kwa bahati nzuri Waziri mwenye dhamana alikuwa mgeni rasmi katika kikao kile, alizungumzia masuala mengi na changamoto zilizopo kwenye Bodi na Mfuko ule wa Wakfu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mwenyekiti wa Bodi amepata fursa ya kujibu maelezo ambayo mgeni rasmi aliyaeleza, alimwomba Waziri kwamba siyo vizuri kusubiri mikutano ya wadau, ni vizuri Wizara iwe inashirikiana moja kwa moja na Bodi katika kutatua changamoto zilizopo na kutoa ushauri. Kwa hiyo, nasisitiza katika jambo hili kwamba tunapounda hizi Bodi ni wajibu wetu kuzisimamia ili kubaini changamoto zilizopo na kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu pia tumezungumzia masuala ya uundaji wa Bodi na upatikanaji wa Wajumbe. Kwenye ile Bodi tumezungumzia upatikanaji wa wakulima kuwa wawakilishi kwenye Bodi. Kamati imependekeza kwamba kuwepo na wakulima wawili badala ya mkulima mmoja kama ulivyopendekeza Muswada. Hata hivyo, dada yangu Mheshimiwa Sakaya wakati analijadili hili na mimi binafsi nilipenda sana mchango wake alizungumzia kuhusu hizi Bodi na alifika mbali, alipendekeza kwamba Bodi hizi ni vizuri zikaenda Kikanda. Binafsi nilishawishika lakini baadaye nilipata shida nikasema tunaweza tukafika mahali tukaweka kikanda lakini kila kanda ina mazao mchanganyiko hatma yake tunaweza tukafika mahali sasa kila mwakilishi wa zao aingie kwenye Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nikubaliane moja kwa moja na mapendekezo ya Kamati kuwa badala ya yule mjumbe mmoja aliyependekezwa kwenye Muswada basi kuwepo na wajumbe wawili wakulima ambao wataingia kwenye hii Bodi. Sote tunafahamu kwamba kidole kimoja hakivunji chawa kwa kuingia wakulima wawili kutasaidia kutatua changamoto zilizopo. Hata hivyo, kubwa zaidi naomba tuangalie sifa za wale wakulima ambao wata…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Frank Mwakajoka na Mheshimiwa Chuachua ajiandae.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nichangie Muswada huu. Muswada huu umekuja kipindi muhimu sana lakini tunachotaka kukizungumza sisi kama Watanzania ni lazima tubadilike sana katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza wajibu wetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti mbalimbali zimekuwa zikifanywa katika nchi hii lakini tatizo kubwa ni kwamba zikishafanyika zinawekwa katika makabati haziwafikii wananchi na hata siku moja hawajaona ni namna gani tafiti hizi zimewasaidia. Ndiyo maana ukiangalia sasa hivi utaona wakulima wetu hawajui walime nini katika maeneo yao kwa kuongozwa na hawa watu ambao wamefanya utafiti. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali tunapokuwa tumepitisha Miswada hii na kuwa sheria ni lazima zianze kufanya kazi tena kwa vitendo kabisa.

Mheshimiwa mwenyekiti, nilikuwa najaribu kupitia Muswada huu na niliangalia baadhi ya maeneo ambayo nataka kuchangia sasa hivi lakini sijaona sehemu ambayo Msajili wa Hazina ametajwa. Jambo hili limenisikitisha kwa sababu ukisoma Sheria za Msajili wa Hazina zinaonesha kwamba Msajili wa Hazina ndiye mtu pekee ambaye anasimamia mashirika pamoja na taasisi mbalimbali ambazo zinaanzishwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza katika sheria hii sijaona inataja Msajili wa Hazina anahusika kuyasimamia mashirika pamoja na taasisi ambazo zinaanzishwa. Naomba sheria zote zinazotungwa sasa hivi zimtaje Msajili wa Hazina kama ndiye msimamizi mkuu wa mashirika na taasisi mbalimbali zinazoanzishwa katika nchi hii. Nia na madhumuni ni kumpa nafasi kubwa Msajili wa Hazina kuhakikisha kwamba anasimamia mashirika au taasisi hizi ambazo zinakwenda kuanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona liko tofauti ni uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi, inaonesha kwamba Mheshimiwa Rais ndiye atachukua jukumu la kumteua Mwenyekiti wa Bodi lakini tumeona mashirika na taasisi mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais ameteua Wenyeviti hawa 90% ni wazee ambao walikuwa wameshastaafu na leo wamerudishwa kazini. Kwa hiyo, wanapata nafasi hizi kama vile fadhila kutoka kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaomba sasa uteuzi huu wa Mwenyekiti wa Bodi ni lazima Mheshimiwa Rais ashauriane na Msajili wa Hazina ili Msajili wa Hazina aweze kumsaidia Mheshimiwa Rais ni namna gani anaweza akapata Mwenyekiti wa Bodi ambaye anaweza kuisaidia Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sasa hivi unaona mashirika na taasisi nyingi zinakufa na hazifanyi kazi ipasavyo kwa sababu watu wanaoteuliwa kwa kweli ni wazee na ambao hawawezi kutoa mawazo mazuri na wakafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, tunashauri sheria hii ifanye mabadiliko na kuhakikisha kwamba wakati Mheshimiwa Rais anamteua Mwenyekiti wa Bodi lazima ashirikiane na Msajili wa Hazina ili kuboresha uteuzi huo tupate Mwenyekiti wa Bodi bora na anayeweza kusaidia taasisi au shirika kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona mashirika mbalimbali ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akiteua Wenyeviti wa Bodi ufanisi wake umekuwa ni mdogo sana. Kwa hiyo,

tunaomba sana *TR* aweze kushiriki kwa 90% katika uteuzi wa viongozi mbalimbali au viongozi wa Bodi ambao wanateuliwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria hii haijatuonesha tafiti mbalimbali ambazo zitafanyika kama zitakuwa zimekosewa na kusababisha hasara kwa wakulima au wafugaji wetu, ni namna gani wananchi hawa wanaweza wakafidiwa na Serikali kwa sababu ya utafiti ambao unakuwa umefanyika vibaya. Tunachokiona pale ni kwamba kama watakuwa wamefanya utafiti na baadaye utafiti ule ukasababisha hasara kwa wakulima na wafugaji ni kwamba wale watu hawawezi kushtakiwa wala hakuna hatua zozote ambazo zinaweza zikachukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaleta mkanganyiko na tunaomba sana tujue juu ya suala hili. Hata Wabunge wengine wamesema wamenunua mbegu za mahindi wakipanda hazioti na kuingia hasara kwa sababu msimu unakuwa umeshapita. Kwa hiyo, lazima pia sheria ioneshe kwamba kama utafiti utafanyika vibaya na ukasababisha hasara kwa wananchi wetu ni lazima wananchi hawa ambao wamepata hasara waweze kufidiwa ili maisha yao yaweze kuendelea kama ambavyo walitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nilikuwa naangalia orodha ya vituo vya utafiti katika Jedwali sijakiona Kituo cha Utafiti cha Mbimba kilichopo Wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe. Kituo kile kinaendelea kufanya utafiti kwa muda mrefu lakini hakipo hapa. Kwa hiyo, wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kuhitimisha atueleze ni kwa nini Kituo hiki cha Mbimba kilichopo Wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe hakionekani kabisa kama ni kituo ambacho kipo wakati ni cha muda mrefu. Kwa hiyo, tutaomba pia tupate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni katika kifungu 27(1), kinasema kwamba Taasisi ya Utafiti inaweza ikakopa na ili iweze kukopa ni lazima Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Kilimo watoe idhini. Naomba tuendelee kupitia Sheria za *TR (*Msajili wa Hazina) kwani ndiye mtu pekee ambaye amepewa majukumu na mamlaka ya kuamua kwamba shirika au taasisi hii inaweza ikakopa kutokana na mpango kazi ambao inao kama inaweza ikarejesha zile fedha au zinaweza zikaleta tija katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wakati tunamzungumzia Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Kilimo ni lazima pia *TR* ashiriki kujua endapo mkopo huo ambao taasisi inaenda kuchukua utaleta tija katika Taifa hili na siyo Waziri mwenye dhamana pamoja na Waziri wa Fedha kushiriki peke yao. Kwa hiyo, naomba sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chuachua, ajiandae Naibu Waziri, Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa hii na mimi nichangie kidogo kwenye Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo. Ni imani yangu kwamba tukiwa na *good legal framework* na *good institution framework* kwa pamoja tunaweza tukafikia malengo yetu. Kwa maana hiyo basi, lazima sheria zetu zitupeleke katika kujenga msingi mzuri wa namna ya kuziendesha taasisi zetu. Nasema hivi nikiwa na maana

kwamba sheria hii inapaswa ituongoze katika kuzisimamia pia taasisi zetu na kuzijengea misingi imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hii tunaambiwa kabisa kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano atakuwa na mamlaka ya kumteua Mwenyekiti wa Bodi. Kuwa na mamlaka ya kumteua Mwenyekiti wa Bodi siyo tatizo, lakini tatizo linatokea pale ambapo sheria haoinyeshi sifa za Mwenyekiti wa Bodi. Nimesoma sheria mbalimbali zinaonesha wazi vigezo ambavyo Mwenyekiti wa Bodi anatakiwa awe navyo ili aweze kuchaguliwa hususani tunapowaweka Wenyeviti wa Bodi ambao wanakwenda kuongoza Bodi zinazolenga weledi wa namna fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo basi, ni muhimu sheria yetu ifikirie Mwenyekiti wa Bodi awe na sifa zipi ili awe Mwenyekiti wa Bodi husika. Nitaleta *schedule of amendment* mezani na nina imani Wabunge wataunga mkono namna ambavyo tunatakiwa tuangalie vigezo vya kuwateua Wenyeviti wa Bodi kwa sababu wana mamlaka makubwa ya ku-*influence* maamuzi ya Bodi hizi. Kwa hiyo, ni vyema wakawa na weledi wa eneo ambalo wanaliongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, Kamati husika imeeleza namna ambavyo kuna mgongano wa kimajukumu kati ya Tume ya Sayansi na Teknolojia pamoja na taasisi hii tunayoitengenezea sheria. Kwa maana hiyo basi, napenda kama kuna uwezekano sheria hii itambue kuwepo kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma sheria yetu hii hakuna mahali ambapo Tume ya Sayansi na Teknolojia inatambuliwa. Ni lazima tujiulize, je, kuna umuhimu wowote wa taasisi hii ya utafiti katika kilimo kutoa taarifa angalau za mwaka au kila mwaka kwa Tume kuhusiana na tafiti inazofanya au inazozisimamia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine la msingi, kuna taasisi hii ambayo ina vituo vya utafiti. Vituo hivi vya utafiti vimetajwa kwenye sheria lakini havijawekewa majukumu yake ya msingi. Nimesoma sheria ya Uganda, Kenya, Malaysia na nchi nyingine vituo vya utafiti vya namna hii majukumu yake yamekuwa *stipulated* kwenye sheria husika. Jambo hili limesaidia sana kuhakikisha kwamba vituo hivi vinakuwa na majukumu yaliyoko kwenye sheria hata kama wanatekeleza majukumu mengine wanayopewa na Bodi au *Director General* lakini wakati huo huo wanayo majukumu yao ya msingi. Ni muhimu tuyataje katika sheria ili vituo hivi viweze kufanya kazi zake kwa weledi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo lipo tatizo kubwa la kutopelekwa kwa taarifa za matokeo ya utafiti kwenye *grass roots*, hili nalo ni jambo la msingi sana. Sheria yetu haioneshi ni wakati gani vituo hivi vya utafiti vinalazimika kupeleka matokeo ya utafiti walioufanya kwa wananchi ambao kimsingi ndiyo *consumer* wa matokeo yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo mambo manne nadhani kama yatazingatiwa tutakuwa katika mstari mzuri wa kuendelea kuiboresha sheria yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Manyanya dakika 15, ajiandae Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi na niseme kwamba naunga mkono hoja. Napenda kuchangia katika Muswada wa Mamlaka ya Utafiti ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu yao yote kwa kuleta Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Tanzania hususani katika sekta ya uvuvi. Kwa muda mrefu nimekuwa pia nikijiuliza sana kwa nini maeneo ya uvuvi watu wake bado ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo nimekuwa nikilichangia hata humu Bungeni mara nyingi, kwa hiyo naona kwamba kupatikana kwa mamlaka hii ambayo sasa itakuwa ni imara kutafanya wananchi hawa sasa wabadilike. Wote tunafahamu asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima na wavuvi, kwa hiyo, iko haja kabisa Serikali kuongeza nguvu katika eneo hili kama ambavyo sasa tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na wachangiaji mbalimbali kwamba kuna umuhimu sana wa sisi Serikali kuongeza bajeti katika eneo hili la utafiti. Kwa sababu bila kufanya utafiti tutashindwa kugundua mambo mengi na sisi tutabaki kuwa watumiaji wa matokeo ya watu wengine bila sisi kuchangia katika matokeo ya utafiti ambayo yatasaidia nchi yetu pamoja na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo naomba nirudi katika kifungu cha 19 kufuatia hotuba ya Upinzani na wadau wengine ambao wamelizungumzia. Malalamiko ni kwamba kwa nini wale wanaofanya utafiti walazimike kupeleka maandiko yao katika mamlaka hii ili ndiyo waweze kupata fedha au wakati mwingine wanakuwa na fedha zao binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi pamoja na kwamba niko katika sekta ya elimu ambayo pia inajihusisha sana na masuala ya utafiti ikiwemo *COSTECH*, nipende kusema kwamba iko haja ya kufanya hivyo kwa sababu tumekuwa na fedha nyingi zinaenda kwa wadau mbalimbali wanaofanya tafiti lakini wakati mwingine *coordination* ya matokeo inakuwa haipo. Sasa hawa kwa sababu ndiyo wenye sekta yao na wanapenda kuona maendeleo ya sekta yao ni vema wale wadau wote wanaokuwa wamepewa fedha kwa ajili ya utafiti wajulikane na ili kujua kwamba fedha zilizokuwa zimetolewa zinatumika sawasawa na zinaleta matokeo chanya katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza hata kama mtu ana fedha zake, fedha zile zinakuwa ni zake pale ambapo anafanyia kazi zake binafsi, lakini anapoenda kufanya utafiti katika masuala ambayo yanahusu nchi na jamii lazima wote tufahamu nini kinachoendelea na matokeo yake ni nini, athari zake ni nini. Pia hata utangazaji wa matokeo hayo, yale matokeo yanayotangazwa yana faida au athari katika nchi, kwa hiyo lazima yawe *coordinated*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naona ni muhimu sana katika eneo hilo kuhakikisha kwamba hao wenye mamlaka wanakuwa ndiyo *custodian* wa matokeo yote hata kama taasisi nyingine zitakuwa zimesaidia kufanya hivyo. Kwa hiyo, niwaombe washirikiane na wadau wote ambao wanataka kufanya tafiti katika maeneo haya, wasione tabu kushirikiana na hii mamlaka ambayo ndiyo kisheria inao wajibu wa kuona kwamba sekta ya uvuvi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda nichangie kidogo katika jambo ambalo jana limenishtua sana kuona kwamba Mamlaka hii ya Utafiti wa Uvuvi inaambiwa kwamba inajilimbikizia kazi halafu ikalinganishwa na Wizara ya Elimu tena kwa maneno mabaya kutokea Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kimsingi sekta husika ndiyo msingi mkuu wa maendeleo ya sekta hiyo, kwa hiyo Wizara haiwezi kujitoa. Kwa mfano, katika suala la elimu

ambapo imezungumziwa vyuo inaonekana kwamba elimu ambayo inatolewa Tanzania haina manufaa kabisa, naomba tusifanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini aliyekuwa anazungumza alikuwa hana taarifa za kutosha kwa sababu kama angekuwa na taarifa za kutosha angeweza kuona jinsi ambavyo Tanzania imepiga hatua kwa kushirikiana na wananchi kuhakikisha kwamba sasa elimu inapatikana kiurahisi nchi nzima na matokeo yake ndiyo haya ambayo yanaonekana sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika udahili wa kuingia chuo kikuu sasa hivi malalamiko yamekuwa makubwa sana watu wana *point* 11, 12 hawajachaguliwa kwenda vyuo vikuu si kwa sababu wamenyimwa bali wanafunzi wengi wamefaulu kwa ufaulu wa juu kiasi kwamba nafasi zimekuwa chache, hiyo ndio kazi sahihi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukisema kwamba sekta binafsi ndiyo inafanya vizuri kuliko Serikali wakati wewe unapima tu matokeo labda kwenye *rank* shule hii ilikuwa ya kwanza na shule ya Serikali inaonekana ilikuwa ya 200 lakini hiyo shule ya Serikali unakuta ina wanafunzi 300 hapo hapo *division one* labda wako 100 na wakati shule isiyokuwa ya Serikali ina wanafunzi 40 tu ndiyo maana labda ikawa na *rank* ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivi vitu vyote lazima tuvifanyie *analysis.* Ndiyo maana sasa hivi unakuta wanafunzi wakishatoka katika elimu ya msingi mpaka sekondari kidato cha sita hawataki tena kuendelea kwenye vyuo vya binafsi wanakimbilia vyuo vya Serikali kutokana na ubora unaoboreshwa kila siku, hata sasa hali ndiyo hiyo.

Kwa hiyo, niwaombe sana ndugu zangu tusitumie nafasi zetu tunapochangia kujidharau wenyewe kwa sababu unaweza ukaongea jambo hata wewe mwenyewe ukaonekana hujui unachoongea. Kwa hiyo, lazima tujivunie kazi kubwa tulizofanya pamoja, kwa kushirikiana Upinzani na Chama cha Mapinduzi kuona kwamba sekta yetu ya elimu inazidi kuwa nzuri na kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizidi kusisitiza utafiti huu uwe na manufaa. Mara nyingi sana tafiti zinafanyika katika ile hali ya ugunduzi lakini inapokuja kwenye *commercialization* yaani sasa iweze kutumika kwa wananchi watafiti wengi hawataki kusindikiza utafiti. *Research* nyingi zinazofanyika ni zile za kuandika lakini *action research* zinazofuatilia nini kimefanyika, wapi tuboreshe, wapi twende mbele zimekuwa ni chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anataka akifanya moja amemaliza anachukua fedha zake anaondoka, tunataka mtu asindikize utafiti wake mpaka mwisho ili tuone matokeo na tuweze kupima fedha zinazotolewa sambamba na matokeo tunayoyatarajia. Mimi binafsi kwenye Wizara yetu tutakuwa wakali katika eneo hilo na tunasema kwamba kila mtu anapofanya utafiti lazima usajiliwe vizuri na tufuatilie matokeo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno yangu haya, nazidi kukushukuru kwa muda wako, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Waziri ajiandae.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata nafasi hii ya kuchangia kwenye Miswada hii miwili muhimu. Nikushukuru kwa kunipa fursa hii na naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Uvuvi na Mifugo kwa kuleta Miswada hii miwili ambayo ni muhimu sana kwa maslahi ya Taifa hili kwenye masuala haya ya kilimo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia Miswada hii na sisi tunawashukuru tumeyafanyia kazi yale mapendekezo yao. Wajibu wangu asubuhi hii ni kujibu tu hizi hoja chache za kikatiba na za kisheria pengine zitatusaidia wale ambao hatuelewi masuala ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni Muswada wa Kilimo kutotaja matumizi ya sheria hii katika pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa Katiba siyo lazima utaje kwenye Muswada kwamba sheria hii itatumika upande upi kwa sababu masharti yenyewe yamewekwa kwenye Katiba. Ukisoma Ibara ya 64(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzani, inasema:-

*"Mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara, yatakuwa mikononi mwa Bunge".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama yanakuwa mikononi mwa Bunge, Bunge linalozungumzwa hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siyo lazima utaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaendelea kusema kwenye ibara ndogo ya (2) kwamba:-

*"Mamlaka yote ya kutunga sheria katika Tanzania Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya muungano yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sheria inapotungwa ina maana itatumika pale pale na Ibara hii ya 64 imeendelea kufafanua mambo mengine mengi. Ibara ndogo ya (4) inasema hivi:-

*"Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge kuhusu jambo lolote haitatumika Tanzania Zanzibar ila kwa mujibu wa masharti yafuatayo:-*

*(a) Sheria hiyo iwe imetamka wazi kwamba itatumika Tanzania Bara na vilevile Tanzania Zanzibar au iwe inabadilisha, kurekebisha au kufuta sheria inayotumika Tanzania Zanzibar".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sharti lililopo pale ni kwamba kama hiyo sheria tunayoitunga itatumika pande zote mbili za Muungano ndiyo lazima utaje. Kwa sababu hiyo tuna sheria nyingi sana ambazo zimetungwa bila kulazimika kutaja hivyo, nitawatolea mifano. Sheria hizo ni kama zifuatazo:-

*(i)* *The Marine Parks and Reserve Act, No.* 29 of 19994;
*(ii)* *The Plant Protection Act, Cap.*132, No. 13 of 1997;
*(iii)* *The Plant Breeders' Right, Cap.*344, Na. 9 of 2012;
*(iv)* *The Merchant Shipping Act, Cap.*165, Na.21 of 2003;

*(v)* *The Tanzania Fisheries Research Institute Act, Cap.*280, No. 6 of 1980;

*(vi)* *The Tanzania Industrial Research and Development Organization Act, Cap.*159, No. 5 of 1979; na

*(vii)* *The Public Service Act, Cap.*298, No. 8 of 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo lazima sheria itaje, lakini tumekuwa tukipokea haya kwa masharti ya Katiba yenyewe. Katika tu kufanya ufafanuzi tumekuwa na tabia sheria nyingine tunaandika kwamba sheria hii itatumika Tanzania Bara peke yake lakini hata usipotaja siyo kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili lina mamlaka mawili; moja linatunga sheria za kutumika pande zote mbili kwa mambo ya Muungano lakini pili linatunga sheria kwa ajili ya Watanzania Bara kama ambavyo tumeshasoma katika Ibara ya 64. Kwa hiyo, kama haikutaja ujue tu kwamba hiyo sheria itatumika Tanzania Bara peke yake. Waheshimwa Wabunge, mkisoma Ibara yote ya 64 mtaona tunachokifanya kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulikubali tu ushauri wa Kamati ili kuleta *clarity* kwenye uandishi. Kwa hiyo, hata jana tulipowasilisha Muswada huu Waziri aliwasilisha pia na *Schedule of Amendment* na Wabunge walipokuwa wanachangia tayari ile *Schedule of Amendment* walikuwa nayo ambayo inataja kwamba hii sheria itatumika Tanzania Bara peke yake. Kwa hiyo, niliona nitoe ufafanuzi wa suala hili ili litusaidie tunapokwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nimeona nilitolee ufafanuzi hapa ni kwamba masuala ya utafiti yako kwenye mambo ya Muungano, ni kweli unaipata kwenye Ibara ya 4(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jedwali la Kwanza linalotaja mambo ya Muungano pale ndiyo unaona utafiti. Hata hivyo, suala la msingi hapa ina maana kila ukishakuwa utafiti unakuwa wa Muungano? Tafsiri ya sheria ni kwamba huo utafiti unaoutungia sheria ni ule unaohusu Muuungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hiyo Nyongeza ya Kwanza ya Katiba utakachokiona ni kwamba suala la kilimo na mazao ya kilimo siyo masuala ya Muungano na suala la samaki na uvuvi siyo suala la Muungano. Kwa hiyo, huwezi kutunga sheria na kuifanya kuwa ya Muungano eti kwa sababu tu imetajwa kwenye utafiti. Kama unataka kufanya utafiti kwenye mambo ya ulinzi na usalama hilo ni la Muungano utatunga sheria ambayo ni ya Muungano na mambo mengine yaliyowekwa pale. Kwa hiyo, hili siyo lazima na nilifikiri nilitolee ufafanuzi ili litusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *Deep Sea Fishing Act*, kule uvuvi umefanywa kuwa wa Muungano kwa sababu ya *United Nation Convention on the Law of the Sea.* Katika *international community* pale hakuna Tanzania Bara wala hakuna Zanzibar *and this should be so much clear and understood by whole Members of the House.* Katika Jumuiya ya Kimataifa tunajulikana kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiyo maana tumetunga sheria kwa makubaliano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba uvuvi katika kina cha chini cha bahari huo utakuwa ni suala la Muungano na hapo hakuna dhambi madam Serikali za nchi mbili hizi zilikubaliana, kwa hiyo, niwatoe wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria iliyokuwepo ya *Tanzania Fisheries Research Act* ya mwaka 1980 ambayo ndiyo tunakusudia kuifuta kama mtaridhia ilikuwa inatumika upande

mmoja tu. Kwa hiyo, hili nalo nilifikiri nilitolee ufafanuzi ili kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulitolea ufafanuzi na ambalo linajirudia mara kwa mara na nashindwa kuelewa ni kwa nini nalo ni jukumu la Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mwanasheria Mkuu wa Serikali anazaliwa na Ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pale anatajwa kwamba pale na katika sheria nyingine ataitwa tu Mwanasheria Mkuu haisemi ni *Attorney General of the Executive.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kuchanganya katika matumizi ya neno Serikali kwa sababu ya umaskini wa msamiati kwenye Kiswahili tu. Tunaitumia Dola/*State* kwa kusema Serikali, tunatumia *Executive* pia kwa kusema Serikali *but* kinachozungumzwa kwenye Ibara ya 59 pale ni *State*/Dola ambayo inagusa mihimili yote na maana yake kwa Kingereza ni *Government,* someni *The Interpretations of Laws Act.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema *Government it includes all the three department of the state that is the Executive, the Legislature and the Judiciary.* Kwa hiyo, pale unaipata Mahakama, Bunge na Utawala. Hata katika kuandika hapo, mimi naandika hizi sheria unaona pale nimeandika *Attorney General* sisemi *Attorney General of the Executive.* Ndiyo maana Mawakili wa Serikali wote kama mimi hapa naitwa *State Attorney*/Wakili wa Dola na hapa ni Dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatuiti Mawakili wa *Executive* ni *State Attorneys, State* ni Dola, kule Uingereza wanaitwa *Crown Counsel.* Kwa hiyo, nilifikiri niliseme hili litusaidie kwa sababu linajirudiarudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlinzi wa maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika *international community* na ndani ya nchi ni *Attorney General.* Ndiyo maana kifungu cha 17 cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuingilia shauri lolote lile ili mradi lina maslahi ya umma na imetajwa pale Waheshimiwa Wabunge someni kifungu cha 17 mtaona. Kinasema Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuingilia masuala yanayohusu Bunge, Mahakama na maslahi ya taasisi yoyote ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 59(4) nafikiri niisome labda itatumalizia mambo haya yasiwe yanarudiarudia, haki hii imewekwa Kikatiba, hamuwezi mkataka *Attorney General* asiingilie kwenye mambo yanayohusu maslahi ya nchi hii, ni mpaka mfute hii Ibara ya 54 ndiyo mtake *Attorney General* asiwepo pale. Inasema hivi:-

*"Katika kutekeleza kazi na shughuli zake kwa mujibu wa ibara hii, Mwanasheria Mkuu atakuwa na haki ya kuhudhuria na kusikilizwa katika Mahakama zote katika Jamhuri ya Muungano." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *so go and amend this Article of the Constitution and then you are done with the Attorney General,* sijui kama itawezekana. Mkiunda Serikali ambayo haiheshimu mamlaka ya *Attorney General,* itakufa siku hiyohiyo. Kwa hiyo, nilifikiri niliseme hili litusaidie tumalize haya mambo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifano mingi sana ya sheria ambazo zimetungwa tangu nyuma ambazo zinataja umuhimu wa *Attorney General* kuingilia kati siyo tu kwenye hizi sheria tunazozitunga leo. Sheria hizo ni:-

*(i)* *The Ports Act* ya mwaka 2004 yaani Sheria ya Mamlaka ya Bandari ya mwaka 2004, *section 4(2)*;

*(ii)* *The Surface and Marine Transport Regulatory Authority,* hii Sheria ya *SUMATRA* ya mwaka 2001;

*(iii)* *The Energy and Water Regulatory Authority* ya mwaka 2001, hii ni Sheria ya *EWURA*; na

*(iv)* *The Tanzania Communication Regulatory Authority* ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo sheria za kwanza hizi. Ukielewa lengo la Katiba kama lilivyo kwenye Ibara ya 59 *then* hutakuwa na shida. Kwanza siyo lazima aingie, anaingia pale ambapo inalazimika. Kwa hiyo, nilifikiri niyatolee ufafanuzi masuala haya kwa faida yetu sisi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kwa muda mfupi kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ikiwa ni pamoja na yale yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia napenda kuongezea kidogo kwa lile alilozungumzia kwa ufasaha sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusiana na kifungu cha 3(5) cha Muswada wa Taasisi ya Kilimo unaopendekezwa. Iliibuliwa hoja na Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba lengo la kifungu hicho ni kuzuia mtu, shirika, taasisi au kampuni binafsi kupata haki endapo *TARI* itashitakiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema lengo la kufanya hivi kwa vyovyote vile haiwezekani ikawa ni kwa ajili ya kutaka kumuathiri mtu binafsi au taasisi. Lengo lake kubwa ni kwa ajili ya kulinda maslahi mapana ya umma lakini vilevile ni kwa sababu ndiyo sheria na Katiba yetu inavyotutaka. Kama alivyosema Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ibara ya 59 inaweka wazi ndiyo maana ofisi hiyo imeanzishwa. Kimsingi Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana nguvu na anapaswa kuwepo pale taasisi ya umma au Serikali inaposhtakiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lake ni pamoja na kulinda maslahi ya umma kwa sababu kwenye mashtaka yale mara nyingine yasiposhughulikiwa kwa ufasaha na kwa weledi, inawezekana Serikali ikapoteza kesi au taasisi ya Serikali ikapoteza kesi na hivyo Serikali ikapata hasara kubwa na umma wa Watanzania ukabeba mzigo mkubwa ambapo pengine kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali angeshiriki labda isingetokea hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba ukitaka kufahamu kwamba hakuna nia mbaya katika kuleta hayo matakwa ya Kikatiba, hata kwenye kesi za uchaguzi anaingia. Jana kulikuwa na Mheshimiwa alikuwa anashangilia kwamba ametoka kushinda kesi, kwenye kesi dhidi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mwanasheria Mkuu naye vilevile anakuwepo. Kama Tume ndiyo imeshtakiwa haijalishi kama Mbunge anayeshtakiwa ni wa Upinzani au ni wa Chama Tawala, Mwanasheria wa Serikali anakuwepo

upande wa Tume na mara nyingine sasa unakuta hata ushindi wanaopata Wabunge wa Upinzani ni kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametia mkono wake. Kwa hiyo, kama mnavyoona hakuna lengo baya, haimbagui mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitoa vilevile mapendekezo kuhusiana na viwango vya posho za Wajumbe wa Bodi, wao wakipendekeza kwamba zipangwe na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Ofisi inayohusika na Utumishi wa Umma. Mapendekezo ya viwango vya posho huandaliwa na Bodi kwa kuzingatia Waraka wa Msajili wa Hazina.

Kwa hiyo, tayari kuna Waraka unaoelezea na kuainisha ni namna gani posho hiyo ilipwe na viwango vinatakiwa viwe vipi. Mara nyingi viwango hivyo huwasilishwa kwenye Wizara Mama kwa ajili ya kuvipitia na hatimaye huwasilishwa kwa Msajili wa Hazina na Idara Kuu ya Utumishi kwa ajili ya kupata idhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwafahamishe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna utaratibu tayari wa kikanuni wa namna masuala ya posho yanavyofanyiwa kazi kwa hiyo, haitakaa itokee kwamba Wizara au Bodi au Waziri wakavuka mipaka ile ambayo haitakiwi kwa sababu tayari Msajili wa Hazina atakuwa na mkono wake pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitolewa vilevile hoja na Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba muundo wa Taasisi ya *TARI* utaidhinishwa na chombo kipi kama Bodi ya Wakurugenzi imepewa nguvu ya kuanzisha Idara na Vitengo kwa kadri inavyoona inafaa? Muundo wa taasisi hutegemea majukumu ya taasisi moja moja na yalivyoainishwa katika sheria ambayo inaanzisha taasisi hiyo. Kwa msingi huo, taasisi husika huandaa mapendekezo ya muundo na kuwasilisha kwa Wizara Mama, Msajili wa Hazina na hatimaye Idara Kuu ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kuidhinishwa. Kwa hiyo, tayari kuna taratibu ambazo zinatumika ili kuondoa nafasi au uwezekano wa Bodi kuweza kuunda vyombo vingine au idara kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliibuliwa vilevile hoja kwamba muda wa watendaji kuhudumu ungekuwa wazi ili kuondoa tabia ya watendaji kukaa muda mrefu katika nafasi zao. Watendaji wa taasisi ni watumishi wa umma ambao wanatekeleza majukumu yao katika taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji katika taasisi watahudumu katika nafasi zao kwa kuzingatia masharti ya ajira zao. Muda wa kustaafu na masharti mengine vinafanya kazi kwao kama ilivyo kwa watumishi wengine wa umma. Kwa hiyo, hamna kitu kipya kinachoanzishwa, wale watendaji wakuu siyo kwamba wao watakuwa na masharti tofauti ya utumishi tofauti na wengine. Kwa hiyo, taratibu za kawaida kuhusu muda, marupurupu zitaendelea kutumika bila ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitolewa vilevile hoja kwamba Waziri mwenye dhamana ya kilimo ndiyo mwenye uamuzi wa mwisho kuhusu rufaa. Utaratibu wa Waziri mwenye dhamana katika jambo fulani kuwa na uamuzi wa mwisho katika maamuzi ni wa kawaida kwa sababu Waziri ndiyo ngazi ya juu kabisa ya maamuzi katika Wizara. Kwa hiyo, anapotoa ule uamuzi inamaanisha tu kwamba katika ngazi ya Wizara yeye ndiyo mwenye maamuzi ya mwisho, lakini haimaanishi kwamba hakuna fursa zozote nyingine za mtu anayefikiri kwamba hakubaliani na maamuzi ya Waziri kwamba hawezi kupata nafuu ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wetu kama mtu haridhiki na uamuzi wa Waziri anaweza akaenda Mahakama Kuu kufanya mapitio na kama itaonekana kwamba Waziri

alikiuka taratibu au hajatenda haki, mara nyingi Mahakama zetu hubadilisha na kuyafutilia mbali maamuzi ya Waziri. Kwa hiyo, *finality clauses* kwenye sheria hizi zisiwape tabu kwa sababu haimanishi kwamba mtu hawezi kwenda Mahakamani, inawezekana lakini kwenye ngazi ile ukitoka kwa Waziri hamna sehemu nyingine ya kwenda katika Wizara lakini anaweza akaenda Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wameleta hoja na hoja ziko nyingi, nitaziangalia baadhi, Mheshimiwa Waziri baadaye atapata naye fursa ya kuangalia hoja za Wabunge. Imetolewa hoja kwamba sheria inayotungwa iainishe ni vipi matokeo ya tafiti zitakazofanyika yatawafikia walengwa. Ili kuongeza ufanisi wa kufikisha matokeo ya utafiti kwa wadau, taasisi inayopendekezwa inatarajiwa kuweka Kurugenzi ya Usambazaji Teknolojia na Mahusiano. Kwa njia hii tunafikiri tafiti zile zitaweza kuwafikia walengwa kirahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa vilevile hoja kwamba muda wa miaka kumi ya uzoefu unaotakiwa kwa Mkurugenzi Mkuu ni mrefu na imetolewa hoja kwamba upunguzwe. Nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ni nyeti sana katika kusimamia na kuhakikisha kuwa Taasisi ya Utafiti inayokusudiwa kuanzishwa inaendeshwa kwa umahiri na kuweza kufikia malengo ya uanzishwaji wake. Ili kumpata mtu kushika nafasi hii kunahitajika weledi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaamini kuwa na sifa au uwezo wa kuiongoza taasisi nyeti kama hii inahitaji mtu aliyebobea kwenye utafiti, mtu ambaye tayari ana uzoefu wa kimenejimenti na mtu ambaye ukimleta ni rahisi kuongoza taasisi kama hiyo. Kwa hiyo, ni kawaida hamna kitu kipya, tunafikiri miaka kumi siyo mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa hoja vilevile kwamba taasisi inayopendekezwa ya *TARI* ingekuwa vema kama ingeunganisha tafiti za kilimo pamoja na mifugo. Tungependa kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba tayari kuna taasisi inayohusika na utafiti wa mifugo na hii inaitwa *TALIRI (Tanzania Livestock Research Institute)*. Hata hivyo, tungependa kuendelea kutenganisha mifugo na kilimo kwa sababu kwa muda mrefu imekuwa ni rahisi mifugo kumezwa ndani ya kilimo. Kwa hiyo, tunapokuwa na taasisi mbili inasaidia utafiti kufanyika kwa umakini zaidi katika maeneo yote hayo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa vilevile hoja kwamba taasisi ione jinsi itakavyoshirikisha vyuo vikuu vinavyofanya utafiti. Napenda kusema kwamba taasisi inayopendekezwa imeweka muundo wa uendeshaji ambapo kwenye Bodi na kwenye Jukwaa la Ushauri, viongozi wakuu wa vyuo vya elimu ya juu ni mojawapo ya wajumbe ili kuhakikisha kwamba wanashiriki kikamilifu katika shughuli za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa hoja kwamba inabidi mfumo wa uteuzi wa kutumia ushindani utumike katika kumpata Mkurugenzi Mkuu. Utaratibu uliowekwa na Muswada unaleta ushindani. Kwa sababu kabla ya uteuzi kufanyika lazima usaili ufanyike ili kuwapata watu wale ambao ndiyo wanapendekezwa waweze kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tayari kuna ushindani katika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imetolewa hoja kwamba Taasisi ya Utafiti ya Kilimo imeonesha kuwa itakuwa Tanzania Bara lakini kwenye Katiba utafiti ni jambo la Muungano, inabidi maelezo yatolewe. Suala la kilimo siyo suala la Muungano, kwa hiyo, taasisi inayoanzishwa ni kwa ajili ya Tanzania Bara tu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Unga mkono hoja.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha katika hatua hii ya mwisho ya mjadala wa Muswada wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(The Tanzania Agricultural Institute Act, 2016)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, kwa masikitiko makubwa naomba kuchukua fursa hii kutoa pole kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera, Mwanza na maeneo mengine ya jirani kwa maafa yaliyotokea kutokana na tetemeko la ardhi lililosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa miundombinu pamoja na makazi yao. Namwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na awajalie mioyo ya subira katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge Viti Maalum, kwa michango na ushauri wao ambao umechangia kuboresha Miswada hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipende kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Semesi Sware, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Miswada ya *TARI* na *TAFIRI*. Niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ambayo kwa kweli imeimarisha sana maudhui ya Miswada hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Miswada hii miwili ambayo imechangiwa kwa pamoja imechangiwa na jumla ya Wabunge 38 kwa kuongea ambapo Wabunge wanne wamechangia kwa maandishi. Kwa sababu ya muda na Kanuni zetu, naomba orodha ya Waheshimiwa hawa nisiwataje lakini iwe sehemu ya maelezo yangu haya. Napenda kuwahakikishia kwamba michango yao tumeipokea na tumeizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila, nichukue muda huu kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndugu yangu Mheshimiwa George Masaju, kwa msaada mkubwa alioutoa sasa hivi. Pia, nimshukuru Mhandisi Mheshimiwa Stella Manyanya, Naibu Waziri, kwa mchango wake mzuri katika maeneo ambayo yanahusu eneo analolisimamia. Vilevile nimshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa William Ole-Nasha, kwa ufafanuzi alioutoa katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda sasa kujibu hoja za Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na michango ya baadhi ya Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Namba 7 ya mwaka 1986 inayoanzisha Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH),* ambayo imeweka sharti la kuelekeza fedha zote katika Mfuko wa *COSTECH,* Wajumbe walitaka kufahamu kama fedha za utafiti katika sekta ya kilimo zitaelekezwa katika Mfuko huo na nini athari zake katika ufanisi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo *(TARI).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba sheria hiyo inasema hivyo na Mfuko wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia *(National Fund for Advancement of Science and Technology)* upo ili wanaofanya utafiti na kuendeleza uvumbuzi wa teknolojia waweze kutuma maombi ya kuzipata kwa kutumia vigezo vilivyoainishwa na Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kinachofanyika ni rahisi sana kwamba utaratibu wa kupata fedha kwenye Mfuko huu ni wa ushindani, kwa hivyo watafiti mbalimbali *across the board* wanachotakiwa kufanya ni kuandika maandiko ambapo vipaumbele katika Bodi pale *COSTECH* vimeainishwa na anayekuwa ame-*qualify* vizuri *then* anapata fedha kwa ajili ya kuendeshea utafiti wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hilo halizuii mamlaka za tafiti ku-*source* fedha kutoka maeneo mengine. Wanaweza wakapata fedha kutoka kwingine kokote na hili ndilo limezingatiwa katika Muswada huu kwa kukubali maoni ya Kamati kuanzisha Mfuko wa Utafiti ndani ya *TARI.* Kwa hivyo, tunapoanzisha *TARI* na kuwawekea uwezo wa kuanzisha Mfuko kwa ajili ya utafiti *then* ile fedha inayopatikana kule *COSTECH* itakuwa tu ni nyongeza ya hicho ambacho wanaweza kukusanya wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Wajumbe katika Kamati walitaka kufahamu utaratibu utakaotumika kwa taasisi nyingine za elimu ya juu zinazofanya utafiti wa masuala ya kilimo. Taasisi zote za elimu ya juu zinazofanya utafiti wa masuala ya kilimo zitaendelea na shughuli hizo na hazitazuiwa na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, uwepo wa *TARI* utawawezesha watafiti katika taasisi hizo kufanya kwa mashirikiano na maelewano na watafiti katika *centres* zetu hizi ambazo zitakuwa chini ya *TARI* kwa kuzingatia vipaumbele vya Kitaifa ambavyo vitakuwa vimeainishwa na *TARI.* Kwa hivyo, kama alivyosema Mheshimiwa Mhandisi Manyanya hili halipingani isipokuwa lina-*complement* na kuweka utaratibu ambao sasa utafanya *duplication activities* kwenye taasisi mbalimbali isitokee tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, kama watakumbuka nilivyokuwa nawasilisha hoja hili ndilo tulisema moja ya matokeo makubwa ya Muswada huu utakapopitishwa ni hilo kwamba sasa angalau kinachofanyika kwenye kila *center* kifahamike *centrally* na kusije kukawa na *duplication* ya *activities.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Waheshimiwa Wabunge walitaka kujiridhisha endapo sheria inayoanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo haitaongeza ukiritimba katika utafiti. Kama nilivyosema hili jambo haliwezi kutokea isipokuwa tu ni kwamba *coordination* ndiyo itakuwa *streamlined*. Badala ya kuwa tu watu wanafanya utafiti *chaotically* kama ilivyokuwa awali sasa watakuwa *coordinated* hasa katika hii tasnia ya kilimo kwa kuhusisha na taasisi nyingine za utafiti kama vyuo vikuu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waheshimiwa Wabunge walitaka kufahamu utaratibu utakaotumika kuhakikisha fedha kwa ajili ya utafiti wa kilimo zinapatikana. Nimekwishasema

*COSTECH Fund* ni moja ya *sources* lakini baada ya ku-*introduce* Mfuko wa Utafiti kwenye taasisi *then* watakuwa na uwezo wa kupata fedha kutoka maeneo mengine na kwa kweli hizo zitakuwa ni nyongeza tu. Jambo lingine ni suala la Serikali kujitahidi kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana ili tufikie lengo letu lile la *percent* moja ya *GDP* tuwe tunaielekeza kwenye utafiti *across the board* kwa maana ya taasisi zote zinazohusika na utafiti ziweze kupata fedha ya kutosha katika kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kidogo mambo yalizungumzwa na Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada huu wa Taasisi ya Kilimo. Wenzetu wa upande wa pili wametaka kujua kifungu cha 3(3) na (5) cha sheria kinalenga kuzuia mtu, shirika, taasisi, ameshasema Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye mambo ya mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walitaka Mwenyekiti wa Bodi ateuliwe kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bodi. Mwenyekiti wa Bodi ni sehemu ya Wajumbe wa Bodi lakini utaratibu wa kumpata Mwenyekiti ndiyo huo sheria inataka ateuliwe na mkuu wa nchi, kwa nini? Kwa sababu hiki ni chombo kikubwa sana kinachoshikilia maslahi ya Taifa zima. Nadhani ni matakwa ya Kikatiba pia kwamba viongozi wa namna hii wateuliwe na Mheshimiwa Rais. Hata hivyo, upatikanaji wake katika kanuni tutakazoziandaa utaweka sifa za huyo Mwenyekiti. Kwa hiyo, kabla ya Rais kufanya uteuzi atakuwa amejielekeza kwenye sifa ambazo zimetajwa katika sheria kwamba Mwenyekiti angalau awe na sifa zifuatazo ili aweze kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nadhani pia namjibu Mbunge aliyechangia mwisho hapa ambaye alisema kwamba Wenyeviti hawa wanateuliwa ambao hawana kabisa mwelekeo wa aina yoyote na taasisi au bodi wanazokwenda kuziongoza, hapana! *This time around* kanuni itataja sifa za yule mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi kama ambavyo zinataja mtu anayetakiwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Mkurugenzi ishindaniwe kwa sifa, hili nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri ameshalisema. Ushindani ni lazima kwa ngazi ya awali kabla ya majina kadhaa kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais mwenye mamlaka ya uteuzi kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani pia wametaka muda wa watendaji kuhudumu ungewekwa wazi ili kuondoa tabia ya watendaji kukaa muda mrefu katika nafasi zao. Hili jambo naomba tulielewe vizuri, watendaji wa hizi taasisi *(centers)* hizi ambazo sasa zinakuja kuwekwa kwa pamoja chini ya *TARI* ni watumishi walioajiriwa na Serikali kwa masharti ya kudumu na pensheni. Hapa wataingizwa kwa sheria hii lakini siyo kwamba wanaenda kuajiriwa upya, hawa wanaingia huku lakini ajira zao zinaendelea na masharti yao ni *permanent and pensionable.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, hatuwezi tukaweka sharti humu linaloweka ukomo wa ajira yao, ukomo wa ajira yao itakuwa ni *either* kutimiza miaka 60 kwa kustaafu kwa kawaida au kufukuzwa kazi kama watakuwa wamefikia hatua hiyo. Kwa sasa hivi kwa sababu sheria inawaingiza tu kwa ujumla kwenye utumishi wa taasisi hatuwezi kuwabadilishia masharti ya ajira kwa sababu hizi sio ajira mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kambi Rasmi ya Upinzani ilitaka watendaji wa vituo wasiteuliwe bali wapatikane kwa ushindani. Ni kweli kabla ya kuteua watendaji wakuu wa vituo itazingatia taratibu za ajira na kwa njia ya ushindani. Vituo hivi vinasimamiwa na Bodi, tunaamini kwamba Bodi itatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kwa Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia hili jambo kwa kuzungumza. Mheshimiwa Jitu Soni amechangia *passionately* na Mheshimiwa mmoja hapa jina nimelisahau, waliuliza kwa nini vyuo vikuu visichukue hii dhamana ya utafiti badala ya kutengeneza taasisi tofauti na hivi vyuo vikuu tulivyonavyo. Ni kweli, hii mifumo yote miwili inatekelezwa duniani na kama mlikuwa mmesikiliza vizuri katika uwasilishaji wangu wa hoja nilitaja nchi zaidi ya tano ambazo zinatumia utaratibu huu wa utafiti katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, hutegemea nchi na nchi inaona iende na utaratibu gani wa utafiti kwa kuhusisha vyuo vikuu na *institutes* ambazo hizi hasihusiki na mafundisho ya aina yoyote wao wanajikita tu kwenye utafiti. Muundo tunaoupendekeza ni huu ambao unatumika katika nchi zingine ambazo zinafanya vizuri tu na wala hazifanyi vibaya kwa kulinganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la mtu anayetaka kufanya usajili anaweza kukataliwa au haonyeshwi fursa ya rufaa. Ni kweli maoni haya tumeyapokea kwamba lazima katika kanuni tutengeneze utaratibu ambao utamfanya mtu ambaye amepeleka maombi ya kufanya utafiti endapo atazungushwa au kukataliwa, basi uwepo utaratibu wa kukata rufaa ili aweze kupata haki ya kufanya utafiti na asitengenezewe mizengwe na sheria yenyewe. Kwa hiyo, hili jambo tumelichukua na kwa kweli tutalifanyia kazi katika kanuni kuweka utaratibu ambao rufaa zitakuwa zinakubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sakaya alisema kwamba Muswada katika kifungu cha 35 umeainisha kuwa Waziri peke yake ndiyo mamlaka ya mwisho. Mheshimiwa Naibu Waziri amelitolea maoni hapa kwamba *administratively* ndiyo Waziri anakuwa wa mwisho lakini bado mwananchi yaani *aggrieved person* ana kuwa ana uhuru wa kutafuta haki yake hiyo Mahakamani au katika vyombo vingine vilivyopo vya kutoa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la masoko na lenyewe limezungumziwa kwa hisia kubwa sana hapa ndani. Baada ya kutambua kwamba lipo tatizo la soko, zipo taasisi nyingi za Kiserikali zinazojihusisha na utafutaji wa masoko wa bidhaa kwa ujumla. Wizara ya Viwanda na Biashara inalo hilo jukumu la msingi la kutafuta masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na kujua kwamba zipo mamlaka zingine za Kiserikali za kushughulikia masoko bado tumeona umuhimu wa kuliweka hili jambo kwenye moja ya majukumu ya taasisi hii ili na wao wajihusishe na utafutaji wa masoko. Kwa hivyo, hiyo habari ya nyanya zinakosa wanunuzi na mazao mengine yanakosa wanunuzi pamoja na jitihada zilizopo kwenye taasisi zingine tumeiongezea hii Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na yenyewe iwe na jukumu la kutafiti juu ya masoko kwa ajili ya bidhaa za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine limezungumzwa kwamba Muswada hauoneshi ni kwa vipi taasisi za kilimo za watu binafsi zinaweza kufanya utafiti. Nadhani aliyesema hivi hakuwa amesoma vizuri, Muswada unaruhusu watu binafsi na watafiti binafsi kufanya utafiti isipokuwa tu kwamba hayo maeneo ya utafiti wanayotaka kufanya waende wakayasajili kwenye taasisi. Pia kwa sheria ya *COSTECH* ilivyo wanapaswa kwenda kusajili maeneo yale ya utafiti wanayotaka kufanya kule *COSTECH*.

Wote mnafahamu mtu anaweza akawa anafanya utafiti kwa ajili ya kupata *academic qualification,* sasa kama hawatatakiwa kwenda kusajili mtu anaweza tu akachukua utafiti wa mtu mwingine akabadilisha *title* akaenda aka-*publish* kule ikaonekana ni wake. Kwa hili la

kwenda kuwasajili *then* inaweka kama *governor* ya mtu kuweza kufanya udanganyifu katika mambo haya ambayo kwa kweli baadaye yana-*attract* vitu vingi ikiwa ni pamoja na *intellectual properties* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2016**
**(*The Tanzania Agriculture Research Institute Bill, 2016*)**

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilileta *amendments* sasa nashangaa sijatajwa hapo.

**MWENYEKITI:** Meza haijapata *amendment* ya Mbunge yeyote tumepata *amendments* za Serikali tu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipeleka jana.

**MWENYEKITI:** Sasa ndiyo nasema hivi Meza haijapata *amendment* yoyote mpaka sasa hivi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28
Ibara ya 29

Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la Kwanza

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la Pili

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la Tatu

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarudia.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae, mtoa hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko sijakuruhusu, soma Kanuni ya 52(2). Mtoa hoja.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima limepitia Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania ya mwaka 2016 (*The Tanzania Agricultural Research Institute Act,* 2016) kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake na kuukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu pamoja na marekebisho yake sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji kuhusu Muswada huu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania ya mwaka 2016 (*The Tanzania Agricultural Research Institute Act,* 2016).

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umepitishwa na Bunge Zima, Katibu kwa hatua inayofuata.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga Sheria ya Kuimarisha Mfumo wa Utafiti wa Kilimo, kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, kuweka utaratibu madhubuti, utawala bora, usimamizi na utekelezaji wa utafiti wa kilimo pamoja na mambo mengine yanayohusiana nayo.

*(A Bill of an Act to provide for the enhancement of an agriculture research system, establishment of Tanzania Agriculture Research Institute, effective coordination, governance, management and conducting of agricultural research activities and to provide for other related matters)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua ya Bunge kazi yetu imekwisha sasa inabaki hatua ya Mheshimiwa Rais kuweza kuuridhia na baadaye taarifa ikaletwa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 6.23 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa mwaka 2016**
***(The Tanzania Fisheries Research Institute Bill, 2016)***

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa mwaka 2016**
***(The Tanzania Fisheries Research Institute Bill, 2016)***

Ibara ya 1

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 1 kina marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufanya marekebisho katika kifungu hicho ili kwenye *application* yake kisomeke, baada ya maneno *by adding the words and Zanzibar immediately after the word Tanzania appearing at the end of clause two.*

Naomba nisome Katiba kifungu cha 98(b) kwamba Muswada wa sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii au masharti yoyote ya sheria yoyote yanayohusika na jambo lolote kati ya mambo yanayotajwa katika orodha ya pili kwenye nyongeza ya pili. Naomba nisiendelee niyasome mambo yaliyopo katika orodha ya pili, orodha ya pili nitasoma kifungu cha 7, orodha ya mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utafiti ni suala la Muungano na suala la Muungano hata Mwanasheria Mkuu mchana alizungumzia habari ya uvuvi wa *deep sea. Research* haiangalii huyu samaki yupo juu sana au yupo chini sana, kama ni suala la Muungano

hamuwezi kufanya *research* ikafanyika *mainland* peke yake, na iko kwenye Katiba, ipo kikatiba hii, haya ni mambo ambayo yapo kikatiba kwa hiyo sheria hii inatakiwa i-*operate* na Visiwani, Tanzania Bara na Visiwani. Kwa suala tu kwamba suala la utafiti ni suala la Muungano na ni suala la Kikatiba ambalo liko ndani ya Katiba kifungu cha 98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mabadiliko ninayoomba yafanyike katika muswada huu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *amendment* ambayo inapendekezwa na Mheshimiwa Mbunge ina-*assume* kwamba suala la utafiti ni suala la Muungano, lakini ukweli wa mambo, hapa hatuzungumzii utafiti kwa ujumla wake, tunazungumzia utafiti katika maana ya Taasisi ya Utafiti katika masuala ya uvuvi na uvuvi sio jambo la Muungano. Kama tungekuwa tunazungumzia Muungano, kwa hiyo kitu ambacho ni cha Muungano ni utafiti katika ujumla wake. Lakini ikija kwenye utafiti wa masuala ambayo sio ya Muungano, hasa pale sheria inapotaka kuunda taasisi ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambayo ni taasisi ya Tanzania Bara, muswada ule hauwi umevunja Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hatupendekezi kubadilisha *application* ya sheria ifanyike Zanzibar kwa sababu Zanzibar kwa masuala ya uvuvi ina sheria zake zinazojitegemea. Tunakutania kwenye bahari kuu ambayo kuna *Deep Sea Authorities Act* ya mwaka 2007, lakini kuhusiana na utafiti hasa wa uvuvi kwenye *territorial water* ambayo ndiyo sheria hii ina-*apply* sio jambo la Muungano, kwa hiyo hatupendekezi ibadilike. Ahsante.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kwamba tunakutania kwenye *deep sea* ambako nako kuna samaki ambao wanaweza wakafanyiwa *research* sidhani kama kuna mpaka wowote unaoonesha hapa tumekwenda *deep,* hapa tusiwe *deep* kwa suala la *research.* Kama unafanya *research* huhitaji kuweka mipaka ya *research,* hii *institute* ifanye *research* mpaka Zanzibar. Na kifungu cha 98 kimesema jambo lolote, kubadili jambo lolote ndani ya Katiba hii na katika mambo ambayo yanataka kubadilika ni pamoja na *research* ambayo tumeungana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nitoe hoja Wabunge tujadili suala hili kwa pamoja. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini, Mwanasheria Mkuu na Mheshimiwa Yussuf, wanatosha hawa. Tuanze na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaonesha mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba yetu haijawahi hata siku moja kuonesha mipaka ya Tanganyika. Sasa kama chombo hiki kinaundwa katika Wizara ambayo ni ya Tanganyika kikafanye utafiti, kama ni utafiti wa masuala ya samaki ni lazima kama itajikita kwa Bara peke yake basi na mipaka ya maji ya Tanganyika lazima ionekane, ndiyo kwa msingi huo tunasema haiwezekani hiyo taasisi ikaundwa kwa ajili ya kufanya utafiti kwa maji ya Tanganyika peke yake, kwa sababu aidha, mnakubali kwamba nchi hii sasa mnaiendesha kwa mfumo wa Serikali tatu au mnakubali kwamba hiki chombo kuundwa kwa mfumo huu ni kosa la kiufundi na kwa hiyo marekebisho yafanyike kifungu kiondolewe kabisa au sheria hii izingatie matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nadhani inapofanyika mambo kama haya ya kutaka kuibagua Zanzibar na Tanganyika, naomba muwe waangalifu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juzi tu unafanyika utafiti wa mafuta na gesi, watafiti wale wakiongozwa na Jeshi la Jamhuri ya Muungano walikuja mpaka Pemba walikuja kufanya nini kama masuala haya hayamo Zanzibar inatolewa. Lakini pia meli zinazokuja kufanya uvuvi haramu, mambo ya *fishing, diving, snorkeling* zinakuja mpaka kule, ulinzi ni suala la Jamhuri ya Muungano, lakini vilevile mipaka hii ya baharini mtaigawa vipi kwamba Zanzibar mpaka wake unaishia hapa na Tanganyika mpaka wake unaishia hapa mfanye utafiti kwenye eneo lenu tu la Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunapofanya mambo kama haya yanaweza yakaleta athari katika suala zima la Muungano. Sasa kama mnaamua hivyo, mfanye iwe ni suala la Muungano turudini kwenye Serikali tatu basi, mfanye mambo yenu ya Tanganyika tufanye mambo yetu ya Zanzibar halafu tufanye shirikisho, kwa sababu suala hili linaleta matatizo.

Kwa hiyo, suala la utafiti wa uvuvi au masuala ya baharini hili ni suala la muungano na tusivunje Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nilipata fursa ya kulifafanua asubuhi. Ambacho naweza kusema ni kwamba Katiba iko wazi, tumefafanua asubuhi, Naibu Waziri amefafanua. Hivi masuala ya kilimo ni ya Muungano, masuala ya uvuvi ni ya Muungano? Tumezungumza juu ya *deep sea fishing,* kama mtu anataka kufanya utafiti kwenye *deep sea fishing* zitatumika taratibu zilizopo kwenye hiyo *Deep Sea Fishing Act* na tumeeleza hayo ni kwa sababu tunakwenda ndani sana kule tunapakana na mataifa mengine, na hilo eneo la bahari kuu sasa linasimamiwa na Sheria ya Umoja wa Mataifa *(The United Nation Convention on the Law of the Sea).*

Sasa haya mnayoyataka ndiyo maana ninasema Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane tu hapa, sheria yenyewe ambayo tumekusudia kuifuta kama mtairidhia tuifute, imekuwa ikitumika upande mmoja, tunaiboresha leo kwa nini mnasema kwamba sasa iwe ya Muungano, na Zanzibar wana sheria yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge naomba sana kwa sababu hili hatuwezi tukaliingiza leo humu ndani, la sivyo itabidi turudi kwenye Ibara ya 98 ya Katiba ambayo sasa na huo hauwezi kuwa Muswada wa kawaida kama huu, ni Muswada unakuja Muswada mahususi wa mabadiliko ya Katiba.

Kwa hiyo Waheshimiwa naomba kwa heshima zote niwashauri, naombeni sana hili tukubali mapendekezo ya Serikali jinsi yalivyo. Haiwezekani kwamba ninyi wakati fulani mnataka Serikali tatu halafu leo mnajifanya sijui mnakuwa vitu gani, haiwezekani, urafiki huu na watu wa Zanzibar umetoka lini, waulizeni watu wanaotoka Zanzibar chama kingine walioko huku upande wa huku, haiwezekani. Kwa hiyo, mnataka kuichanga tu hapa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge wayakubali mapendekezo ya Serikali jinsi yalivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago funga hoja yako.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na hoja inayotolewa ya kukataa mabadiliko haya kwa sababu kimsingi samaki hawana mipaka. Ndani ya bahari huwezi kusema huyu samaki yuko Visiwani na huyu samaki yuko Bara, unapofanya *research* yako utafanya *research* na samaki aliyetoka Visiwani akaingia Bara bila kujua huyu samaki kaingia huku au katoka kule.

Kwa hiyo, nashangaa Mwanasheria Mkuu anaposema tuvunje, huku ni kuvunja Katiba, tukubaliane tuvunje Katiba na iwekwe kwenye *record* kwamba tunatengeneza huu muswada ambao unavunja Katiba. Kama kuna uvuvi wa *deep sea fishing* ambao *reseach* yake inatakataa huu muswada umesema… *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**TAARIFA**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Taarifa… sasa hii *Lake Victoria* tumepakana na Kenya na Uganda. Ziwa Tanganyika ina nchi nne…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hajaruhusiwa!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** …Ziwa Malawi ina nchi tatu, utaingizaje hii ukasema tu Zanzibar…

**MBUNGE FULANI:** Hajaruhusiwa!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** …Malawi, *DRC Congo*, Burundi, Zambia, Kenya, Uganda, Ziwa Victoria…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy…

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Unasemaje hapo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago, endelea na hoja yako uifunge.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya Mheshimiwa Keissy wala siwezi kuyazungumzia kwa sababu yako nje ya utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* yangu iko hivi, tunapozungumzia suala la mipaka kwenye ziwa au bahari, tukiwa baharini hapa kuna nchi moja, kuna Visiwani na Bara, utafiti huu haujazungumza hautashughulikia *deep sea,* utafiti huu utakwenda mpaka *deep sea* ambako tutakuja kukutana na Zanzibar humo humo kwenye *deep sea,* ni *research, research* haiwezi kutenga huyu samaki wa chini na huyu samaki wa juu sana. Kwa hiyo, lazima hii *research* itakwenda mpaka Zanzibar visiwani, *otherwise* mtuambie itapakana tutaweka mipaka sehemu gani ya kufanyia hiyo *research* ndani ya bahari. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Waliosema siyo wameshinda na kifungu kama kilivyo na marekebisho ya Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 2

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 2 kina marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona marekebisho ya Serikali, lakini hiyo hoja ambayo ilikuwa inajadiliwa ndiyo hoja ambayo nilikuwa nazungumzia hapa, kwamba sheria inasema itafanya kazi Tanzania Bara peke yake na maelezo yangu ni kama alivyokuwa ametoa Mheshimiwa Bilago. Na kwa sababu mmeamua kusimamia kuvunja Katiba kwa kupiga kura kwa mdomo bila hata kuhesabu, bado maelezo yangu ni kwamba sheria hii na bahati mbaya sana tunapotosha watu hapa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaunga mkono upotoshaji, kwa sababu hapa kwenye Katiba imesema tu utafiti, haikueleza habari ya *deep* wala *over* wala chochote kile na hakuna maelezo yanayosema kwamba unapozungumza utafiti kutakuwa na makundi kwamba kuna utafiti utafanyika Zanzibar na utafiti utakaofanyika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachokuwepo hapa ni kwamba kwa sababu najua Katiba inasema Ibara ya 98 kulipaswa kuwe na huu Muswada uanzie Zanzibar na wenyewe wajadili na Bunge, lile Baraza la Wawakilishi lipitishe kwa 2/3 halafu lije huku tupitishe 2/3 ndiyo ije kuwa sheria, na ukweli ni kwamba tunachokifanya hapa … bado tunasisitiza kwamba hii sheria ingepaswa ni *pre-mature* na kama Serikali haikujiandaa ilipaswa kuirudisha. Vinginevyo mkubali kwamba mnatumia wingi wenu vibaya kupiga kura hapa kuvunja Katiba ya nchi, na sidhani kama ni sahihi kupiga kura kwa kuvunja Katiba ambayo kila mtu hapa ameapa kuitii. Kwa hiyo, bado tunasisitiza kwamba hii sheria kimsingi inapaswa kutumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na si vinginevyo kwa namna ilivyo hapa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana Mheshimiwa hakuwepo wakati tunalijadili hili lakini labda kwa ufupi sana nieleze msimamo wa Serikali kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumika neno utafiti haifanyi taasisi hii iwe ni ya Muungano, leo hii kama tukizungumzia kuhusu utafiti kwenye Serikali za Mitaa haimaanishi kwamba Serikali za Mitaa inakuwa ni suala la Muungano, leo hii tukizungumza kuhusu utafiti kwenye maliasili, kwa mfano *TAFORI* haimaanishi kwamba leo hii *TAFORI* inakuwa ni taasisi ya Muungano, haimaanishi kwamba leo hii tukifanya utafiti kwenye *TAWIRI,* basi *TAWIRI* inakuwa taasisi ya Muungano, haimaanishi leo hii…

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mifano hii kwa sababu inaelekea ni suala la la uelewa zaidi, kuna maji ya aina tatu; kuna kitu kinachoitwa *inner water* (maji ya ndani), kuna kitu kinachoitwa *territorial sea* (maji ya kitaifa), kuna kitu kinachoitwa *exclusive economic zone* yanaitwa maji ya kiuchumi na *exclusive economic zone,* utafiti ule ambayo ni sehemu ya Tanzania Bara na *inner water* itafanywa na *TAFIRI,* lakini ikija kwenye kitu kinachoitwa *exclusive economic zone* chombo ambacho kinahusika ni cha kimuungano kinaitwa *Deep Sea Fishing Authority* na huko ndiko utafiti unafanyika na hicho chombo kinakuwa na kazi ya kusimamia utafiti. Lakini niseme tu kwamba wenzetu Wazanzibari fahamuni kwamba haimaanishi kwamba

*TAFIRI* haiwezi kusaidia kwenye utafiti ambao unafanyika Zanzibar lakini ili mradi ni kwa makubaliano maalum na taasisi yenye mamlaka ya utafiti Zanzibar. Kwa hiyo, bado utafiti tutashirikiana lakini kama ni taasisi hii ni taasisi ya Tanzania Bara na si ya Muungano. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasema maelezo yote anayozungumza, kuhusu *zone, whatever* hayapo humu kwenye sheria, hakuna mahali inasema kwamba ikifika wakati huo sasa hiyo sheria itatumika haikutajwa mahali popote nah ii ni sheria inatungwa na hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wenzetu wa Zanzibar wapo hapa kuangalia maslahi ya Wazanzibari wenzao na hili jambo hapa linataka kupokwa.

Kwa hiyo, bado nasisitiza kwamba naomba nitoe hoja Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono tulijadili jambo hili ili kama maamuzi yamefanyika rekodi iwe kwamba sisi tulipinga uvunjaji wa Katiba ambao unafanywa na Bunge hili kwa sasa. Naomba nitoe hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Mbunge wa Temeke, Mheshimiwa Mbogo, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Kubenea. Haya, tunaanza na Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo yanayotolewa na Serikali kwamba huu Muswada unatumika Tanzania bara peke yake, ibara ya 2(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza wazi eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni eneo la Tanzania Bara, ni eneo la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo. Katiba hii hapa, inaeleza bahari kwamba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano na utafiti huu unaenda kufanyika baharini na bahari yenyewe imetajwa kwamba ni suala la Muungano sasa mimi nashangaa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasimama hapa, anapotosha Bunge. Suala la utafiti limeelezwa katika nyongeza ya Katiba hii. Halijaelezwa kwamba ni utafiti wa maliasili, haijaelezwa kama utafiti wa hiki, limeelezwa kama utafiti suala zima la utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala hili hata ukisoma huu muswada wenyewe na maelezo ya Waziri haya ukisoma kuna vyombo vimetajwa humu kama Tume ya Sayansi na Teknolojia, kwenye Katiba hii hiki chombo ni chombo cha Muungano ambacho kinatajwa katika huu utafiti, sasa ni vizuri watu wakaheshimu Katiba. Tusije sisi hapa tukawa sehemu ya watu ambao tunapinga Katiba. Tukishakuvunja sisi Katiba humu ndani nani nje ataheshimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Hoja yangu haiko sana kinyume na Mheshimiwa Kubenea ni kwa sababu na mimi nilikuwa napitia Katiba hii kwamba hoja yetu namba moja tulikuwa tunajaribu kuainisha Tanzania ni nini? Ni nchi moja, hiyo ni Ibara ya 1 kabisa ya Katiba tunayoilinda, ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini ukija kwenye Ibara ya 2 ambayo inaonyesha ile mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakwambia eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu yake ya Bahari, weka *capital* Bahari ambayo Tanzania inapakana nayo.

Sasa unakuta kwa mfano hata Mheshimiwa Keissy hapa alikuwa amejaribu kutoa hoja kwamba Tanganyika kule, Victoria alikuwa anatuunga mkono sisi kwa sababu ndiyo maana hayajajumuishwa hapa ndani. Kwa hiyo, kwa hoja ya Keissy ambayo alitaka kuijadili hapa anazungumzia kwamba yaani ukiiondoa Zanzibar maana yake Zanzibar ni nchi kamili yenye Mamlaka sasa kama Zanzibar ni Nchi kamili yenye mamlaka basi na sisi hapa tunakuja na hoja ya kudai Tanganyika, lakini ukishazungumzia utafiti na ndiyo maana kila siku tumekuwa tukilalamikia kwenye nyongeza ya 18 imejadili utafiti sasa mimi naweza kuelewa *concept* ya utafiti uliyoweka hapa. Iliwekwa *concept* ya utafiti wa mafuta pamoja na gesi, lakini ukija na hoja kama iliyopo sasa hivi utafiti, tunapojadili kuhusu samaki waliopo ama vile viumbe vyote vilivypo baharini, tunajadili suala linalohusu Muungano.

Kwa hiyo, ni wazi tuliapa kuilinda na kuitetea Katiba hapa sisi Wabunge wote sasa tusiwe sehemu ya kuivunja hii Katiba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoteze sana muda kwa sababu maelezo ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Naibu Waziri kuhusu ile mipaka iko *very clear* na ndiyo maana kuna mipaka kati ya Dar es Salaam na Pwani, kuna mipaka kati ya Bahi na sehemu zingine, kwa hiyo, naona kinachowapa shida ni mipaka kati ya Pwani huku Bara pamoja na Zanzibar. Sasa kama hicho kinawapa shida siyo tatizo. Utafiti utafanyika kulingana na mwisho wapi Tanzania Bara inaishia. Nenda kwenye ramani utaukuta.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa upande huu.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Kwa hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, upande huu Waheshimiwa nawaombeni sana. Mmechangia mara mbili upande mmoja wamesikiliza. Muacheni na yeye, usinyanyue vidole namna hivyo. Ukivunja au ukileta madharau kwenye mamlaka kuna tatizo, nakuombeni jamani, tunatunga sheria. Wachache waseme, wengi wapitishe ndiyo demokrasia ilivyo na naombeni meza ikiwaheshimu na ninyi mjiheshimu. Hatutaki kuchukua maamuzi mengine ambayo hayana malengo ya umoja wa Bunge hili. Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sheria inavyosema kwamba itatumika Tanzania Bara si kwamba itavuka mipaka ya Tanzania Bara haitavuka, kwa hiyo lazima muelewe hiyo *logic* msilazimishe tu kulingana na mambo mengine yanavyosema. Naunga mkono hoja ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa hapa tunalolifanya ni kuitetea hii Katiba ambayo tuliapa kuilinda na kuitetea humu Bungeni. Hili jambo liko wazi kabisa. Tuna mipaka ya mikoa, tuna mipaka ya vijiji lakini inapokuja suala la maji ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni suala la Jamhuri siyo suala la upande mmoja wa Bara au wa Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waziri katika sheria hii angetusaidia sana angeweka kipengele humu aseme kwamba, kwa mujibu wa sheria hii, maji ya Tanganyika yataishia Chumbe. Ukishatuambia hivyo umemaliza ni lazima tujue *jurisdiction* ya hii sheria ni wapi sasa ukituacha tu hivi tuogelee unatuambia ya Bara lakini maji yenyewe ni ya Muungano tunakuwa hapa hatuitendei haki Katiba hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo ni vzuri tukaacha ushabiki katika hili, tuungane katika kuitetea hii Katiba ama tuingize au tutoe kwamba tuunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara ili tuweze kuingiza haya marekebisho kwa sababu hakuna sehemu ambayo inatofauti kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mtolea. Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao wanazungumza jambo hili ni vizuri wajibu kwanza hoja muhimu. Suala la mafuta na gesi ni suala la Muungano, lakini tulifika mahali Bunge hili tukaamua ya kwamba suala la mafuta na gesi sasa halitakuwa suala la Muungano na tukatunga mpaka na sheria na mafuta na gesi yanapatikana baharini, sasa wajibu hiyo hoja kwamba hiyo mipaka ya bahari wanayoizungumza tutakapokuwa tunafanya utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi tutaupata wapi mpaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hilo wakilijibu na lingine ambalo wanatakiwa wafahamu kwamba, tunayo taasisi ambayo inafanya utafiti wa Bahari Kuu na inafanya kazi yake vizuri sana ile Taasisi ya Sayansi ya Bahari. Shughuli zote za tafiti ambazo zinatakiwa kufanyika Bahari Kuu zinafanywa na hii taasisi na wanatafiti mwenendo wa bahari na wanatafiti viumbe vyote vilivyomo ndani ya bahari vikiwemo samaki na vitu vyote. Kwa hiyo hatuna pungufu lolote lile ukizungumza suala la utafiti wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile wajue kwamba tunae *coordinator* wa utafiti wote wa kisayansi ambaye ni *COSTECH*. *COSTECH* anafanya *coordination* ya tafiti zote ambazo zinafanyika za kisayansi hata katika *sharing* ikitokea ya *information* ya Bara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinaratibiwa na *COSTECH* kwa hiyo hakuna mapungufu yoyote hapa katika hoja hii ambayo inazungumzwa ukishajua kwamba tunayo Taasisi hiyo ya…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu. Mheshimiwa Mwigulu, ajiandae *Attorney General.*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Mwanasheria Mkuu alishaongea vizuri sana kuhusu jambo hili na pili Naibu Waziri wa Kilimo amesema vizuri na hizo ndiyo *definition* halisi. Ninachokiona kinachotupa shida hapa ni baadhi yetu tunatafsiri sheria hii na tunatafsiri muelekeo wa sheria hii kiugomvi ugomvi, kimafarakano farakano ndiyo inayotupa shida kushindwa kuelewa ni wapi tunakoelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia baadhi ya sheria ambazo tuliwahi kutunga, tunazitumia kufuatana na *perspective* kwa mfano; sheria ya suala la *NBS* ni jambo la Muungano lakini tunapotaka kutafasiri sehemu yake na maeneo ambayo tunataka tuitumie sheria ile upande mmoja wala hauathiriki na ndicho alichosema Mwanasheria Mkuu na ndicho alichosema Naibu Waziri kwa maana hiyo ndugu zetu hii tunayoitunga, kuna sehemu ambayo tunaunganishwa kama Taifa moja, yako maji ambayo tunaunganishwa kama Taifa moja,

hatuyahitaji kuyatungia sheria yake maalum na yako ambayo tunayatumia kama Tanzania Bara hatuhitaji kuyatungia sheria maalum lakini ninyi shida mnatafsiri huku mkiwa na tafsiri yenu ya kitofauti ya kitimu kenu tu ambako ndiyo kanawasumbua na mnatusababisha tukwame wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo hii mnasumbuliwa na jambo moja tu la mpaka hata ndugu yangu Mtolea na wewe inakusumbua, hivi mlipokuwa mnasema Serikali tatu ile mipaka mngeitoa wapi kama hamna mipaka? Mngei-*define* vipi na mngetoa wapi? Kwa hiyo mlikuwa mnaongelea kitu ambacho bado hamjakijua? Mimi niwaambie kwa hili hebu tuendeni na nia njema wala tusipoteze muda tuendeni na nia njema……..

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...na yale ambayo hatuungani tutatumia katika sehemu hiyo ambayo hatuungani.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHARIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo ni dola lazima nisimame kwa nguvu zote, moja, kutetea Katiba lakini inakuwepo tu kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hoja kama hii wanayoileta wenzetu wanataka kufanya Zanzibar isiwepo na hapa ni la Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ibara ya 1 inasema hivi; Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vilivyozunguka na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwa hoja hii ni kwamba Zanzibar haitakuwepo kwa sababu tu ya bahari, hatufanyi hivyo jamani. Hiki kinachozungumzwa kwenye Ibara ya 2 *sub article* 2 ya Ibara ya 2 inayotaja eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hii ni mipaka. Katika *international community;* katika Jumuiya ya Kimataifa hii ndiyo inayojulikana kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna mamlaka ya Serikali mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimegawana mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

Kwa hiyo hii hoja haina maana yoyote. Naomba mapendekezo yaliyoko kwenye muswada wa Serikali ndiyo Waheshimiwa Wabunge wayakubali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara, hitimisha hoja yako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru waliochangia hoja upande wa CCM walitusaidia sana wanaunga mkono hoja yangu kimsingi maana yake wanaonyesha kama tungezungumza habari ya Zanzibar katikati tungeweka mipaka na hiyo mipaka kwa sababu haipo maana yake Jamhuri inabaki kuwa ya Muungano jambo la kwanza.

Jambo la pili, maelezo ya Mheshimiwa Mpina alikuwa anazungumza ya kwake wala hakuchangia hoja yangu mimi sikuzungumza habari ya mafuta wala ya gesi mimi nimezungumza utafiti ambao umefanyika na utakuwa unafanyika juu ya samaki waliopo baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, hayo mapendekezo tunayozungumza ya sheria yanaleta utata walikuja nayo wenyewe. Hakuna maelezo yoyote ambayo yanasema kwenye sheria hii kwamba utafiti utakaofanyika kuna sheria nyingine ya Bahari Kuu itatumika, hii haitatumika hakuna hayo maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne na la mwisho, kama ndugu zetu wameamua kwamba wao wanavunja Katiba kwa kupiga makofi mengi sana hapa waendelee kuvunja Katiba naomba Bunge liamue. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunahoji wanaokubaliana na marekebisho ya Mheshimiwa Waitara waseme ndiyo. Wasiokubaliana na marekebisho ya Waitara waseme siyo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Kura zihesabiwe, sisi tumeshinda kura zihesabiwe.

**MWENYEKITI:** Waliosema siyo wameshinda. Kifungu hichi kinapita kama kilivyo?

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 3 kina marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MWENYEKITI:** Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye hii *clause* ya kwanza hapo kwenye *bio-safety* napendekeza kwamba tutoe neno *of fish* bali tu-*substitute* na *aquatic organism and a respective habitats* kwa sababu *bio-safety* haiangalii samaki peke yake au wanyama wa baharini peke yake lakini kuna viumbe vingine vya baharini ambavyo ni mazalia au chakula au maeneo ambayo wale samaki na viumbe wengine wapo kwa hiyo hatuangalii tu *bio-safety* ya *fish* peke yake bali na viumbe vyote vinavyopatikana baharini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachosema Mheshimiwa Dkt. Sware kwamba *bio-safety* katika muktadha wa maji ina-*apply* zaidi, inafanya kazi zaidi kwenye viumbe vingine na siyo kwenye samaki tu lakini kwa nini tumeleta katika hali hii tumesema *fish* ni kwa sababu muswada huu unahusu zaidi mambo ya uvuvi. Kwa hiyo katika muktadha wa muswada huu tunapozungumzia *bio*/maisha tunamaanisha samaki hatumaanishi mimea au kitu kingine kwahiyo anachosema yeye ni kweli, lakini sheria inavyotungwa inatungiwa kitu *specific* ndiyo maana *definition* kwa mfano ya *bio-safety* hapa ukiipeleka labda kwenye Sheria ya Afya inakua na maana nyingine, ukipeleka tuseme kwenye Muswada wa Misitu inakuwa na maana nyingine kwa hiyo katika muktadha wa kitu tunachotungia sheria *fish* bado sisi tunaona kwamba iko sahihi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilivyo *propose* kwamba tuandike *aquatic organisms and a respective habitats* nilikuwa nina maana hiyo hiyo kwamba hapa tunapoongelea *Tanzania Fisheries Research Institute* na kwenye hii kwa huku chini kuna *definition* ya *fish. Fish* haimaanishi samaki, tunapoongelea uvuvi hatuongelei uvuvi wa samaki lakini na viumbe vilivyo baharini na *research* inayopendekezwa na hii *institution* haiongelei samaki peke yake. Unapofanya utafiti wa huyo samaki na viumbe vingine vya baharini vinaingiliana, kuna ikolojia inabidi uangalie samaki anakula nini. Kuna samaki wengine wanakula mimea au wanakula *argie* na vinginevyo. Kwa hiyo, unapoongelea *bio-safety* huongelei samaki kama samaki lakini viumbe vyote vilivyo mle yaani viumbe hai vya baharini ni hivyo Mwenyekiti kwa hiyo naomba mui-*take*, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hoja ni ya msingi lakini.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimemuelewa Dkt. Sware na tunalikubali marekebisho hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, mnaona Serikali sikivu, mambo mazuri yanakwenda. Kifungu hiki kinaafikiwa na marekebisho ya Serikali na mheshimiwa Dkt. Sware. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aaah! *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH:** Kifungu cha 5 kina marekebisho ya Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia kwenye kifungu hiki cha 5(6)(b) kwamba tutoe neno *fish* ila tu-*replace* hili neno *fish* na *aquatic*.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali ina mantiki katika muktadha huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa kifungu hiki kinapita na marekebisho ya Dkt. Sware?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 6 kina marekebisho ya Serikali, Mheshimiwa Mmasi na Mheshimiwa Mbogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(6)(d) tumeruka.

**MWENYEKITI:** Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa na-*propose* pia neno *fish* inayosema tuondoe neno *fish* tuweke *aquatic organisms* kwa sababu *fish* ilikuwa mara ya kwanza haija-*include aquatic flora* ilikuwa haijaangalia mimea ya baharini.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** 5(6)(d).

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mapendekezo anayoyaleta Mheshimiwa Dkt. Sware hapa kwa kweli ukitazama *definition* ya *fish* kama ilivyokuwa *defined* huku kwenye *definitions* ya *fish* utakuta kwamba anayoyapendekeza tuyaongeze hapa yako *actually* kwenye *definition* ya *fish*. Kwa hiyo, nilidhani kwamba tusingeendelea niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tazameni ukurasa wa nne kwenye *definition* ya *fish* mtakuta hayo maneno yote ambayo yanapendekezwa kuongezwa hapa yapo, unaona? Kwa hivyo kwa maana ya neno *fish* tungekuwa tunazungumzia kitu kingine tofauti na *fish as defined* tungeweza kweli ku-*allow* sasa haya mabadiliko ya kila mahali kuweka *aquatic* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa maana hii tunamuomba tu na yeye atuache tuendelee mbele kwa sababu tutakuwa tunafanya *repetition* ya jambo ambalo limeshakuwa *defined* tayari tena tunalitengenezea *definition* ndani ya sentensi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Dkt. Sware Waziri yuko sahihi nakuomba ulikubali kwasbabu limeshakuwa *accommodated.*

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nifanye tu *clarification* na niiombe Serikali hii *definition* ya *fish* haijai-*include* mimea. Kwa hiyo, unapoongelea *either* uvunaji au nini, kote huku mbele utaona kwamba sehemu ambayo wanasema *fish* basi waongeze na neno *aquatic flora.* Kama basi wanaona kwamba itakuwa ni ndefu waseme tu *aquatic organisms. Definition* haina mimea Waheshimiwa, wamesema hapa kwenye *definition* ya *fish*, *means all forms of aquatic and amphibians life including finfish,* wakataja wanyama, jamii ya wanyama sio mimea, ni hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha hoja yetu hapa tulisema kwamba tumekubaliana na ile neno *aquatic flora* ili li-*capture* kila kitu ambacho kitakuwa katika *context* ya hii sheria. Sasa tukiendelea na hizi *definitions* maana yake tutakuwa tuna-*dilute* jambo lile ambalo tulikwisha likubali mwanzo. Unaelewa vizuri Mheshimiwa Dkt. Sware kwamba ulikwishaleta lile pendekezo kama Kambi ya Upinzani na sisi tulilikubali tukasema kwamba kweli *aquatic flora* inakuwa *or encompassing all source of marine life* ambayo tuna *intend* kutungia sheria hii kwa maana ya *research.* Sasa tunapoendelea tena na kuongeza *definitions of an agreed definition* tunakuwa tu hatujengi sura nzuri ya muswada huu na tungekubali tu kwamba *much as* lile jambo limekwisha kuwa *accommodated,* tusonge mbele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Na ushauri mwingine Dkt. Sware wakati una-*present* hoja zako uzi-*present* zote sababu uki-*recall* kifungu hiki tumeshakipitisha. Kwa hiyo, ungeyasema yote kwa pamoja na ushauri mwingine hizi *amendments* mzipeleke kwa Wanasheria sababu watawasaidia namna gani kuzi-*draft* ili ziwe *friendly* kwako na kwetu.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, ndiyo nilichokuwa nakisema pale kunaposoma *fish* basi kusome *aquatic organisms* kwa sababu *definition* ya *fish* haijataja mimea ndiyo maana tukaweka *component* ya nini cha *aquatic flora* ambacho Mheshimiwa Waziri amekikubali. Sasa huku mbele bado kuna neno tu limesema *fish* na halijaongeza neno *flora* ndiyo maana nasema basi tu-*stick* na *aquatic organisms* yaani ni vyote vilivyoko hai baharini au kwenye maji ya…

**MWENYEKITI:** Serikali imeshakubali lakini Mheshimiwa Dkt. Sware. Serikali imeshakubali na kifungu hiki tumeshakipitisha. Tuendelee.

Ibara ya 6

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 6 kina marekebisho ya Serikali, Mheshimiwa Mmasi na Mheshimiwa Mbogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nilikuwa napenda kwenye *clause 6 (1)* tu-*insert phrase* inayo-*supplement* hii *statement (a)* ambayo nafikiri bado ina *hang* pale na *insertion* yenyewe inasema kwamba; *for the purpose or providing scientific data and information to enhance sustainable exploitation, management and conservation of Tanzania Fisheries.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana nyingine tukikubali kwamba hii sentensi ina-*hang* nina *suggest* pia tuiue *section (c)* kwa sababu naona hii ni *repetition. Section (a)* inaongelea kutekeleza na kukuza uchunguzi na majaribo ya utafiti wa uvuvi na viumbe vya majini kwa ujumla wake, lakini *section (c)* pale inaongelea kufanya utafiti na uchunguzi wa magonjwa ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaposema utafiti kwa ujumla wake ni pamoja na magonjwa ya samaki. Kwa hiyo, *comment* yangu ya kwanza ni kwamba *section (a)* ina-*hang* na ili tuweze ku-*maintain* hiyo *continuity* kama *section (b), (c)* na zinazoendelea kwamba kila jukumu linaonesha na *purpose* yake basi tu-*supplement phrase* kama nilivyoi-*suggest* kwenye *paper* yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uandishi wa sheria mara nyingine unaandika kitu cha jumla ili kuweza kuweka vitu ambavyo haujaviweka hapo, maana yake ukiweka *generally* kuna vitu vingine hapo inawezekana hujaweka kwenye hicho kifungu lakini vilevile unaweka vitu moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo (a), inaongelea kuhusu ujumla lakini (c) inaongelea kuhusu *diseases,* kwa hiyo sio kwamba ni shida kwa sababu tungeweza tu kusema kwamba itafanya kazi ya ku-*provide* kuhusu mambo ya *research generally* hiyo moja ikatosha kila kitu. Kwa hiyo, kuna maana ya kuweka vipengele moja moja. Kwa hiyo, nafikiri tuendelee kama ilivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa na nasema ahsante sana kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pia nilikuwa nina *concern* mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kama ilivyowekwa na mimi nimeafiki nafikiri hiyo *section (a)* bado ina-*hang* na kama ina-*hang* ili tuweze ku-*maintain continuity* kama tulivyoziendeleza hapo kila jukumu na *purpose* yake basi tu-*supplement* hiyo *section (a)* ili ilete maana iwe *complete.* Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri. Hoja Waziri anasema haina *ambiguity (a)* zimesimama *separately* katika nguzo zake peke yake.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu inazungumzia kuhusu utunzaji na ufugaji wa viumbe kwenye maji katika ujumla wake. Maana yake ni mambo ya *aquaculture* lakini vile vile kuna kitu kinaitwa *cage culture* kuna kitu kinaitwa *eco phonics* kwa hiyo imekusanya viu vyote lakini ile nyingine inayofuata inazungumzia kuhusu magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiri imejitegemea. Hii ni *aquaculture generally* na nyingine inazungumzia kuhusu magonjwa, sioni kama kama ni *contradictory* na iko *complete* hapa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mmasi kubali yaishe.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubali. Tuendelee.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 6(c) kwenye magonjwa sasa hapa uchunguzi kwamba unafanyika kwa samaki tu sasa nimependekeza iongezwe au neno libadilishwe kama alivyokuwa anasema hapa Dkt. Sware ili kwa sababu katika maji hatuna samaki tu lakini tuna viumbe wengine na wenyewe pia magonjwa yao yaweze kuchunguzwa. Kwa hiyo, isiseme *fish* tu, iseme katika lugha ya kitaalam kama ni *aquaculture* au mtasema ni *organic aqua* kama itakuwa ni namna hiyo kwa hiyo nafikiri Waziri anaweza akalichukua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kile kipengele cha *definition* tayari tulishatoa maana ambayo inajumuisha hata *aquatic flora.* Kwa hiyo, tayari tunapozungumzia samaki ilishabeba maana pana ku-*include* hata mimea. Kwa hiyo, sidhani kama kuna shida kama tukiendelea hapo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbogo, Waziri kajieleza vizuri sana.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri nimemuelewa vizuri kabisa ningeomba sasa kama anatuongoza namna hiyo basi kwenye kanuni aende akatoe maelekezo kwamba kama *somewhere* kama imetajwa *fish let us take as aquaculture or aqua something whatever* akaitaja kwenye kanuni lakini namuunga mkono.

**MWENYEKITI:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haina shida, kwenye kanuni tunaweza tukaweka *details* nyingi zaidi kuliko kwenye sheria. Sheria inakuwa ni *general* lakini Kanuni inaweza kwenda kwenye *specifics.* Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimwa Wabunge, na hii inakuwa *redundant* sasa, kwa *future* mtu yeyote mwenye suala la *amendments* ikishakuwa suala la *fish* akae. Serikali imeshalipokea hilo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH:** Kifungu cha 7 ina marekebisho ya Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH:** Kifungu cha 8 kina marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Waitara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mapendekezo yangu ya marekebisho yapo kwenye *second schedule* ambayo inataja *composition* ya hawa Wajumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza kwa sababu kwanza kimsingi naomba niipongeze Serikali kwamba angalau katika kile nilichokuwa nataka kwenye Sheria iliyopita ile ya mchana hapa imetaja vitu vingi sana ambavyo sheria itafanya kazi. Kama itasimamia hata ubora, itaangalia soko, aina gani ya samaki wafugwe na vitu vya namna hiyo. Sasa kwa sababu ya kazi hizo ambazo mmeziona pale, nikawa nashauri kwamba moja, sikuona kama kuna uwakilishi wa kwa mfano zile *Fisheries Researchers Organization;* sikuona uwakilishi wake hapa kwa sababu ......hazifanyi kazi, sasa ni muhimu ukawa na uwakilishi katika hii taasisi sikuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nikadhani kwamba unapozungumzia samaki unazungumza habari ya soko ambayo watakaofanya utafiti wanaweza hata wakaishauri Serikali vizuri kama hata bidhaa inaenda nje isiwe na madhara yoyote yale. Kwa hiyo, nikadhani kwamba kulikuwa na haja ya kuishirikisha taasisi yetu ya chakula, *Tanzania Food and Drug Authority* kuwa na uwakilishi hapa ili hata haya mazao ya samaki yakienda nje ina maana tuna

uhakika kwamba kule hakuna shida wakitunga labda hapa na sisi tufanye utafiti na tulithibitisha iko sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile hapa tumepitisha sheria mbili juu ya *chemist laboratory* na *professional* wale na wenyewe sikuona wametaja pamoja na watu ambao wanahusika na mazao ya samaki, lakini na chuo chochote maalum ambacho kina-*deal* na sayansi ya wanyama wa baharini hakuna uwakilishi hayo ndiyo yalikuwa mapendekezo yangu namna ya ku-*accommodate* katika shida hii. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mapendekezo anayoyaleta Mheshimiwa Waitara yote yako *captured* kwenye *schedule* yenyewe. Kwa sababu ukisoma wanaotajwa kwenye hiyo *schedule* ya pili, wote hawa anaowasema wapo na ni maana pana sio kama anavyojaribu kuiweka yeye, na kwa sababu labda tu arudie tena pale aangalie vizuri waliotajwa kule. Kwa mfano anasema…

**MWENYEKITI:** Unaendelea bado?

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Ndiyo. Mjumbe mmoja lazima toke Hazina, wajumbe wasiopungua watatu lazima wawe wataalam kutoka nyanja za uvuvi na kwenye viumbe kwenye maji. Sasa ile wataalam wa uvuvi na viumbe kwenye maji ni pamoja na mfano hao wanyama wa majini anaowazungumza Mheshimiwa Waitara. Naomba tu tuelewa kwamba hili jambo liko *taken care* vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hicho kipengele hapa, lakini kwa mfano nimetoa hoja hapa ya hizi sheria mbili wale watu *professional* wa maabara wale na Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Chakula, hakuna uwakilishi hapa. Vyuo vikuu ambavyo vina–*deal* na hii elimu kwa sababu unaunda taasisi ambayo hawa maprofesa wakiingia humu ndani kama wawakilishi nadhani watawasaidia katika ushauri hapa.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, namuomba tu arudie tena kutazama vizuri. Kwa sababu katika *composition* ile ya *board* wapo wawakilishi kutoka vyuo vikuu pia. Sasa kama hawa wapo huwezi kwenda ukachukua mtu kutoka Chuo Kikuu cha Sanaa kumuweka kwenye hii *professional board* ya namna hii, lazima watakuwa ni wanaotoka kwenye vyuo vikuu ambavyo vinafanya pia utafiti kwenye maeneo haya ya samaki. Kwa hiyo, nimuombe tu atukubalie tuendelee kwa sababu kila kitu anachokizungumza kiukweli kweli sheria imekizingatia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Waziri anasema kipo sahihi na wameshakuwa *accommodated* humu na kwenye sheria huwezi kuandika wote, Mheshimiwa Waitara na watoto wake wote humo humo, unasema familia ya Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Unaleta habari za Ilala Mheshimiwa Mwenyekiti!

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nisome hapa kidogo na mimi nadhani tunaenda vizuri tu. Hapa kwa mfano anasema; *not less than seven or more than ten other members* baada ya *Chairman of the Board; roman (i)* inasema *one member from Treasury; roman (ii) not less than*

*three members being expert in fisheries and aquaculture; (iii) one member from the Ministry responsible for fisheries; (iv) a law officer from Attorney General Office; (v) ambayo off course* amerudia ameandika *tena (iv) one member who has knowledge in economics as the Minister may deem necessary.*

Kwa hiyo unaona haya mambo yanazozungumzwa hayawakilishi. Ame-*capture* ile hoja ya wataalam kama kuna *experts* sawa, lakini nimesema kwa nini kusiwe na uwakilishi kutoka Mamlaka ya Chakula kwa sababu amezungumza kwenye sheria hapa kwamba hawa taasisi hii itashauri pia product hii na ubora wa samaki, ndiyo hoja yangu.

Lakini pili, tuna wataalam wa maabara hapa, kwa hiyo ni uwakilishi tu huu, hawa anaowazungumza hawapo hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua namna jinsi tunavyojadili Jedwali la Marekebisho la Mheshimiwa Waitara kidogo hatuendi vizuri. Tunajadili *second schedule* iliopo katika ukurasa wa 25; *second schedule* imetengenezwa kwa mujibu wa kifungu cha 8(3). Ilitakiwa tumalize vifungu vyote 39 halafu ndiyo tuje kwenye zile *schedules* na kumalizia na ndio maana watu wengine wanapata taabu wanashindwa hata kuchangia kwa sababu kidogo ameunganisha marekebisho yake katika kifungu cha 8 alitakiwa apeleke kwenye *second schedule* na sio hapa.

**MWENYEKITI:** Uko sahihi. Mheshimiwa Waitara funga hoja yako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kweli Mheshimiwa Waziri anachosema nimetoa mapendekezo na umesema mwenyewe hapa kwamba kama nazungumza kifungu cha 8 unazungumza *in totality* yaani nisirudi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesema *second schedule,* kwa hiyo naomba hiyo hoja kama Mheshimiwa Waziri hawezi kutoa maelezo kwa ku-*accommodate* angalau basi napendekeza tujadili. Nitoe hoja lakini nimeunga mkono maelekezo yako Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, umeridhika na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri, kwa hawa wataalam unaowataka wameshaku-*accommodate.*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** I-*move* mbele kwenye *schedule.*

**MWENYEKITI:** Ni *move* kwenye *schedule?* Haya.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Ibara ya 11 ina marekebisho ya Dkt. Sware na Mheshimiwa Waitara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! Nilikuwa na-*propose* kwamba sentensi ya mwisho ya kifungu hiki ambacho kinasema *prescribe upon the recommendation of the board* kitoke kwa kuzingatia kwamba tumuachie Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na ofisi inayohusika na utumishi wa umma wapange kiwango cha posho hiyo husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *practice* iliyopo ni kwamba Bodi huwa zinafanya mapendekezo kutegemea na hali ya taasisi yenyewe ilivyo na haya mapendekezo kwa sababu *these are public funds* yanapelekwa kwa Waziri, sasa Waziri kabla hajayaidhinisha ana-*consult* kwa *Treasury Registrar* ambaye ndiye *custodian* wa mashirika haya na baada ya kujiridhisha kwamba hayo mapendekezo hayawezi kuathiri *both ways* au kufanya taasisi isi-*function* au kuifanya taasisi i-*overspend* ndipo hapo uamuzi unapotolewa kwamba yapitishwe au yapelekwe vingine. Kwa sababu gani, tukilifanya hili jambo lazima liende kule Idara Kuu ya Utumishi kwanza bajeti za haya mashirika hazipitishwi na Idara Kuu ya Utumishi na tunapozungumzia *renumerations* hapa maana yake tunazungumzia bajeti ya mashirika haya. Kwa hiyo, ni vyema ibaki hivi hivi, Waziri anaepitisha bajeti ndiye aangalie matumizi anayotaka kufanyika kutokana na wajumbe wa Bodi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nime-*propose* hivi ili kutoa ule ukiritimba au kuleta ile hali ya utata kwa sababu wewe unapokaa unasema jipangie ulipwe kiasi gani lazima ile *level* itakuwa *scale* ile unayotaka kujilipa inakuwa juu. Sasa ili kutoa hiyo hali tuiachie Hazina inayoshikilia hizo hela ikihusisha wale wanaohusika na mambo ya utumishi wa umma au mambo ya *employees* nafikiri Mheshimiwa Angellah anatingisha kichwa anakubaliana na mimi, hiyo hali itoke. Tutoe tu hii sentensi sheria ibane, Bodi isiwe na *mandate* ya kujipangia nilipwe kiasi gani. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angellah.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiyaondoa hayo maneno mwishoni *upon the recommendation of the board* kwanza wao wenyewe ndiyo hawawezi kujipangia maslahi yao wenyewe, cha msingi Mheshimiwa Waziri ndio anayewapangia mslahi atashauriana na Msajili wa Hazina hatuwezi kusema vyombo vyote vitakavyofanya mashauri haya, lakini mwisho wa siku watawasialiana na mamlaka zinazohusika ikiwepo utumishi pamoja na mambo mengine. Kwa hiyo, bado *Treasury Registrar* inaweza ikabaki lakini yale maneno mengine ya mwishoni yanaweza kuondoka na bila kuathiri maana nzima ya kifungu hichi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware umekubali?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane tu kwamba hayo maneno yatoke yasichanganye.

**MWENYEKITI:** Mmekubali, Mheshimiwa Waziri, tunatunga sheria maneno yakitoka myatoe hapa hapa *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri yaani kuonyesha mwelekeo wa kukubaliana na hili jambo la Mheshimiwa Waziri wa Utumishi lakini bado nadhani ni *prudent* kwamba Waziri anayeshikilia bajeti ya ile taasisi na kui-*approve* kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina *(custodian)* wa shirika lenyewe wanatosha sana kufanya vitendo ambavyo havitaathiri utendaji wa taasisi. Lakini hili tunalotaka kulifanya la kuliondolea mamlaka hii Wizara maana yake ni kwamba jambo liamuliwe nje ya Wazira ambayo haihusiki katika kupitisha na kuandaa bajeti yenyewe.

Kwa hiyo, niombe tu watukubalie tuendelee kama ilivyo na tutakapofika hiyo hatua anayoisema Mheshimiwa Dkt. Sware kwamba sasa mashirika yote nchini taratibu zake za *remuneration* zinafanyika *centrally then that will be the time* ambapo tunaweza tuka-*accomodate* haya mambo. Lakini *as long as* sheria bado haijatoa hiyo ya mashirika yote kuwa *managed centrally in terms of remuneration* na *structure* tuiache hii sheria ibaki kama ilivyo.

**MWENYEKITI:** *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Tizeba lakini nadhani kidogo asome vizuri hatuyaondoi yale ya *Treasury Registrar* tutabakiza mpaka mwisho kifungu hichi kiishie *prescribed.*

Kwa hiyo, naomba na Mheshimiwa Dkt. Sware pia kwenye *recommendation* yako ufute maneno peke yake ya *upon the recommendation of the board* kwa sababu ukifuta neno *prescribed* mamlaka ya Waziri huku mwanzo *may* halafu mtakuta huku mwisho hakuna kifungu ambacho kinafanya *clausing,* kwa hiyo bado mwisho wa siku kifungu kitabaki kama kilivyo isipokuwa kitaisha pale kwenye *Treasury Registrar* halafu unaongezea yale maneno *prescribed,* unaondoa *upon the recommendation of the board.*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Tunaondoa *recommendation?*

**MWENYEKITI:** *No! no!* Mheshimiwa Waziri hebu ki-*phrase* kabisa sababu tunaandika sheria hatutaki baadaye huko ndio walete maneno yao.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Sawa sawa.

**MWENYEKITI:** Tukubaliane humu ndani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Sawa sawa, kitasomeka *the board members shall be entitled to such remuneration fees or allowances for expences as the the Minister may after consultation with the Treasury Registrar prescribed. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kubali yaishe tu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubali yameisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni sawa na ya Mheshimiwa Dkt. Semesi kwa hiyo imekuwa *accommodated* naondoa hiyo hoja.

**MWENYEKITI:** Kifungu hichi kinaafikiwa pamoja na marekebisho ya Mheshimiwa Dkt Sware, Mheshimiwa Waitara na Serikali. Waheshimiwa tupo kwenye Bunge tunaomba ndiyo au siyo?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 12 kina marekebisho ya Serikali, Mheshimiwa Mmasi na Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi niweze ku-*table* kama *amendment* zangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri kwenye kipengele clause 12(2)(a*) to delete the whole paragraph* na badala yake tu-*substitute* kwa *statement* ifuatayo kwamba; *the appointed Director General shall have first degree in fisheries aquaculture* or *marine science plus doctorate degree in related subject from a reputable and recognized higher learning institution.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo kwanza kama nilivyotanguliza mchango wangu wa jana ukisema kwamba *doctorate degree* ndio inaweza ika-*lead* taasisi kama hii kwanza nafikiri si sawa kwa sababu kwenye *doctorate degree what we can have there is only about the methodology and tools of analysis of that particular subject* ambayo mtu ameifanya. Kwenye *doctorate degree* huwezi kupata msingi wa ubobezi ambao unaweza kuendesha taasisi kama hii. Kwa maana nyingine ninashauri kwamba *primary* iwe *first degree in fisheries, aquaculture and marine science. Marine science* haikuwepo na ninasema hivi kwa sababu *fisheries* Mbegani wanatoa *certificate* ya *fisheries,* lakini pia SUA wanatoa *aquaculture first degree* na *marine science* inatolewa na *University of Dar es salaam*. Tukifanya *omission* ya *marine science it means* tunaweza tuka-*omit* kada maalum sana kwenye fani hii ambayo ninafikiri kwamba kwenye nafasi kama hii ni muhimu mtu akawa nayo katika *level* ya *first degree.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nikasema *plus doctorate degree* iwe ni *must* sio *additional credit* ni kwamba *plus doctorate degree in related subject* kwa sababu ninasema hivi unaweza ukapata mtu ambaye amefanya *Ph.D* kwenye *geographical information system,* kwenye *marine ecosystem* au amefanya *a GIS* kwenye *habitat* au amefanya *Ph.D development studies* ameangalia *fisheries* au amefanya *MBA* na ameangalia *marine*

*aquaculture*. Kwa hiyo, ninaomba kwamba iwe ni *plus doctorate degree in related subjects from* nimeongeza hapo *reputable and recognized higher learning institution.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoweka *reputable it means* tunaangalia *quality* kwa sababu tunazo *institution* ambazo zinatambulika lakini *not all of them* kwamba ziko *reputable,* kwa hiyo kwa nafasi kama hii na kwa uzito wa nafasi hii nafikiri kwamba Serikali ipokee ushauri wangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mawazo mazuri tu sana ya Mheshimiwa Mbunge, lakini katika *context* ya taasisi ya utafiti maana yake hapa hatuzungumzii *a service delivery institution,* tunazungumzia taasisi ya utafiti wa eneo maalum na ndio maana pamoja na ubobezi katika masuala yanayofanyiwa utafiti yaani hiyo ya kwanza kwa mfano anayotaka ifanyiwe *amendment* inamtaka huyu *Director General* awe na ubobezi katika masuala yanayofanyiwa utafiti yeye mwenyewe, lakini pia haishii hapo zinaongezeka tena sifa zingine *requirements* zingine, ukisoma (b) inataka *intergrity;* ukisoma (c) inataka *proven knowledge and experience of at least ten years in matters relating to fisheries or aquaculture* na *innovative* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *a combination* ya haya za hizi sifa hizi ndizo zinatupa mtu anayeweza kuongoza hii taasisi na asiishie kuwa na *professional inferiority* kwa sababu hili nalo lipo katika maeneo ya hivi. *This is an area of highly trained people,* kwa hiyo wangependa wawe na kiongozi *they can talk and speak the same language.*

Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba kweli *idea* yake ilikuwa ni nzuri lakini aiache hizi sifa zibaki kuwa *stringent* hivi hivi kama zilivyo kwa sababu *we are dealing with the specialized areas of research.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena kwamba msingi wa ubobezi katika taasisi hii siamini sana kama utaweza kujengwa kwa shule ya uzamivu, siamini lakini pia nilipotoa ushauri wangu haimaanishi kwamba tuna-*wave* hii *Ph.D requirement* hapana. *Ph.D* ndio maana nikasema *plus* kwamba *it's a must not an optional* kwa hiyo, ninashauri kwa nia njema kabisa kwa Serikali yangu ninaamini kwamba hii siyo *service delivery institution* na ninaamini kabisa hii ni sehemu ya utafiti na pale ndio maana nikasema *plus doctorate degree.* Ninasema hivi kwa sababu unaweza ukakuta mtu amefanya *Ph.D* kwenye eneo ambalo sio hili lakini ni mtu mzuri huwezi kumwacha mtu akifanya *let say* amefanya kwenye *GIS* anaangalia labda *climatic change and marine ecosystem* huwezi kumwacha mtu kama huyu lakini hapa umeambiwa kwamba *Ph.D* kwenye *area* mbili tu. Kwa hiyo mimi ninashauri ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwa nia njema kabisa ninafahamu mchango wake ni mchango chanya lakini ajaribu kuangalia hili suala kwamba msingi wa ubobezi katika taaluma hii ya tafiti…

**MWENYEKITI:** Ahsante lakini hivi kuna ubaya gani inaharibu nini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli haiharibu chochote isipokuwa ni kwenye weledi wa kawaida wa kuandika sheria. Unapoandika sheria hautaki kujaza vitu vyote vidogovidogo ndio maana ukisema kwamba mtu anakuwa na

*doctorate degree* kwenye mambo ya *aquaculture* na *fisheries* unafikiri huyo mtu mpaka afike pale atakuwa tayari ana elimu nzuri ya *fisrt degree* na *masters,* lakini vilevile kwa sababu leo hii tukianza kuandika *details* zote za huyu mtu inawezekana muswada huu ukawa *loaded* na vitu vingi sana. Kwa hiyo labda Mheshimiwa Mbunge atueleze kwamba…

**MWENYEKITI**: Siku hizi si mnaomba *degree* na *form four.*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Naam.

**MWENYEKITI**: Siku hizi si mnaomba vyeti vya *degree* na cheti chake cha *form four?*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana Mheshimiwa Waziri alisema hiyo ni sifa moja tu na hao watu ni kwamba wana-*compete* mpaka jina lake lipatikane kwa hiyo sio kwamba...yaani kuna vitu vingine vingi ambayo inatakiwa hakidhi.

**MWENYEKITI:** Nafikiri hoja ya Mheshimiwa Mmasi ni *valid* na hata mkisema mna-*accommodate part* ya maneno yake kwenye *first degree I don't see any harm in it.* Mheshimiwa Waziri tukubaliane yaishe twende. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo makofi yanani-*compel* kukubaliana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza kwamba kwenye hii *clause 12* tuongeze kifungu kidogo cha (2) ambacho kitasoma kwamba *without prejudice to the provisions of section 12(1) of this act the board shall recommend three names of persons who are suitable for appointment to be the Director General of the institute.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Dkt. hapa ndio *actual practice* ilivyo kwamba hizi *appointment* hazipatikani tu kwa kuchukuliwa Tizeba *from the street,* kwanza *initial process before recommendation to the appointing authority* inakuwa ni *on competitive basis* na kanuni zitasema hivyo, kwamba *names* ambazo zitakuwa *forwarded* kwa *appointing authority for appointment* lazima ziwe kwanza zimepatikana *through a competitive basis* na baada ya hapo ndio mmoja wao atakapokuwa ameteuliwa. Kwa hiyo, hatuna haja ya kui-*prescribe* ndani ya sheria huo utaratibu kwa sababu ndio utaratibu uliopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Waziri ile sasa tusiweke kwa sababu ni sheria na inatu-*guide* basi tusiache hiyo *loophole* ikawa wazi ila iandikwe kama nilivyopendekeza, watawa-*polish* wale wataalamu wa sheria hiki kifungu kiwepo ili iwe *very clear,* tusiache wazi.

**MWENYEKITI:** *No,* lakini kiko *clear* Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haipo *clear* Mheshimiwa mwenyekiti, kwa sababu kama ingekuwa *clear* nisinge-*recommend* kwa sababu sio kila mtu anajua kwamba Mheshimiwa Rais anapoteua anatumia *criteria* gani na nimeangalia kwenye mfano hata kwenye kitabu chetu hiki cha katika Sheria ya Utawala wa Bunge ya 2008 kifungu cha 7(3) kwenye kumteua tu Katibu wa Bunge, Kamishna anatoa majina matatu kwa Rais yale majina matatu ambayo yamekuwa yame *go through a process* ya ku-*employ* mtu, una-*apply for the job board* inakuwa kama *panelist* wanatoa the *top three*. *Top three* wanapelekwa kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais anatoa jina moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kinajitegemea kinasema; *the President shall upon such terms and condition as he may specify appoint the Director General from amongst persons with knowledge and experience.*

Kwa hiyo, maana yake hii hata imetupeleka mbali zaidi haiweki *prescription* ya watu watatu imesema *amongst person* na ikaendelea kutoa sifa, kwa hiyo, nafikiri tusiwe na wasiwasi kwa sababu sio kwamba anamchukua mtu mmoja tu watu wengi wanaangaliwa wenye sifa na ndio analetewa ateue.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware kubali yaishe.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naona tu ni lugha labda hazieleweki labda sasa nionge kitaratibu kidogo ninakubaliana na hiki kifungu jinsi kilivyo, ninacho-*recommend* kwamba tu-*add* hao Mheshimiwa Rais anaowa-*appoint* ambao wana hizo sifa wametoka wapi, ambao hata sisi wenyewe tunatumia hivyo yaani tusiache *loophole* tusiache nafasi tu wazi haibadilishi mamlaka ya Rais kuteua, tunaongezea tu pale kwamba tuna-*specify* tunajipanga vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Dkt. Sware uko utaratibu wa kiserikali wa *appointment* kama hizi uko kwenye *standing orders* kabisa. Rais anapelekewa majina yanapita kwenye ngazi tofauti, *vetting* wapi wapi mpaka inafikia Rais anaamua nani anayetaka kumchagua, anaweza kwa mamlaka aliyokuwa nayo Rais hayo majina matatu yanayokwenda hata moja asimteue, akamteua anayemwona yeye anafaa, nafikiri Serikali imekaa vizuri tu basi. Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kumpa *comfort* pia pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ukiangalia katika sheria ya Tume ya Utumishi wa Umma suala zima la *competition* lipo, lakini vilevile imeweka *specification* majina si chini ya matatu, Mheshimiwa Rais ndio anayopelekewa na ndio anateua kwa hiyo walau tayari *consideration* yake ipo katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Umma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Mawaziri husika sidhani kama inaleta madhara yoyote lakini inakuwa ni ule utawala bora, uwazi, kwa nini kunakuwa kuna *ambiguity* au ipo au haipo kwa nini hata ukitafuta Katiba, Sheria ya Utumishi wa Umma iko wapi kwa nini kisiwepo kitu kimoja sheria ikawa iko timilifu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware funga hoja yako.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Abee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware funga hoja yako.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Sasa...

**MWENYEKITI:** Mimi nafikiri kama bado unaishikilia unazo haki zako za kikanuni.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** *Okay...*

**MWENYEKITI:** Kama unafikiri una *give in,* umekubaliana na maamuzi haya sema nimekubali tuendelee na shughuli zingine.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasita kidogo kutoa hoja kwa sababu tutapiga kura iatasema ndio au hapana utasema wenye hapana ndio ikapita. Na sasa sitaki kwenda kiushabiki, tunachotengeneza hapa ni kwa ajili ya mimi, wewe na yule na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika kujenga ule utawala bora nafikri Mheshimiwa Waziri Kairuki naomba uni-*support* kwenye hili, tunataka tu kiwe wazi hakibadilishi *power of the President* kumpata mtu wake ila tunataka kila kitu kuwe kuna uwazi kusiwe kuna vikonakona na vi-*loopholes* za pale na ninyi wanasheria mnajua hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuji-*commit* kwa hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware *institution* kama hii haina kona.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware haina kona kabisa mtu kama hafai siku ya pili anatumbuliwa anaondoka. Mheshimiwa *Chief Whip*. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si kila nafasi mtu anayeteuliwa imeingizwa katika sheria, hapa ni kwa sababu tu huyu *Director General* anateuliwa kwa mujibu wa sheria mahususi ili waweze kuajirika katika taasisi hii.

Pili, kama nilivyoeleza awali katika utumishi wa umma na hawa wote watakaoteliwa humu ni watumishi wa umma iko sheria yake ya Tume ya Utumishi wa Umma ambayo ina-*govern* masuala mazima ya uteuzi, ndio maana nasema huwezi ukaingiza kila kitu katika kila sheria ukaweza kuongelea uteuzi ufanyike vipi, kwa hiyo, nikawa nampa *comfort* ndio maana nimesema *amongst the persons* lakini mwisho wa siku utasoma sheria zaidi ya moja katika kutekeleza suala hili. Kwa hiyo ni kumpa *comfort* na sio kwamba tunataka kubishana naye lakini tunataka tumpe tu *comfort* kwamba bwana kwamba hayo yamezingatiwa. Kuna Sheria ya Tume ya Utumishi wa Umma tunamuomba akubali mapendekezo ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware nakuomba kubali yaishe, usisikilize ushabiki wa kutoa hoja, wewe ni Daktari.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu basi nitoe hoja. Tumalize tu naomba mniunge mkono Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Mpina, tumpe Hawa Ghasia safari hii. Mheshimiwa Hawa, Mheshimiwa *AG* na Mheshimiwa Heche. Tunaanza na Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri dada yangu Sware alikuwa anajitahidi kuwa-*convince* watu ambao hawako tayari kuwa *convinced* ametumia lugha nzuri sana nikawa namsikitikia tu moyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachofanya na ni bahati mbaya mimi napenda tu haya mambo yabaki kwenye rekodi Rais tumempa mamlaka ya kuteua mpaka *Poster Master* kwenye nchi hii, hata kama *institution* hii ya Uraisi ni kubwa tunajua sio mtu. Lakini hizi *powers* zote Rais alizonazo mpaka kwenye *research* ya *fish* tunataka Rais ateue, ndugu zangu kweli, yaani samaki! Rais ateue kwenye samaki, ateue kwenye mbegu, ateue sijui kwenye miti, kwenye korosho! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, najua hapa tunazungumza na dunia itaona haya mambo baadae na watoto wetu, tunaomba kama hamtatuelewa, walau yawe basi yanapita. Wenzetu wa Kenya mmeona wanachofanya, majina yanaenda hata matatu, yanakuwa *vetted,* yanaletwa kwenye Bunge, baadaye anapelekewa anateua. Sasa mtu mmoja tu anaenda na jina lake huko amefurahishwa na mtu fulani, sasa hivi tumeona, mmeona Wakurugenzi hawa, mmeona Wakuu wa Wilaya ma-*DAS*… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche twende kwenye hoja iliopo mbele yako.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio hoja yenyewe hiyo ya uteuzi.

**MWENYEKITI:** Aahhaa! Kaa chini! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Hawa!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamaliza.

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha. Unazungumza ma-*DC* humu ndani saa hizi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Hawa. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipingane na hoja ya Mheshimiwa Dkt. Sware kwa sababu taratibu na Sheria za Utumishi wa Umma zimeweka wazi jinsi ya kuteuwakatika nafasi zile za uteuzi. Ni kwamba majina yanapelekwa zaidi ya matatu na yanafanyiwa *vetting* na yanapatikana matatu kumpelekea yule anayeteua. Na kwa vile Sheria ya Utumishi wa Umma inaainisha kwa kila nafasi na nani mamlaka za uteuzi, mimi sioni kama

kuna sababu au kuna konakona zinazosemwa. Sidhani kama kuna kona katika Sheria za Utumishi wa Umma, hakuna kona hata kidogo na nimuombe aondoe huo wasiwasi alionao.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Utangulizi wangu kama aliosema mdogo wangu, Mheshimiwa Heche kwamba Mheshimiwa Dkt. Sware anajaribu kutuweka sawa ili tukae sawa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *transparency* na *clearance* ndio msingi mkuu kwenye utawala bora. Vinginevyo tuambiwe uteuzi huu ukisomwa pamoja na sijui Sheria ya Utumishi wa Umma, *why? You have one document* ya ku-*guide,* kila kitu kiko pale. Sasa huyo Rais akikwambia nimeangalia hapa nimesema nifanye hivi, aah, Mheshimiwa Rais ulitakiwa uangalie na utumishi wa umma? Kwani kuna kosa gani tukiweka hiyo *transparency* na *clearance,* na *clear* ni yetu sote, muhimu tunalenga kwenye utawala bora. Mdogo wangu Mheshimiwa Angellah Kairuki, itazame hii ni jukumu lako; si kona, lakini *ambiguity.* Naomba kuwasilisha na namuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Sware, niseme ifikie wakati hata Rais tumpe kazi za msingi za kufanya. Kuna kazi za msingi ambazo Rais wa nchi anapaswa kuumiza kichwa kufanya, sasa na kwenye uteuzi, hizi teuzi ndogo ndogo. Kama juzi tu, Rais wa nchi kaongopewa anamteua Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya anafika unaambiwa sio mimi, ina maana anafika Ikulu anaambiwa sio wewe! Tunaanza kumuaibisha Rais kwa kuteua teua tu, vitu ambavyo viko ndani ya mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sifa za watumishi wa umma, achaguliwe *among three* ambao wana *qualifications,* mmoja kati ya huyo anaweza kujaza hiyo nafasi, sio kuteua teua tu kwa sababu ni Rais afanye kila kitu, tunamuaibisha na ndio tunachokifanya wakati huu.

Mimi ninaona Kanuni za Utumishi wa Umma zisimame, Rais afanye majukumu makubwa ya Kitaifa, lakini hii kazi ya kuteua teua kuna watu wana sifa wanaweza kujaza hizo nafasi kutegemea na vigezo vyao; naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MWENYEKITI:** Unajua hata *argument* yenyewe iliyokuwepo wala hakuna *argument* yoyote, ukitizama hiki kifungu kimetulia vizuri tu. Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo umemaliza kusema wewe mwenyewe, kwanza Waziri hapo wa Utumishi wa Umma ameongea vizuri sana kwamba ipo Sheria ya Utumishi wa Umma ambayo inaongelea jambo hili na imeliweka vizuri na ndio maana hata tukienda kwenye *accounts* hatuwezi tukazungumza *how the auditing will be audited* kwa sababu tunajua ipo sheria, *The Public Audit Act* ambayo inazungumza jambo hili. Na humu ndani kwenye sheria hii kuna sheria nyingi tu; kuna *The Public Procurement Act* na yenyewe utaanza kuzungumza kwamba *procurement* itafanyikaje. Kuna suala la *Public Audit Act* lipo humu, utazungumza na lenyewe litafanyikaje! Sheria zile zipo ambazo zinazungumza suala hili na sio Mwenyekiti. Nadhani kwamba, hatuna sababu ya kupoteza muda katika hoja hii kwa sababu sheria ambazo zina *guide* jambo hili zipo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ambalo naomba kushauri mbele ya Bunge hili, Bodi haiwezi ku-*recommend* kwa Rais. Anaye-*recommend* kwa Rais ni Waziri mwenye dhamana ya hiyo taasisi, hilo la kwanza. Lakini cha pili Waheshimiwa

Wabunge naomba sana Waziri Kairuki na Mawaziri wengine wamezungumza hapa na Wajumbe, wamefafanua vizuri, huwezi kuandika sheria kwa namna ambayo Mheshimiwa Riziki na Mheshimiwa Dkt. Sware mnapendekeza; muda mfupi uliopita hapa wewe ume-*move schedule of ammendments.* Ambayo ilikuwa ile, *Section 11* ile ambayo ile ya mwisho ile ilikuwa ni *clarity* tu kwamba, Waziri atapendekeza baada ya kupendekezwa na Bodi, mkasema sasa *we can not be so much contradictory,* hilo la kwanza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la Rais kuteua hawa watu ni la Kikatiba. Ibara ya 36 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema hivi…

**MWENYEKITI:** Jamani, sikilizeni vitu, tatizo lenu hamtaki kusikiliza hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ndogo ya (2) inasema hivi, Rais atakuwa na madaraka ya kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka ya viongozi wanaowajibika kuweka Sera na Idara za Serikali na Taasisi za Serikali na Watendaji Wakuu wanaowajibika kusimamia ile. Ibara ya 35 inasema shughuli zote za utendaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatekelezwa na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais. Kama hawa wote, sisi wote tunatekeleza majukumu yale kwa niaba ya Rais, kwa nini asituteue?Kwa hiyo, naomba kushauri sana, tuache mapendekezo ya Serikali, kama yalivyoletwa na Waziri mwenye dhamana ya muswada huu na ninawashauri Wahedshimiwa Wabunge tuunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Na kuweka rekodi sawasawa Tanzania ni mwanachama wa *African Peer Review Mechanism.* Suala la *transparency Tanzania number one.*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Iko kwenye *record*. Mheshimiwa Dkt. Sware funga hoja yako kama umekubali tunaendelea, hujakubali tuendelee na taratibu za Kibunge.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tupige tu kura isitoke hivi hivi.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Hoja ya Mhe. Dkt. Immaculate Sware ilitolewa na kukataliwa)*

**MHE. ESTER M. MMASI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Kaa chini Mheshimiwa Mmasi. Kifungu hiki kinaridhiwa pamoja na marekebisho ya Mheshimiwa Mmasi na Serikali?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 13 kina marekebisho ya Mheshimiwa Profesa Tibaijuka na Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pendekezo langu hapa linatokana na kutaka ku-*rationalise* na mfumo mzima wa hizi taasisi zetu za utafiti wa

kilimo wa *agricultural disciplines* na nimeona kwamba sasa hapa tunaweka Makamu katika taasisi ambayo kimsingi ni ndogo zaidi ya ile nyingine ambayo ni kubwa iliyopita asubuhi. Bahati mbaya imepita, naweza nikasema kwamba kwa haraka haraka, mwendo wa kasi! Hatukupata nafasi ya kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo pendekezo langu hapa ni kwamba huyu Makamu kama Waziri anampenda sana anaweza akamuweka kwenye kanuni zake, kama tulivyoelezwa, lakini sioni kwamba, aingie kisheria kwa hiyo, naomba kwamba, hii *clause* ifutwe, naomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutunga sheria nadhani hata Profesa anaufahamu vizuri kwamba ni mchakato unaoanzia mbali sana na kwa kweli kwa kiwango kikubwa mengi yaliyomo katika huu muswada ni mawazo ya wadau wenyewe walioko kwenye taasisi hizi. Na bahati mbaya, *it is actualy by default* kwamba tunazungumza hii miswada miwili leo kwa namna hii kwa sababu ya mabadiliko yaliyotokea katika muundo wa Serikali, vinginevyo haya mambo yangekuja *separately* kabisa kwa sababu muswada huu ulianza maandalizi wakati wa Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau walioshiriki katika kuandaa muswada huu wao waliona umuhimu kwa sababu, ilikuwapo *TAFIRI* ambayo haikuwa na *Deputy Director General,* lakini baada ya wao kutafakari utendaji kazi wao ulivyokuwa wakaja na wazo kwamba hapana, kuna *Directors* na kadhalika, lakini tuanzishe *position* ya *Deputy Director General* ili ikidhi mahitaji yao kama taasisi. Kwa hiyo, sasa sio mapenzi ya Waziri, lakini nadhani ni mapenzi ya wadau wenyewe walioko kwenye taasisi hii ndio walioona kwamba kuna haja ya kuwa na *Deputy Director General* na kwa hiyo, naomba sana tu Profesa Tibaijuka atukubalie tuliache hili kwa sababu ni pendekezo la wadau wenyewe.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia sana maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, lakini naamini kwamba wadau mbalimbali wameleta mawazo yao na sisi kazi yetu tuna-*rationalise* kusudi mambo yawe yanaonekana. Sasa *Tanzania Agricultural Research Organisation* haina Makamu kwa sababu, wadau hawakusema hivyo. Bado nafikiria kwamba siko peke yangu katika hili kwa sababu nimeona pia na Kamati na wengine walizungumza, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ndio maana nimesema kwamba kama wadau wanaweza pia wakawa *accommodated* kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sisi wadau ambao tumekosa nafasi asubuhi, tunakuja kwako kwenye kanuni utuangalie maana *issues* tulikuwanazo hapo. Sio kwamba, zimeyeyuka tusije tukalazimika kuja na hoja binafsi humu katika Bunge linalokuja. Kwa hiyo, nafikiri kwamba bado kuna nafasi ya *accommodation* kwamba lakini tu-*rationalise, there is a need for rationalization,* kwa hiyo, hiyo ndio hoja yangu, kama Mheshimiwa Waziri naomba uipokee sina zaidi, lakini kama haitapokelewa nitaomba ijadiliwe, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inafanana na mimi nichangie hapo hapo.

**MWENYEKITI:** Subiri nikuite basi. Haya Mheshimiwa Mbogo. *(Kicheko)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hoja yangu na mama yangu Mheshimiwa Profesa Tibaijuka tunafanana, wote tunapendekeza hii *clause* ya 13 ifutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunapandekeza kwamba ifutwe; ni kwamba hii taasisi itakuwa na *Directors,* itakuwa na *Head of Departments* na *Head of Sections.* Sasa huyu *Deputy Director* ambaye atakuwa anamsaidia maana yake atamsaidia *Director* kwa majukumu pale wakati hayupo, labda kasafiri au yupo likizo, kwa hiyo, hatuoni haja ya kuwepo na wakati huohuo taasisi kwa kifungu cha 14(3) kitaajiri *professionals and non professionals* ambao watafanya hizi kazi. Kwa hiyo, kama *Director* hatakuwepo, huyu *Director General,* hawa *Directors* wata-*act on his or her behalf* kwa hiyo, hatuna haja ya kuwa na *Deputy* katika hii taasisi. Kwanza pia tunaangalia *geographical coverage, number of staff* na *activities* zenyewe kwa hiyo, kwa *research institute* hatuna haja ya kuwa na *Deputy Director.*

**MWENYEKITI:** Aah, Serikali, lakini hata hivyo nafikiri ukitizama mifano ya taasisi nyingine hawa ma-*deputy* hawa wanakuwa na fitina sana hawa. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka ilikuwa kwamba sio kwamba hii nafasi iondolewe, ilikuwa ni kwamba tuipeleke kwenye kanuni. Sasa imekuja nyingine kwamba tuiondoe moja kwa moja. Kama alivyosema Waziri…

**MWENYEKITI:** Aahhaa! Mheshimiwa Profesa Tibaijuka amesema *clause 13, by deleting the entire clause.*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio, lakini wakati anatoa maelezo ndio sasa amezungumzia haya.

**MWENYEKITI:** Jibu, jibu endelea.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inayotolewa ni kwamba hii taasisi ni ndogo. Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba kati ya eneo ambalo tunahitaji kwa kweli kufanya maendeleo na mabadiliko kama nchi, ni suala la uvuvi. Hata kama inaonekana kwamba kuna taasisi chache au ambazo hawa watu watakuwa wanaongoza, lakini kitu ambacho kinatakiwa waongoze ni kitu kizito sana ambacho kinahitaji msukumo mkubwa na ndio maana tunahitaji timu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba turidhie tu mapendekezo ya Serikali kwa sababu, tukipeleka kwenye *schedule* maana yake ni rahisi Waziri kwa utashi wake akamuondoa, lakini tunapoweka kwenye sheria maana yake kama ukitaka kubadilisha inabidi uje Bungeni. Kwa hiyo, kwa sababu wadau ambao wamekuwa wakijadiliana kwa miaka saba sasa wameona hii nafasi kwamba, ni muhimu naomba Waheshimiwa Wabunge turidhie mapendekezo ambayo yanaletwa kwenye muswada.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja kwamba, ijadiliwe kwa sababu hizi ni *research institutions.* Ni vyombo vya utafiti na kama ulivyosema wewe mwenyewe ni mahali ambapo kwa mfano Chuo Kikuu, Chuo Kikuu hakuna mtu anayeruhusiwa kuongoza kitengo zaidi ya miaka sita, ukitoka hapo una-*rotate* unakwenda kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiria kwamba hoja yangu hapa Mheshimiwa Waziri anielewe; niliposema kwamba na kama ulivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni *entire deletion,* lakini nimesema kwa sababu kufuta hapa hakuondoi mamlaka ya Waziri kuweka kwenye kanuni kama akiona kwa kweli hiki kitu ni muhimu, lakini *at least* kwa sababu, bado ana *powers* za kufanya *ammendments* kama hizo kwenye *regulations* zake. Kwa hiyo, nafikiria kwamba kusudi uwe na *atmosphere* ambayo ina afya katika taasisi za watafiti, ni vizuri usilete vitabaka tabaka sana kwa sababu pale tunafanya kazi, ndio *nature* ya wasomi, yaani *scientist* hawana vitabaka sana, huyu sijui ni Naibu nini, hakuna vitu kama hivyo, kila mtu anakwenda na kichwa pale mnafanya *research. (Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri kwamba alivyosema Mheshimiwa Mbogo *argument* yetu ni moja kwamba watu wanaweza waka-*rotate,* Mkurugenzi anaendesha anaweza akamuomba *Director* yeyote wakati fulani akawa pale kama hayupo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo, ili *Hansard* iwe sawasawa na wewe nipate kauli yako.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye menejimenti mambo ya *planning, staffing, organizing* na kwamba hapo tunasema tunamchagua mtu mwenye *experience* ya miaka kumi, bado hoja yangu palepale kwamba *this clause should be deleted* na *renumbering done accordingly.* Kwa sababu ufanisi na tuna taasisi kubwa zina *DG,* hazina ma-*deputy,* zinafanya kazi vizuri na mwelekeo wa *vetting* ni Serikali tu ikafanye *vetting* nzuri, ichague mtu ambaye kwamba ni mchapakazi na tuachane na ule mfumo wa kizamani. Kwa hiyo, Serikali ikubali tu kama itaona baadaye inafaa itakuja ilete mbele huko, lakini kwa sasa tunaona bado haifai kutokana na ukubwa wa *institute* kwa hiyo, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa mahitaji wa Wabunge ni sawa, kwa hiyo wametoa hoja wote kwa pamoja, kwa hiyo tutakuwa nauchangiaji wa pamoja na tutahoji kwa pamoja. Mheshimiwa Nyongo...

**MHE. STANSALAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante....

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Riziki. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani lisituharibie sana, namadhali *lee way* ameshai-*propose* Mama Tibaijuka kwamba *should need arise* tunaweza kuliweka kwenye kanuni basi tuondokane na hili jambo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbogo na wewe. Nataka *Hansard* irekodi.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Naunga mkono hoja ya mama.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa hapa ninapendekeza kwamba kati ya maneno "*person*" na "*who*", tunasema "*who is not a fisherman or a land based fish pond farmer.*" Naona nijieleze kidogo kwa sababu katika Miswada yote hii, huu mmoja ambao tumeufanyia kazi umeona kwamba Mheshimiwa Waziri kwa busara zake amekubali kwamba tubadilishe maneno. Kitu kimoja ambacho nimeona kina tatizo ni kwamba utafiti hasa huu katika *agricultural sciences* unajikita kwenye kitu tunakiita "*on farm research.*" Mtafiti wa kwanza katika fani hizi ni mkulima mwenyewe, ni mvuvi mwenyewe. Kwa hiyo, ukisema kwamba mtu yeyote anaetaka kufanya utafiti aende kujiandikisha kwenye chombo, utaua dhana nzima ya *research.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *on farm research,* hawa wavuvi, sasa mimi kidogo ile ya kuingia kwenye maji, kwa mfano, *aquatic culture,* zile naona zinaweza zikaingia kwenye mambo ya mazingira, unaweza ukasema ziwe na *control.* Mtu ambaye anafuga samaki wake pale, ana uhuru wa kufanya *research* na ni lazima afanye *research*. Wale sasa ndio wanawaita hawa watalaam kuja kuangalia. Uvumbuzi mkubwa duniani umetoka kwenye *garage*, umetoka kwenye mashamba, umetoka kwa watu ambao wana-*deal* na vitu hivi *on a day to day basis.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii kama nilivyomwomba Mheshimiwa Waziri, hata kwenye kanuni zake ni lazima kuangalia kwamba tunakwenda na sayansi yenyewe; maana yake tunatunga sheria ya sayansi hapa. Sasa nimeona kama kipengele hicho labda *AG* kama namwelewa vibaya, lakini mnaweza mkafafanua, inaonekana kwamba mtu amefungwa, hana *freedom* ya kufanya *research.* Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Tibaijuka ina mantiki, lakini moja kati ya malengo ya kuleta muswada huu mbele ya Bunge ni kwa sababu tunahitaji kuondoa *duplication* ya tafiti. Kwa hiyo, tunahitaji kuwa na *database* ya watu wanaojihusisha na utafiti. Kwa sababu hali ilivyo sasa ni kwamba kuna watu wengi na taasisi nyingi zinafanya utafiti kwenye mambo ya uvuvi lakini hatufahamu. Kwa hiyo, mara nyingine tunatumia rasilimali nyingi kurudia kitu kile kile, ukitaka kutafuta na kujua kama kuna utafiti umefanyika kwenye eneo fulani huwezi kupata. Kwa hiyo, tukiruhusu tu kwamba kuna baadhi ya watu ambao hawatahitajika kujisajili, tunapoteza hilo lengo la kuwa na *database* lakini vilevile kuondoa hiyo *duplicity.*

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa hiyo, tunaomba tuendelee, kwa sababu hakuna madhara; kama tayari wewe kawaida ni mvuvi tu, kujisajili wakati unafanya utafiti, itatusaidia sisi tujue ni aina gani ya utafiti ambao umeufanya ili tuweze kuutumia na ipatikane. Ili hiyo habari iweze kupatikana na tuweze kutumia na tuwape wale ambao wanahitaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mweyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri. Tatizo langu ni kwamba, bila *amendment* yangu hii kuingia, huyu mtu anayefanya *on farm research*, *fisherman* ambaye anaangalia *environment* yake ana i-*study* anaona vitu vina-*emerge and that is essence of science;* sasa tunakuja kwenye kipengele cha 17(3), tutamfunga huyu mtu. Nimeiweka pale kusudi tuweze kuokoa kifungu cha (3) kwa sababu kinasema: *"any person who contravenes the provisions of subsection (1) commits an offence and shall on conviction be liable to a fine not less than two million shillings but not exceeding five million shillings."*

Mheshimiwa Mweyekiti na Waheshimiwa Wabunge, hizi ni *serious matters.* Hii inakwenda kuua *research* kabisa, maana yake hizi taasisi ni za kitaalam jamani. Kwa hiyo, niliyaweka yale maneno kuonesha kwamba *offence* ni kwa wale ambao kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, wanaoweza kufanya vitu hivi kwa *grand scale*. Kwa mfano, muswada wa *crops* tungewahi tungeweza pia kuona ni haya haya, lakini sasa tutakwenda na Mheshimiwa Waziri kwenye kanuni.

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa hiyo, nimeleta hayo maneno kwa sababu ya hatari inayo-*lie* kwenye kifungu cha 17(3). Kwa hiyo, naomba Bunge hili Tukufu liangalie kifungu cha 17(3), mvuvi anakwenda kufungwa kwa sababu hakujiandikisha kwamba anafanya utafiti wa ki-*pond* chake; *that is what it is saying.*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, naamini kwamba utani-*accommodate,* yaani ni kwa sababu naona ninachokisema, vitu hivi ni kazi nzuri, lakini ni *oversight*. La sivyo, natoa hoja ijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hizi sheria nazo ziwe *friendly* vilevile. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ya kuleta huu muswada hapa ni matatizo ya hivi hivi ya watu kufanya chochote wanachotaka huko *in the name of research,* halafu wanachokifanya hakijulikani kwa mtu mwingine yeyote. Sasa hii sheria inachokitengeneza hapa, haimzuii huyo mvuvi peke yake kule kufanya *research* kwenye *pond* yake au kwenye eneo la ziwa aliko; tunachokihitaji hapa ni kwamba awashirikishe na wengine kwa kutoa taarifa kwamba mimi ninafanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusifike mahali ndugu zangu tukasema na kwa kweli kwa namna hii *to the contrary,* ndiyo itakuwa aina-*strengthen* hizi *institution* kwa maana ya kwamba kila kinachoendelea *in this aspect* kitakuwa kinafahamika sasa *centrally* na tunaweka kumbukumbu za nini kinachofanyika. *Otherwise,* mwanakijiji kwangu kule Kome Kisiwani ataendelea kufanya anachokitaka na hatakabiliwa na *liability* yoyote ya kisheria kwa sababu atasema nafanya *research* kwenye ka-*pond* kangu haka hapa, kumbe ana haribu mazingira, anafanya kitu kingine cha hivi na hivi. Kwa hiyo, ndiyo lazima hawa watu wafahamike. Namna ya kuwafahamu ni kuwafanya waje wasajiliwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka, funga hoja yako, Mheshimiwa Waziri amejieleza vizuri tu.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Waziri, tena amezungumza vizuri, anasema mkulima wake kule Sengerema; yeye mkulima wake kule Sengerema anatafika kwenye ofisi za *TAFIRI* lini? Hiyo gharama ya kuwatafuta wako wapi.

Ninachokisema, sipingi wazi wazi kwamba *documentation* na *registration* ni safi, lakini kuna *question* ya *scale* pia. Kwa sababu utafiti unaweza ukaanza na kitu kidogo. Ni *observation* ndogo unaiona, sasa wakati upo kwenye hiyo *process,* anakuja mtu anasema wewe unafanya *research* hapa, hujaenda *TAFIRI;* sasa kifungu cha (3) kinakwenda kufunga, unaliopa shilingi milioni mbili, mkulima wa Sengerema wa Muleba Kusini kwangu, wa Burigi ambapo hakuna barabara inayofika kule mpaka leo anakuta kwamba ameshavunja sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema, hii *provision* yangu haibadilishi kitu chochote, lakini inatoa *freedom* kusudi hawa watu *on farm researchers* wawe *protected;* kwa sababu bila *on farm research there is no research, I can state that categorically.* Kwamba kama tunakwenda kubana *on farm research, then* hapa tunafanya kosa kubwa sana na Mheshimiwa Waziri wewe ndio *custodian* wa hii sekta. Hiki kitu ninachokisema ni *reasonable*. Kwa hiyo, naomba kutoa kutoa hoja kwamba jamani, hoja yangu ipo pale pale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa. Mheshimiwa Dkt. Nagu, Mheshimiwa Nyongo, Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Dkt. Sware, Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Profesa Sigalla na Mheshimiwa *AG.* Haya, tutatazama na muda, siyo lazima wote mtapata nafasi.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kuungana na upande wa Serikali kwamba tunategemea huyu mtu ni *researcher* na *research* yoyote na *especially* hizi ambazo ni *scientific* kwanza huwa inaombwa mtu atafute *ethical clearance* ili aweze kufanya *research.* Mtu anayetafuta *ethical clearance* ni kwamba anaonesha kwamba huyu mtu pengine ana uwezo wa kufanya hiyo *research* kwa sababu *research* yenyewe inatakiwa iwe *valid* ili itumike kwa matumizi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda kufanya *research* tunategemea kwamba ile *significance* ya ile *research* tuitumie na sisi. Sasa kama tutaweza kumfungulia tu huyu mmiliki wa *pond* ya *fish* anayefuga, ambaye katika *research* mimi naweza nikamchukulia kama ni *correspondents* kwamba huyu akutane na *researcher* ajibu aidha ni maswali halafu baada ya *research* kupata matokeo, yule ndio apewe maelekezo ya kutumia *information* ambayo inatokana na *research* ile. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kuungana na Serikali. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Nagu.

**MHE. DKT. MARY H. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niseme kwamba mimi nipo kwenye hii Kamati ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na hoja ya Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, lakini nakubaliana naye kwamba ni kweli uvumbuzi wa kwanza umetokana na *field,* iwe ni kwenye shamba, iwe ni kwenye zizi, iwe ni kwenye *garage;* lakini ninavyoona *clause* hii ndiyo itawasaidia wakulima, wafugaji, wanaofuga samaki na *aquaculture* nyingine. Kwa sababu wajanja ndio wanaodhibitiwa na *clause* hii kwa sababu mkulima anaweza kuwa ndio mvumbuzi, mjanja akachukua alichovumbua akapeleka kule kwenye *TAFIRI.* Kwa hiyo, wavuvi na wote wanaohusika wakijua kwamba *research findings* zao pamoja na *research yao* zitakwenda kuwa *registered,* itasaidia wale wengine ambao sio wajanja na kuwanyima fursa wale wajanja kuweza kuchukua kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Profesa Tibaijuka aone kwamba *clause* hii kutokana na *research* yao itawasaida wale ambao sio wajanja na itawanyima

wajanja fursa ya kuchukua *findings* na kazi za wengine. Nashukuru, nami naunga mkono upande wa Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namuunga mkono Profesa Tibaijuka kwamba unaangalia *scale* ya *research* inayoenda kufanywa, *COSTECH* wanatoa *clearance*. Inategemea na *research* gani unayoenda kuifanya. Sasa hapo tunakuwa tunambana yule mnyonge anapofanya utafiti mdogo ambao unamnufaisha yeye; kwa nini agharamie kuitafuta *TAFIRI* iko wapi ili atoe taarifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kunakuwa na *extension officers*, kama kuna kitu kizuri kimejulikana, basi kuna *line of communication* iwatafutie *TAFIRI*. Kwa hiyo, *TAFIRI* watafute *other means* ya kupata *information* na wawe na *information centre* badala ya kumkandamiza yule anayefanya *research* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuna *chance* kwamba unaweza kuwa na *proposal* nzuri ya *research*, ukaipeleka *TAFIRI* ile *proposal* yako wakaifanya ni yao au wakaiba ile *title*. Kwa sababu hata huku kwenye sheria wanasema *any discoveries* unazofanya, *patent* inabaki *TAFIRI*. Kwa hiyo, kuna vitu ambavyo viko *controversial* humu ndani na hiki kifungu kitakuwa kinambana yule *researcher* mdogo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sigalla.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwa masikitiko makubwa, naunga mkono msimamo wa dada yangu Profesa Tibaijuka; kwa jinsi kama kifungu hiki kilivyokaa, kabisa kabisa wanazuoni tulioko kwenye Bunge hili tutakuwa tumedharaulika. Huwezi hata kidogo kwenye nchi ya watu milioni 46 unawa-*peg* kwamba waombe kibali. Halafu ile *section (3)* inatoa *penalty* kwamba ukifanya utafiti bila idhini ni kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, makosa mengine ya kuharibu mazingira yako *covered* na sheria nyingine. Kwa hiyo, mtu ukiharibu utashitakiwa kwa sheria nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *institutions* zinazofanya tafiti ziko nyingi, unaviambiaje vyuo? Unawaambiaje *funders* mbalimbali ambao kama kukiwa na ukiritimba kwa mfano…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Umeeleweka vizuri. Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi namuunga mkono Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka. Natamani tuone kama tukipitisha kifungu jinsi kilivyo ni kwa jinsi gani tuta-*discourage* ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga na Mheshimiwa Dkt. Sware, ni lazima tuangalie *of which scale*, kwa sababu kuna *research* zinafanyika katika *level* ndogo na inatumia *fund* ndogo kwa watu kutaka kugundua kitu. *Unless publication* ya majibu imefanyika ndiyo aende sasa kutoa taarifa kwamba nimefanya moja, mbili, tatu kwa sababu ya matokeo yaliyokwishafanyika lakini katika *level* ya kwanza turuhusu watu wafanye ubunifu.

**MWENYEKITI:** Ahasante. Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Serikali kwa mantiki moja tu kwamba suala la zile *scale* ndogo ndogo za utafiti, Mheshimiwa Waziri atazizingatia kwenye Kanuni namna ya kuwafikia hao wanyonge, lakini hawa wenzangu ambao wanazungumza, wanatakiwa wajibu hoja ya uvuvi haramu unaoendelea sasa hivi. Ukienda sayansi ya bahari, wanalalamika kwa hali ya juu sana juu ya uvuvi haramu unaoendeshwa huko baharini pamoja na kwenye maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ubunifu, *COSTECH* mpaka sasa hivi wana-*accommodate* mpaka watafiti wadogo wadogo, wanapeleka kwenye *incubators* za kwao. Kwa hiyo, hoja inayozungumzwa hapa kwamba hii itaua utafiti, siyo kweli. Inabiti tuikatae hii tusije tukaruhusu huu uwazi wa watafiti kuja. Ukienda sayansi ya bahari peke yake, watu wanaokuja kutoka nje kufanya utafiti ni zaidi ya 30. Wanaotoka kanda yetu hii kwa maana ya wanaokuja kufanya utafiti ni zaidi ya 50… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa umeeleweka. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Muungano na Mazingira.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tukienda kwenye tafsiri, nini maana ya *research?* Ukisoma tafsiri hapa ya sheria, inasema *research means, any systematic study conducted in order to develop, verify and disserminate appropriate technologies for the benefit of stakeholders and fishery industry.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kuangalia maana ya *researcher, is a person trained to design and implement research protocols, collect, analyze and interpret data relating to fishery,…*" na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huyu mtu anayekuwa *described* humu kama mtafiti na shughuli hii inayokuwa *described* humu kama *research, requirement* ya ku-*report* haiwezi kumshinda mtu ambaye tunam-*define* humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kweli *sentiment* zinaeleweka, lakini tunakuwa *academic* zaidi ya kuwa *practical* kwenye suala hili. Nchi yetu hii hata kwenye kufanya utafiti wowote ule hata wa kuwauliza watu masuala, ni lazima upate kibali *anyway* kutoka *COSTECH* cha kufanya *research*. Kwa hiyo, hakuwekwi *requirement* mpya hapa ambayo itazuia shughuli hii kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani tuunge mkono kifungu hiki kama kilivyo kwa sababu hakiwezi kuzuia maendeleo ya utafiti kufanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze tu; moja, siyo kila mkulima au mvuvi au mfugaji ataenda kusajiliwa. Ni yule ambaye amekusudiwa kama *researcher* na chini ya sheria hii. Mheshimiwa Naibu Waziri amefafanua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tusipowataka kwenda kusajiliwa tu, tuta-*create* mwanya mkubwa, hatutaweza kumdhibiti mtu yeyote. Kwa hiyo, nilikuwa nawashauri Waheshimiwa Wabunge waione hii athari ya kutomtaka huyu mtu kwenda kusajiliwa tu. Kwa hiyo, watashindwa ku-*regulate* hii kwa sababu mtu yeyote atakuwa anajifichia mle anasema; kwa mfano mimi ni mfugaji na ni mkulima, lakini siwezi kufanya *research* hii. Nami nitajifanya nafanya mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushauri Waheshimiwa Wabunge tukubali hii hoja ya Serikali kama ilivyofafanuliwa na Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuika, funga hoja yako.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza naomba niwashukuru wale waliochangia, walioweza kuona wasiwasi wangu na ninaomba niseme kwamba hoja nimezisikia kwa upande wa Serikali, na mimi pendekezo langu lilikuwa ni kutoa huo wasiwasi wa watu kwenda kuhangaishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake hapa tunaporuhusu hiki kitu ni lazima tujue *what we are doing, I want to be on record* kwamba tunakwenda kabisa kufunga ubunifu kwa sababu Mheshimiwa Makamba amejaribu kuelezea hapa; inasema *any person,* haijasema *any researcher.* Hii sheria inasema "*any person,*" haijasema "*any researcher who engages.*" *Any person* ndio huyo mkulima, mwanamke ambaye anafanya ubunifu pale shambani kwake, Bunge hili linakaa hapa leo linakwenda kusema kwamba kwa kuwa hajajiandikisha *TAFIRI* anakwenda kulipa shilingi milioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *I want to be on record* kwamba kwa kweli jambo hili tumelijadili, lakini naomba pia niwasihi wenzangu kwamba hoja yangu ni kuweka tu maneno matatu ya kuwalinda hawa watu; tulinde ubunifu. Hii kwenda kama tulivyoandika ni kuonesha kutoelewa sayansi maana yake ni nini. Hicho ndicho tunachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba mniunge mkono jamani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, unataka tulihoji Bunge, siyo?

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Nataka lihojiwe maana yake lazima *record* iwepo kwamba tulisema na Bunge liliamua, maana yake mwisho wa siku Bunge…

**MWENYEKITI:** Nimeshakuelewa, nakushukuru.

*(Hoja ya Mhe. Prof. Anna Tibaijuka ilikataliwa na Bunge)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umechakachua matokeo, naomba tuhesabu kura, siyo kweli!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Hapana, hapana, umechakachua matokeo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, hebu kaa!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Haiwezekani hilo jambo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, hebu kaa. Utaratibu wa kuhesabu kura umeshachelewa.

Waheshimiwa Wabunge, kiti kimeshafanya maamuzi!

Ibara ya 18

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Hansard* ndiyo itaamua mambo yalivyokwenda lakini…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, tuko kifungu cha 18 na Bunge likishafanya maamuzi yamepita.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo na mimi nasema kwamba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, nenda kwenye kifungu cha 18.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye kifungu cha 18.

**MWENYEKITI:** Haya, twende.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba kumlinda mtafiti anayejaribu kubuni mambo. Sasa hapa anaweza akawa mtafiti mdogo ambaye sasa hivi nimejaribu kumtetea lakini nimeshindwa na kuna mtafiti mkubwa wa *COSTECH.* Hizi taasisi kama zinaitisha taarifa ni lazima tulinde haki zake. Kwa hiyo, nataka ku-*insert* maneno *with due regard for protection of intellectual property rights;* kwa sababu huyu mtu anayefanya *research* maana yake hizi ni taasisi za kitafiti; au siyo. Sasa mimi nafanya *research* yangu na wenyewe wanasema wewe leta habari yoyote unayofanya. Kwa hiyo, *intellectual property rights* zangu nitazi-*protect* namna gani?

Kwa hiyo, hapa naomba nisisitize, tunatunga sheria lakini tunaweza kuja kuonekana uelewa wetu wa sayansi labda kidogo kuna walakini, kwa sababu nasema *intellectual property rights,* hapa kwamba tulimnde mtafiti ambaye anaweza akashindwa kutoa taarifa kwa sababu yuko kwenye *stage* ya kulinda *intellectual property rights* zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kuna sheria nyingi ambazo zinalinda haki za wagunduzi kama vile Sheria ya *Copyrights and Neighbouring Rights Act,* kama Sheria ya *Intellectual Property Rights* na *patent rights,* hata *Cybercrimes Act;* kwa kweli sisi kama Serikali tunakubaliana na anachopendekeza Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwa sababu moja kati ya sababu zinazotufanya tulete Muswada huu ni kwa ajili ya kulinda haki za wagunduzi. Kwa hiyo, ni *oversight,* imesahaulika, tunakubaliana na pendekezo lake. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 19

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwenye *clause 20* hapo nilikuwa na *concern* moja kwamba *to insert that, incase we have independent researcher…*

**MWENYEKITI:** *No, no,* Mheshimiwa Mmasi, ni 19 si 20.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Ahsante sana, na mimi naona nilijichanganya hapa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *concern* yangu ilikuwa kwamba itakapotokea tunakuwa na mtafiti *whether* ni wa ndani au wa nje, cha kwanza lazima mtafiti huyo aweze ku-*seek permission from the concerned authority.* Tunapoongelea *local research* basi a-*seek permission* kutoka kwenye *Institute of Fisheries and Research* na tunapoongelea *external researcher* basi huyu mtu a-*seek permission from COSTECH.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu nafikiria kwamba ni vyema tuka-*admit* kwamba hapa tulipofika tumeshaumizwa sana kwenye masuala mazima ya uhifadhi wa maliasili ya Tanzania; na kufanya hivi ni njia moja wapo ya kuweka *controls.* Pia tukisema kwamba mtu huyu a-*seek permission* tutamwondolea adha mtu huyu ambaye leo hii ni mtafiti wa ndani ambaye anagharamiwa na Serikali, kachukua pesa ya Serikali, kasafiri nje ya nchi kwenda kufanya *literature review,* amechukua pesa nyingi, anarudi hapa anakwenda ku-*submit COSTECH* anaambiwa kwamba *research* haiko *valid,* haifanyiki.

Kwa hiyo, nafikiria cha kwanza tuombe *permission* na badala ya mtu ku-*submit research proposal,* basi a-*submit synopsis,* inatosha hiyo kuweza ku-*validate* kwamba hii *research* inafanyika au haifanyiki. Kwa hiyo, kwa namna moja, kwanza tuta-*protect* maliasili yetu ya baharini lakini pili tutaondoa adha ya usumbufu kwa maana ya muda na *resources* ambazo *researcher* huyu ame-*incur* kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nina *concern* moja hapo kwenye *section (3),* kwamba *foreign researcher* ambaye amekuja kufanya tafiti, basi siyo tu alazimike ku-*submit final research report,* lakini basi hata…

**MWENYEKITI:** Maliza, maliza upesi!

**MHE. ESTER M. MMASI:** …basi hata *progressive report* nayo a-*submit* kwa maana ya kuweka *controls* kwenye maliasili ya baharini. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Serikali inakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Mmasi kwa sababu hata tulichokuwa tukijadili katika kifungu kilichopita hivi karibuni tulikuwa tunataka hili hili na hapa limesahaulika kwamba watu wafahamike na wapate ruhusa kabla ya kuanza kufanya haya mambo. Nakubaliana naye. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware. Mheshimiwa *Chief Whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini ni marekebisho tu kidogo kwenye lugha. Ukiangalia kwa namna Mheshimiwa Mmasi anavyokipendekeza, ukiangalia kile cha 19, baada ya *"shall"* ukiingiza maneno anayopendekeza "*first seek permission from*" badala ya "*to the concerned authority,*" halafu "*and thereafter develop a proposal blah blah blah,*" kulikuwa kuna maneno kidogo yana-*miss.* Kwa hiyo, kwenye 19(1) na baadaye kwenye 20(1).

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, wewe ume-*refine* tu *wording.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeboresha kidogo.

**MWENYEKITI:** Haya, haina shida. Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina mapendekezo tofauti kidogo kwa hiyo *clause 19(1),* sisomi vizuri hiyo sheria inasema kwamba; mtu yeyote anayetaka kufanya utafiti wa uvuvi na kadhalika anatakiwa aandike *proposal* iende *TAFIRI for approval.* Mimi sikubaliani na hiyo *concept,* ninataka iwe kwamba mtu anapoandika *proposal TAFIRI* basi ni kama yule mtu anahitaji *funds for research from TAFIRI.* Kwa hiyo, nina-*propose* kwamba itoke neno "*conduct research*" iseme kwamba *a person or institution who intends to request for research funds from TAFIRI* ndio a-*submit* hiyo *proposal. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kifungu cha 19 (d) kwa mantiki hiyo, basi kisome kwamba kuwe kuna *detailed cost of research and amount* ambayo inakuwa *requested* hapo *TAFIRI.* Ukianglia kifungu cha 19(5) inabidi isome kwamba *"a person or institution who intends to conduct research on the fisheries or aquaculture shall inform the institute." (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Sware, lakini ifahamike tu kwamba lengo la hii sheria kwa ujumla ni ku-*regulate research*. Kwa hiyo, *regulatory function* hii na katika *context* ya hiki kifungu cha 19 haiwezi ikabakizwa kwa wanaoomba pesa peke yao. Kwa sababu hapa anachopendekeza ni kwamba wengine wote kama hawaombi pesa huko *TAFIRI,* basi waendelee tu na haya yote yaliyotajwa bila kuwa-*checked.*

Mheshimiwa Menyekiti, kumbe lengo zima la Muswada kwa ujumla ukiliweka ni kwamba tunataka kuwafahamu *whether* anatumia fedha yake binafsi au anatumia fedha ya Umma lakini afahamike; na afahamike tu siyo kwa jina; na hicho anachotaka kukifanya. Kwa nini ili

tumjue yuko wapi, anataka kufanya nini na kama hilo jambo limekwishafanyika, basi aambiwe hii *area of research* unayotaka kuifanya ilikwishafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamepata tuzo za kitaaluma kwa sababu ya kudandia kazi za watu wengine. *This is one area* itakayozuia hayo mambo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri hajaipata hoja yangu, kwa sababu hata hicho kifungu cha sheria kinasema hapo; *"for approval." I am not seeking approval from TAFIRI,* sawa. Kama mnataka kupata *information* nini kinaendelea kwenye *fisheries research in the country,* mtafute *other mechanisms* ya kuwa ninyi ndio *center* ya ku-*collect information* kwenye *issues* za *fisheries.* Sasa hapo mnakuwa mnabana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinafanya *research,* kuna Kitengo cha *Fisheries* kinafanya *research,* kuna *Institute of Marine Scienes,* kuna *University of Sokoine,* kuna watu binafsi wanafanya *research.* Mimi siwezi nikaandika *proposal* yangu niipeleke *TAFIRI* eti ndiyo iseme fanya au usifanye, hiyo siyo sawa, *unless* kama ninakuja kuomba *proposal* yangu mui-*approve* ni kama ninyi mnani-*fund* mimi niweze kufanya hiyo *research.* Anayetoa *approval,* inategemea na *scale* ya *research* kama ni mtu kutoka *foreign countries* anapata *approval or clearance* kutoka *COSTECH,* ninyi ni *institution* ambayo mnasimamia *research;* lakini siyo mnasema fanya au usifanye, hiyo siyo sawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumesema kwamba Serikali ilikwishawasilisha *amendment* ya hili jambo, angeisoma na yenyewe angeweza kuelewa. Tumekwishasema *"without prejudice to any other existing laws,"* na kwa maana hiyo sheria zinazoanzisha vyuo hivyo vyote, vyuo vikuu na kadhalika, labda nikusomee, *amendment* iliyokuwa *moved* na Serikali, Mheshimiwa Dkt. Sware sijui kama unayo hii *amendment* ya Serikali kwenye hiki kipengele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware, unayo?

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niisome tu ili muisikie.

**MWENYEKITI:** Isome!

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba *in clause 19 by deleting the contents of sub-clause (1) and substituting for them the following,* kwamba *19(1) without prejudice to powers vested to a university or a research institute established under the Universities' Act or any other written law, to conduct fisheries research or related matters, a person who intends to conduct research on fisheries and aquaculture shall develop a proposal in an identified priority reseach area and furnish the proposal to the institute for approval."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ni kwamba hicho anachokiogopa yeye sasa kiko *taken care of;* na kwa sababu mtu anayetaka kufanya *research,* yeye aendelee kwa hela

zake, kwa hela za kupewa kwa hela za namna gani; lakini sheria kwanza inampa hiyo nafasi haimzuii lakini afanye kueleweka kwa mamlaka hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi sio mtaalam wa sheria, lakini hii sentensi au hili neno hapa *"for approval"* ina maana kwamba ni ndiyo au siyo. Sasa leo hii Sware Semesi nikiandika *proposal* nika-*seek for funds,* nikapata *funds* na nika-*clear* labda nimefanya *EIA whatever it is,* kila kitu kime-*clear, then* bado niende *TAFIRI,* nipeleke *proposal* yangu *for approval* ili ifanye kazi; hiyo si sawa. Hii for *approval* siyo sawa hata kwa lugha ya *layman. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo jipya anaanzisha Mheshimiwa Dkt. Sware, kwa sababu *amendment* aliyo-*move,* nakuomba tu uwe *consistent* jamani, *amendment* uliyo-*move* wewe ni kusema mtu anayeomba pesa.

**MBUNGE FULANI:** Hujamwelewa.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Sijaelewa vipi? *Clause 19 (1),* anaomba "*deleting the words conduct research and substituting it with request for research funds from TAFIRI,*" ndicho anachosema. Unaelewa? Kwa hiyo, sisi tulikuwa tunazungumzia *that particular sentence.* Mazungumzo kama yanahama kwenda kwenye neno "*approval*", *that is different,* tutajadili hilo na lenyewe; lakini *at the time being* kwa sababu, jamani tunatunga sheria. Eeh, kwamba maneno yanayotakiwa kuongezwa na naomba nirudie kuyasoma, anasema "*by deleting the words conduct research and substituting it with request for research funds from TAFIRI.*" Sasa hii *it does not concern approval…*

**MBUNGE FULANI:** Hajamwelewa.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Aaah, tumalizane na hili kwanza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kila atapata nafasi ya kusema, mwache Mheshimiwa Waziri mwenye hoja azungumze na Mheshimiwa Dkt. Sware. Mheshimiwa Heche.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sijamaliza. Kwa kweli kama angekuwa yuko *agreed* na neno "*approval*" ambalo hata kwenye Kamati lilileta maneno mengi sana, na yeye alikuwa ni Mjumbe wa Kamati, ange-*move* ku-*amend* neno *approval,* lakini hapa alicho-*move* ku-*amend* ni maneno mengine na siyo *approval* na sisi tulikuwa tuna-*respond* kwa hayo aliyoomba kubadilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware, funga hoja yako.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijafika huko naomba labda nifafanue tena kwa utaratibu. Kifungu hiki cha sheria kinasema kwamba mtu yeyote au *institution* yoyote inayotaka kufanya *research* lazima ipate kibali cha kusema fanya au usifanye kutoka *TAFIRI.* Mimi nikasema hiyo sio sawa. Kwa nini nimesema siyo sawa, tuna *institutions* nyingine, tuna vyuo vikuu, kuna watu binafsi wanafanya *research,* wana *sources* zao za *funds.* Ambacho *TAFIRI* mnakisema kwamba mmepitisha hii ili mpate *information,* nimesema kwamba

tafuteni *other means* za kupata *information* nini kinafanywa kwenye *research* za *fisheries.* Sasa nimesema kama hiki kifungu kinatakiwa kibaki, basi kiboreshwe kiseme kwamba unapoandika *proposal for approval* kwenda *TAFIRI* ni yule tu anayehitaji fedha za kufanya hiyo *research* kutoka *TAFIRI. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwelewa sana Mheshimiwa Dkt. Sware alivyosema hapo, na ninachelea kusema namuunga mkono Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu utafiti sasa umefika kwenye *level* ambayo tunahangaikia vinasaba na vitu *specific* ambavyo ni *endemic* kwenye nchi mbalimbali na sisi tuna vingi hivyo, tunataka tujue kila mtu anayehangaika na vitu vyetu hivyo; na tumeliwa kwenye simba. Yuko Mmarekani mmoja amepata *free ticket* ya kufanya utafiti wa simba, amefanya *genetic research* ambayo ameficha yote.

Kwa hiyo ni vizuri na ukiwa Mtanzania ni vizuri zaidi kushirikiana na taasisi zilizoko ndani ya nchi katika kuendeleza fani ya utafiti ili tujue kwamba kinachoendelea ni nini na lengo la Mheshimiwa Waziri ndiyo hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui niongee Kirangi au sijui niongee lugha gani? Tunaongea vitu vitu viwili tofauti, yaani maelezo ya Mheshimiwa Waziri na ninachokiomba hapa kifanyike, ni vitu viwili tofauti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware, *the way scenario,* unatoa hoja tu ipigiwe kura.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** *Okay.* Naomba nitoe hoja japokuwa sidhani kama Waheshimiwa Wajumbe wanaelewa tunacho-*discuss* ni kitu gani. Hamjaelewa ndiyo maana mnakazania "*approval.*"

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester, Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Makani, Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Riziki nimeshakuandika. Mheshimiwa Nagu, Mheshimiwa Mpina tutatazama nafasi. Nani huko?

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Rehani hutaki kuniona huku. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sikuoni Mheshimiwa Rehani. Haya, Mheshimiwa Rehani. *(Makofi)*

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru angalau umenipa na mimi nafasi ingawa niliomba muda mrefu sana kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nieleze kitu kimoja; anachokieleza Mheshimiwa Dkt. Sware na maelezo yanayotolewa na Wizara yanatofautiana padogo tu. Kinachosemwa, Mtafiti, ni lazima utafiti uweze kusajiliwa ujulikane. Kwa sababu utafiti ni *process,* siyo kitu tu ambacho unakurupuka kwenda kufanya kitu kwa matakwa yako. Lazima *process* ifuatwe na kuna *ethics* za utafiti, lazima zifuatwe, zijulikane na nchi na wale ambao wanamiliki kama *institute* hizo lazima zifuatwe. Isipokuwa kama nimeweza ku-*source fund somewhere,* nimekuja na *proposal* yangu, nimeshaileta kuwajulisha wahusika *(authority)* iwe *TAFIRI*, iwe mtu mwingine

yoyote yule, sawa, nisikae pale kungoja *no objection* kutoka *TAFIRI* wakati yeye hani-*fund* kwenye ule utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema, niwe na uhuru wa kufanya ule utafiti na *results* niweze ku-*submit* kwa yule aliyeni-*fund* lakini na kwa *TAFIRI for country reference*. Hicho ndicho kitu ambacho Mheshimiwa Dkt. Sware anakihitaji na ndicho tunachokihitaji sisi kama watafiti; tupewe *freedom* ya kufanya utafiti ndani ya nchi na tu-*submit* hizo *findings* kwa *authority party. Thank you very much! (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna *two different things;* kuna *approval on one hand* na kuna ku-*collect findings* za *research,* na mimi naungana na Mheshimiwa Dkt. Sware, *h*ivi ni vitu viwili tofauti. Kama *TAFIRI* ina-*fund project then approval should come from TAFIRI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunao utaratibu kupitia *COSTECH,* watu wanaoenda kufanya *research,* kwa mfano, mimi nafanya *research,* nina *proposal* yangu, mnaniwekea *bureaucracy* kwamba mpaka nipate *approval* ya *TAFIRI*, kama kuna *conflict of interest TAFIRI* anaweza akaniambia tu, *yes thank you, we are not allowing you;* nenda halafu wakafanye wao *behind my back. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba kwa kuwa Serikali ina nafasi, *objective* ni kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Maghembe kwamba watu wamefanya *research* wameondoka na *findings,* tuweke kwenye utaratibu wa kanuni kwamba *findings* zote lazima ziletwe *TAFIRI.* Kwa kuwa mtu huyo anapata *approval* kutoka *COSTECH,* tunayo *control mechanism*. Kwa hiyo, tusiweke *bureaucracy* kwa sababu tu labda hatujajiwekea utaratibu mzuri wa kudhibiti. Nadhani *researchers* wetu wasifungiwe milango. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwneyekiti, nakushukuru. Kaka zangu hawa wawili wamesema vizuri sana, sasa mimi niende kwenye hizi *phrasing* zenyewe. *Proposal* ya Mheshimiwa Dkt. Sware, haya marekebisho yake, yanakuja ikiwa hii sentensi itabaki vile, kwamba lazima upate *approval* ya *TAFIRI.* Sasa yeye anasema *approval* hiyo iwe tu kama huyu mtu ana-*request research funds and not* kwamba ana-*conduct research* kama ambavyo Mheshimiwa Bashe amesema. Sasa Mheshimiwa Waziri akaleta maneno ya nyongeza kule mbele ambayo *to me, I am sorry to say, they are just redundant,* hazihitajiki kwa sababu yanarudia yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mjadala ukija, basi kama mnataka kupamba kwa kuweka yale maneno na yabaki hivyo hivyo, basi neno "*approval*" liondoke, lakini bado *point* ya Mheshimiwa Dkt. Sware ni ile ile kwamba *approval* iwe *subject to requesting funds,* lakini *conduct research as such* isihitaji *approval* ya *TAFIRI.* Wao watafute njia nyingine ya ku-*collect data* za *research* zote zinazofanywa kulingana na hii *field* yao, nadhani tumeelewana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Labda tu nianze, tukumbushane kidogo. Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, mimi nilikuwa pale *post graduate*…

**MWENYEKITI:** *No, No,* Mheshimiwa, ni Ester huyu.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mimi hapa, Ester Mmasi ndio mimi Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mimi ndiye ninayechagua. Nimemchagua huyu. Esther Matiko samahani. Ndiyo niliyemwandika hapa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Na mimi nimesimama kuunga mkono anachokisema Mheshimiwa Dkt. Sware. Nafikiri labda ili tupate uelewa wa nini Mheshimiwa Dkt. Sware anasema, Waheshimiwa Wabunge nafikiri mna hivi vitabu, mjaribu kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hicho kipengele cha kwanza ambacho kina-*propose* iondolewe neno *"conduct research"* na iwekwe *"the request for the research fund;"* ukisoma kipengele cha tatu kilivyoandikwa, ukaenda kipengele cha nne *is as if* hii *phrase* imeandikwa kwa yule mtu ambaye anapata *funds* kutoka kwa *TAFIRI and not otherwise. Unless otherwise* labda mnataka sijui mpokwe mamlaka ya *COSTECH,* basi hivi vipengele vingine vyote yaani huwezi ukasema ipite *30 days* kama uta-*approve, then* tuende kipengele cha (4) ambacho kinaelezea kwamba *TAFIRI* ikae ione kiasi gani cha fedha kiwe *approved.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakuja na *proposals* zangu, nimeshapata mtu anani-*fund why do I have to submit my proposal* kwa *TAFIRI?* Nini *role* ya *COSTECH?* Kwa hiyo, nafikiri tukubaliane tu, hapa tunatunga sheria. Mheshimiwa Dkt. Sware alichoki-*submit* kipo *valid,* tukisome tu kwa ukamilifu wake. Hii *framing* inayokuja iwe tu *subject* kwa yule mtu ambaye anataka *funds on TAFIRI. Apart from that* tunajua tukifanya tafiti ili tuweke kumbukumbu, kuna mamlaka tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uki-*submit proposal* wanaweza wakaiba *idea* yako wakakwambia hatu-*approve proposal* yako, kwa hiyo, *research* yako *is not valid.* Kwa hiyo, hii kitu sivyo kabisa. Tumeshaona mara nyingi *idea* za watu zinaibiwa halafu zinafayiwa kazi na watu wengine.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ramo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri mahali pa kuanzia ni pale ambapo tunatakiwa kujiuliza kama Taifa, hoja itakuwa ni fedha au kufanya utafiti? Huo utafiti unaofanyika, manufaa yake kwa Taifa na hasara zake kwa Taifa; lakini hata kama usipoenda kwa majumuisho namna hiyo, nafikiri tukiwa tunaenda kwenye vifungu vya mbele tuwe tunarudi na vifungu vya nyuma. Hii *TAFIRI* imepewa *functions;* imepewa mamlaka, shughuli zake za kufanya. Nenda ukurasa wa nane *section 6(d)* inasema mojawapo ya majukumu yake ni ku-*coordinate research in fisheries and aquaculture, carried out within the mainland Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitafuta tafsiri ya neno *"coordinate,"* mojawapo ya *meaning* yake ni *getting things done in order;* yaani kufanya vitu kwa usahihi, ndiyo maana yake. Sasa unataka kuangalia kama iko *inorder,* ukikuta siyo *inorder* upitishe? *If you find it not inorder,*

maana yake ni kwamba *you will just drop it down,* ndiyo maana yake. Vilevile hata (j) pia ipo naambiwa na yenyewe inasisitiza. Kwa hiyo, tusome sheria mbele, lakini turudi nyuma kwa sababu sheria ni *just only one document.* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kwanza napenda ni-*declare interest.* Mimi niko upande wa Serikali na ninaunga hoja kwa upande wa Serikali.

Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Semesi, mimi na wewe tumetoka pale *Univeresity of Dar es Salaam* pamoja, tuna historia nzuri sana pale. Nikiwa pale ofisi ya *Post Graduate,* nikiwa na-*head section* ya *examination* kwa maana kwamba *viva vote* nasimamia, vitu gani, miongozo yote, ilikuwa mezani kwangu. Utakumbuka kwamba kama *candidate* wa *Master Degree* anaomba kwenda kufanya *research, whether* alikuwa ni *private, whether* alikuwa ni *government sponsored* lazima kuna utaratibu wa kuomba kibali. Hiyo haiepukiki mahali popote. Hatuwezi kufanya Tanzania ikawa shamba la bibi kwa sababu tu kuna maslahi ya pesa katikati, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote yenye macho ya mwilini na macho ya rohoni hatuwezi kuachia nchi yetu tukaanikwa kwenye mataifa ya kigeni kwa sababu tu ana hela yake, haitatokea mahali popote. Naombeni tuitendee haki nchi yetu, hebu tuipende nchi yetu. Jamani huu uvamizi umetokea; tumelia mangapi kwenye Hifadhi ya Taifa pale? Haiwezekani! Tukumbushane tulikopita jamani, haiwezekani! Taratibu hizi ziko mahali pote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja upande wa Serikali na wazo hili nimelileta na ninashukuru Mungu Serikali wameipokea hoja yangu na ninaomba tusonge mbele hivi kama ilivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Heche. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa yote yaliyozungumzwa na hapa hatushindani. Yaani *research proposal* inakuwa karibia asilimia 75 ya *research* yote. Mtu ameshafanya *research proposal* yake, akuletee ukae nayo miezi miwili au mitatu, halafu ndiyo uje umwambie tumekukatalia au tumekubali ufanye *research?* Hii siyo sawa. Yaani wote tusikilize vizuri; na anachosema Mheshimiwa Dkt. Sware ni sahihi, kama anachosema Mheshimiwa Mmasi kuhusu kuomba kibali au kujisajili sehemu fulani ueleweke unafanya *research, we have no problem with that,* ifanyike hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu amefanya *proposal* yake, humpi hata senti moja, aipeleke *TAFIRI;* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa mfano, kinataka ku-*conduct research* wapeleke *TAFIRI* wakaombe kibali, sijui mimi nataka kufanya *research,* nipeleke *TAFIRI.* Ukiritimba wa nchi hii wote tunaujua; na sasa tulikuwa tunaanza kupunguza mambo ya ukiritimba, lakini tunayarudisha kwa mgongo wa nyuma kwa kutumia sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kuna wakati tutapitisha mambo humu watu watakuja kushangaa hawa watu walikuwa wanatumia akili za aina gani? Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waelewe vizuri haya mambo mawili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kumwambia Mheshimiwa Dkt. Sware kwamba yeye ni Mjumbe wa Kamati yetu na tuliufanyia kazi huo muswada kweli; na siyo hiyo tu, hiyo haitoshi, ndiyo maana tuna hii *session* sasa hivi kwamba hatukatai mawazo ya watu wengine. Sasa nirudi kusema *limits* za *powers* za hii *institution* zipo kwenye *clauses* nyingine, hiyo moja.

Pili, *amendment* iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri inakubali kwamba kuna *organizations* nyingine, inakubali kabisa, someni hiyo *amendment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya tatu, nataka kusema, hivi ni fedha tu ambazo tunazilinda au tunalinda na *resources* ambazo zinatumika ndani ya nchi hii kufanya *research?* Siyo hiyo tu; ya nne, ni kwamba hivi mnajua kwamba kunaweza kuwa na watu ambao watafanya *research* na kupotosha mambo ya nchi yetu? Kwa hiyo, kuna mambo mengi ambayo yanahusika hapa zaidi ya fedha, lakini nashukuru kwamba Wizara imefanya *amendment* ya kujua… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Nagu kwa mchango wako. Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Kigwangalla jiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti hoja yangu aliisema vizuri sana Mheshimiwa *Engineer* Ramo, kwa hiyo...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, labda ngoja na wanasayansi tusimame tuseme kidogo. Wengine tumeishi na kupata ugali wetu kupitia *research.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye dunia ya tafiti hususan tafiti ambazo zinahusu *subjects* kama binadamu, wanyama, mifugo, *resources* za baharini, *resources* ambazo zina utajiri, huwezi kuruhusu mtu yeyote yule awe wa ndani ya nchi ama wa nje ya nchi kwenda kupewa kibali tu na…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla hebu kaa kidogo. Kaa kidogo, samahani. Kaa tu dakika moja. Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 153 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kutoa hoja ya kutengua Kanuni ya 28(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo inaelekeza vikao vya Bunge kumalizika saa 1.45 usiku na badala yake tuendelee na shughuli iliyoko mbele yetu hadi hapo tutakapoimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:** Kamati ya Bunge Zima inaendelea.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima. Tukae, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Sianzii kwenye ugali, naanzia kwenye mkate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa najaribu kutoa kama utangulizi ni kwamba kwenye tafiti mbalimbali ambazo zitahusisha *subjects* ambao nimewataja kwa mfano *resources* kama za baharini, za wanyama, za mifugo, za maliasili iliyoko huko msituni, binadamu yaani *human subjects* ni lazima mamlaka ya kisheria iliyoundwa na nchi husika kusimamia tafiti za sekta hiyo itoe *clearance* kwenye *research* yoyote ile itakayohusisha *subjects* ambayo inawasimamia. Kwa sababu taasisi hiyo inakuwa ndiyo *think tank* kwenye nchi inayofanya mambo mbalimbali ya tafiti, ugunduzi na ulinzi wa kisayansi wa *subjects* ambao wapo kwenye sekta husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa msingi huo sasa, pamoja na kuwepo kwa *COSTECH* ambao wanahusika na kutoa *research permit,* pia kwenye *research* zinazohusisha *human subjects,* kwa Wizara ya Afya kuna Taasisi inaitwa *The National Institute for Medical Research (NIMR)* ambao ni lazima tafiti yoyote utakayoifanya kwenye sekta ya afya, kama inahusisha binadamu, ni lazima *NIMR* wakupe *clearance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa msingi huu Serikali inaleta mapendekezo ya kuwapa nguvu *TAFIRI* kupitisha tafiti zote ambazo zitahusisha mambo ambayo yapo kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, unataka kuongezea?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa namna ulivyotumia busara kuruhusu mjadala kuhusu jambo ambalo halijaombewa *amendment,* kwa sababu hakuna *amendment* yoyote inayo-*propose* tuondoe neno "*approval.*" Pamoja na hayo, napenda tena kwenye *a serious note* kuwashauri Waheshimiwa Wabunge, watuelewe katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuleta muswada huu ni *precisely* kuweza kuweka *mechanisms* za *control* katika utafiti. Kwa hili, naomba Waheshimiwa Wabunge, tuangalie maslahi mapana ya Taifa na tuache ushabiki au kufanya mjadala ambao ni wa kiuanazuoni zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa muda mrefu sana imekuwa shamba la bibi kutokana na *biopiracy* na *bioprospecting* kwa sababu ya jina na kisingizo cha utafiti. Kuna

mimea ya nchi hii na jinsi za wanyama zimeshakuwa *patented* nje kimsingi kwa sababu hatuna namna tunavyo-*control research. (Makofi)*

Kwa hiyo, lengo la kuleta muswada huu siyo kudhibiti *research* ya kiuanazuoni, ndiyo maana tumeleta *amendment* inayosema kwamba vyuo vikuu na taasisi za kiuanazuoni hazitanyimwa kuendelea na utafiti wao kama kawaida. Tunachofanya, tumeleta utaratibu wa kulinda maslahi ya nchi ili tuweze kuwa na njia ya ku-*control* nani anafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama leo hii tukiruhusu mtu kwa sababu tu ana fedha, anakuja anaenda sehemu yoyote anafanya utafiti, tutakuwa tunapoteza vitu vingi, tutakuwa tunahatarisha rasilimali tulizonazo. Kwa hiyo, naomba mtuelewe kwamba lengo hasa ni kuleta *control* ili kuwe na taasisi ambayo ndiyo hasa ina-*vet* na ku-*determine* aina ya *research* ambayo tunairuhusu kwa malengo ya kulinda maslahi ya Taifa letu. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imetolewa hoja kwamba kama mtu anapata *funding,* basi haina haja ya kuomba *approval.* Nilichosema ni kwamba, ilivyoandikwa kwenye kifungu 19 ni kwamba hata baada ya ile *proposal* kukubaliwa, bado kuna hatua nyingine ambazo taasisi inaangalia katika mchakato mzima wa kuruhusu na kuweka *timeframe* ya ile *research.* Kwa mfano, *proposal* ilishakubaliwa, bado itaangalia mambo mengine ikiwa ni pamoja kuulizwa; je, una fedha wakati huo huo hauna? Ndiyo *essence* ya hiyo *sub-section (4). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ndiyo wataangalia na kukuwekea *timeframe* kulingana na vigezo kwamba tayari una fedha au hauna. Ndiyo lengo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naombeni pamoja na kwamba hakukuwa na *movement* yoyote ya *amendment* kuhusu hili, naomba Waheshimiwa Wabunge tuelewane na tutangulize maslahi ya nchi yetu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hatukutumia busara kuleta hii. Hii *amendment* ipo, sisi tunayo hapa. Mheshimiwa Dkt. Sware funga hoja yako. Tumechukua muda mwingi sana kwenye hoja yako.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nafikiri imechukua…

**MWENYEKITI:** Najua unazo nyingine, tutahoji moja kwa moja. Moja baada ya moja…

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** *Yah!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka ni-*make it clear* au ni *clarify* au nisisitizie kwamba hakuna kanuni inayomzuia Mjumbe wa Kamati husika kutoa hoja kuhusu jambo fulani linaloongelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sikuwepo kwenye Kamati wakati mna-*discuss and you know that.* Kwa hiyo, huwezi kuniongelesha kama vile kwa nini naongea wakati niko kwenye Kamati husika. *(Makofi)*

Tatu, *issue* inayoongelewa hapa, nilichokuwa naki-*propose* kama *TAFIRI* inataka kufuatilia *information* nani anafanya nini kwenye *fisheries,* itafute *clause* mpya iandikwe humu

ndani *or mechanism* ya kupata *information* na *patent rights.* Hata hizo *patent rights one of the clauses is clause No. 24* imesema kuhusu *patent.* Kwa hiyo, udhibiti, *research results* zinabaki na nani na nani alifanya hiyo *research, you can still do that;* lakini hii *clause 19* inambana mtu *either* unatoka kwenye *institution* au *as a person* unataka kufanya *research,* basi lazima *TAFIRI* uiandikie *proposal* yako, *TAFIRI* ndiyo iseme ndiyo au hapana.

**MBUNGE FULANI:** Ni sawa.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo sawa, siyo sawa. Ndiyo hicho ninachokisisitiza. Ninyi mnataka ku-*control* nani anafanya *research* ya *fisheries?* Si ndiyo! Ili kwamba *whatever results* au nini kimekuwa *discovered,* kiwepo *TAFIRI* kijulikane na ndiyo kazi ya *TAFIRI*. Sasa *TAFIRI* yenyewe kama *TAFIRI* haina *capacity.* Tupo *researchers* wangapi *in terms of capacity?* Tuko *researchers* wangapi na *TAFIRI* ita-*handle proposal* ngapi ili *in 30 days* uniambie *go ahead or not?* Hiyo *capacity* mnayo? Haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hapa hapa hii sheria yenyewe ndiyo maana nikasema iseme kwamba *researcher seeking for funds from TAFIRI* ndio aandike hiyo *proposal,* ukishuka huku chini, hata kwenye hiyo *sub-section (4)* inasema kwamba itani-*determine* mimi ninaye…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Dkt. Sware umekubaliana au unataka kuingia katika kulihoji Bunge?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sijui tunapigia kura nini, maana kuna *different views,* kila kitu kimekuwa *politicized…*

**MWENYEKITI:** *No! No! No!* Tunapigia kura hii hoja yako tu.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui napigia kura *approval* au napigia kura kwamba hiyo tu-*rename…*

**MWENYEKITI:** Kifungu chako wewe ni cha 19, ikawa na *clusters* ambazo kama nilivyokwambia, hukuchukua ushauri wa kisheria kuandaa *amendment* yako, kwa sababu ungechukua ushauri wa kisheria zote hizi zinawekwa kiutaratibu. Zina-*appear* zote lakini kwa utaratibu maalum kwenye *amendment.* Umeifanya iwe kama *segment* kwa *segment, cluster* kwa *cluster.* Sasa ushauri wangu ulikuwa tunapiga kura kwa kifungu chako namba 19 tu.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Chote?

**MWENYEKITI:** Ambacho ulikirekebisha.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Basi ni hiyo tu. Sasa unataka tupige kura au umekubali yaishe?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubali vipi yaishe?

**MWENYEKITI:** Yaishe.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** *No! No! No!* Sijakubali yaishe. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umeshatamka lakini.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wapige kura ibaki kwenye *Hansard*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, unabadilisha?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kubadilisha nini?

**MWENYEKITI:** Kauli yako.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ipi?

**MWENYEKITI:** Ulisema unakubali yaishe. Kwa hiyo, unataka kura ipigwe? Kaa tu, tutapiga kura haina tatizo.

*(Hoja ya Mhe. Dkt. Immaculate Sware ilikataliwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunakwenda kwa Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mjadala ulivyokuwa mrefu hapa, kuna kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kidogo nimeielewa lakini naomba wasilisho langu liweze kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kiingie Kifungu kipya kwenye kifungu cha 19(4), kwa hiyo, kitakuwa hii *su-bsection (e)*. Hii inatokana na 19(4)(a) kwamba ikishakuwa mtu *proposal* yake iko pale atapewa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kuwa mtu amepewa pesa, ukienda kifungu cha 22 kinaelezea mtu ambaye ameshindwa; utafiti wake ume-*fail* na kinamhitaji arudishe ile fedha na ameshatumia. Kwa sababu ya udhaifu wa kifungu cha 22 ndiyo maana hapa kwenye kifungu cha 19(4) nimependekeza kiongezwe kidogo hicho cha (e) kwamba "*the amount of funds approved shall be reimbursed as per submitted research project.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, mantiki yake ni nini? Badala ya kumpa mtu fedha *in advance* anafanya kazi na kutokana na zile kazi zake anazofanya, ndiyo tunakuwa tunam-*reimburse* kwa *the whole proposed budget.* Hiyo ndiyo mantiki ya hiki kifungu ili hasara ya Serikali na hii taasisi ambayo imetoa fedha tunaondoka kwenye ule uhatari wa kupoteza fedha kwa mtu ambaye anafanya utafiti ambao hauna faida halafu baadaye tunaukataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maoni yangu kwa Serikali kama tutakubaliana, basi itakuwa ni vyema au kama Mheshimiwa Waziri atatoa maelezo ya kutosha, kama ataweza kuliweka vizuri kwenye kanuni, nitaanza kumsikiliza yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo anayozungumza Mheshimiwa Mbogo yamejadiliwa sana pia kwamba mtu ameandika *proposal,* imekubaliwa, ameomba pesa amepewa, ameanza utafiti, halafu *somewhere* katikati hapo anaamua tu kuacha na kutokomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki kifungu kilikuwa kinamwekea kama *mechanism* ya kutotumia vibaya hiyo fursa aliyopewa ya kufanya utafiti, ili awe anajua kwamba ikifika mahali akaamua tu kuacha kwa utaratibu ambao kwa maoni ya taasisi itakuwa hakufanya sawasawa kama ilivyotaka sheria, basi arudishe hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kuna neno *prescribed* hapa ambalo linaashiria kwamba maelekezo aliyokuwa amepewa wakati anapata hizi fedha kwa ajili ya *research.* Kwa hiyo, hiki anachokisema Mheshimiwa Mbogo, nadhani hii sheria tuiache isimame hivi kama ilivyo na tulipeleke kwenye kanuni ambayo itatengeneza na utaratibu mwingine zaidi. Kwa sababu hata hapa ilivyo haisemi kwa ufasaha wake wote kwamba hata *reimbursement process* ile itafanyikaje.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MGOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naiomba tu Serikali ielewe kwamba kwa sababu kifungu cha 19(1) tumesema kwamba ile *proposal* mtu akiwasilisha tumeiona halafu ndiyo tunai-*approve,* tunampa *go ahead;* kwa hiyo, tulikuwa tumeona kitu ambacho kimefaa. Basi naomba tu niungane na Mheshimiwa Waziri kwamba kwenye Kanuni wakiweka utaratibu mzuri, na kwa sababu *proposal* tumeshaipitisha kwamba ni nzuri inafaa, *go ahead;* basi tutumie mfumo wa *reimbursement* kwa gharama ambazo ameingia ili kwa kifungu cha 22 tusiweze kupata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa hoja ya kanuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa nitawahoji, kifungu hiki cha 19 pamoja na marekebisho ya Mheshimiwa Mmasi, Mheshimiwa Mbogo na Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina *amendments* hapo kwenye *clause 20* ambayo ilikuwa inatoa adhabu kwa mtu yeyote ama mtafiti yeyote, *whether it is a local researcher* ama *an external researcher,* kwamba atakaposhindwa ku-*submit his or her final report then* atakuwa ametenda kosa la jinai na badala yake atapaswa kulipa shilingi milioni 10, *incase* huyu atakuwa ni *local research* au kifungo cha miezi sita; na akiwa ni *external researcher,* basi atapaswa kulipa shilingi milioni 20 za Kitanzania au kifungo cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimeshauri kwamba tu-*delete* ile *six months and replace with "one year but not exceeding three years."* Kwenye *paragraph (b)* tu-*delete "one year" and replace it with the phrase "one year but not exceeding five years."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ni dhahiri kwamba kwa kweli kama tulivyo-*argue* hapa kwa muda mrefu kulingana na hoja ambayo ameleta pale Mheshimiwa Dkt. Sware, ni kwamba tunahitaji kulinda maliasili ya Tanzania. Pia kwenye suala hili, kwa nini nasema hivi? Ni kwamba tunahitaji pia ku-*envy institution memory* kwenye tasnia nzima ya tafiti ya viumbe hai vya baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tusipofanya hivi, kuweka sheria kali, tunaweza ku-*endanger* hizi *marine species* kwa maana ya samaki na viumbe hai vya baharini. Pia kama alivyosema Mheshimiwa mama yangu Mheshimiwa Dkt. Nagu pale, ni kwamba imefika mahali kumekuwa kuna kelele nyingi duniani, uongo mwingi duniani. Kwa hiyo, ni lazima tuweke *controls* lakini pia na adhabu kali kwa mtu ambaye atashindwa ku-*comply.*

**MWENYEKITI:** Sekunde tano, maliza.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuwasilisha hoja yangu kwa Serikali na ninaomba kwa moyo mkunjufu kabisa waipokee.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ombi lenyewe ni la kuongeza adhabu, sisi tunaliridhia tu. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa langu ni dogo tu. Katika kifungu ya 20(1) kwamba mtu kabla hajapeleka *research proposal* kule kwenye taasisi anatakiwa apate *certificate of clearance* toka *COSTECH.* Sasa mawazo yangu hapa ni kwamba hii *certificate of clearance* itolewe moja kwa moja na taasisi ili tupunguze urasimu. Kwa mfano, maeneo mengine unakuta mtu mpaka upate kibali *TFDA,* sijui *TBS;* ni mzunguko mrefu. Kwa hiyo, tujaribu *as a shortcut;* taasisi yenyewe itoe *tax clearance* halafu mtu ana-*submit proposal* kuliko nenda *COSTECH,* rudi na mazingira ya kazi. Kwa hiyo, tujaribu kubadilisha mazingira ya kazi kupunguza urasimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Serikali.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli inajengeka dhana kama vile hili jambo la kwenye *COSTECH* ni urasimu, lakini tukumbuke kwamba iko Sheria ya *COSTECH* tayari ambayo inawataka hawa *foreigners* kupata *clearance* pale; na kwa kweli hapa kinachosemwa ni kama kuweka tu msisitizo kwamba *foreigners* hawa watapata hizo *clearance* kutoka *COSTECH* kwa ajili ya kufanya *research.* Watakapokuwa wanakuja sasa kwenye eneo la *TAFIRI* bado watatakiwa ku-*submit* hiyo *proposal* kwenye kifungu ambacho tumekijadili hapo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wapate hiyo *clearance* na ndiyo utaratibu wa sheria ambayo ina-*exist* tayari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli hiyo sheria ipo lakini tujaribu kuwa na *one stop shop,* siyo mtu anaenda huku, huku na huku. Mtu ajue akienda sehemu moja, anafanya vitu vingi anaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri ni suala tu la Serikali kuchukua ushauri. Kama ni kwenye kanuni, wachukue taratibu za *COSTECH,* jinsi gani ya kutoa *clearance certificate,* ndiyo waziweke kwenye kanuni, lakini iwe ni *one stop shop* ili tuharakishe, tuendelee na kasi na awamu ya tano hii.

**MWENYEKTI:** Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(2)(b) cha sheria ya *COSTECH* ndiyo imeweka hilo sharti kwa ajili ya mtafiti anayetoka nchi za nje. Kwa hiyo, ukitaka ubadilishe hii, uende ubadilishe na ile sheria, tutakuwa na sheria ambazo zinapingana.

Kwa hiyo, naomba kuwashauri Waheshimiwa Wabunge, nia ya Mheshimiwa ni nzuri lakini katika moyo ule ule wa kulinda maslahi ya nchi yetu kwenye mambo kama haya, nadhani ni vyema kwanza hawa watu wanaotaka kufanya *research* kutoka nje ya nchi wapate hii *clearance.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo tayari sheria hii. Kwa hiyo, hata ukiondoa hapa, bado utaenda kule. Sasa ili hizi sheria zisomeke sawa, nilikuwa nashauri kwamba ni vyema hiki kifungu tuki-*retain* hivi hivi kama kilivyoletwa kwenye mapendekezo ya Serikali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sisi ni watunga sheria na nafasi tunayo hata kipindi kingine, basi naunga mkono hoja ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 21

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilipo-*propose* hii ilikuwa inaenda sambamba na *clause 19.* Sasa kama *clause 19* haijafahamika, basi hiki nilichokuwa na-*propose* kiko *redundant*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, *amendment* yangu ni kama ilivyowasilishwa na kupokelewa na Serikali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kifungu hiki kinaafikiwa pamoja na mapendekezo ya Mheshimiwa Mmasi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati na-*propose* hii, nilikuwa nataka kujua kama *TAFIRI* inakuwa kama ni *stamp* ya kusema fanya ama usifanye *research* au inataka kudhibiti *information* ambazo zipo kwenye *fisheries*. Sasa kama yenyewe inafanya vyote; inadhibiti na kuchukua *information*, basi pia hiki ninachoki-*propose* kiko *redundant.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kifungu hiki kinapita na mapendekezo ya Serikali?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 23

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA. M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta mapendekezo yangu hapa kwa sababu kifungu cha 23(4) kinaonesha kwamba kama kuna mtu maamuzi yake hayajakubaliwa, atakata rufaa kwa Waziri. Sasa napendekeza hapa, kama huyu mtu atakuwa amekataliwa na taasisi, maana yake akate rufaa kwenye Bodi; kama atakuwa hajaridhika na maamuzi ya kwenye Bodi, pia anaweza akakata rufaa kwa Waziri; na hata kama hajaridhika na maamuzi ya Waziri anaweza akaenda kwenye hatua nyingine za kisheria kwa maana ya Mahakama Kuu na nini, ndiyo ilikuwa hoja yangu hapa. Yaani kuwa na ule mlolongo kwamba mtu anaweza akapata haki, kusiwe kumefungwa kwa upande mmoja kwamba kama hajaridhika akate rufaa kwenye bodi ndiyo itakuwa *final*; au Waziri ndio mtu wa mwisho. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachopendekeza Mheshimiwa Waitara ni kitu ambacho kitakuwa kinaanza upya, kwa sababu katika hali ya kawaida hata katika utaratibu wa kufanya maamuzi hauchanganyi *executive* na *judiciary* katika sehemu moja, kwa sababu ni *organs* tofauti. Kwa hiyo, kwa kawaida sheria haiwezi kuandika kwamba kama huridhiki na uamuzi wa Waziri, basi unaenda Mahakamani. Tunachosema tu ni kwamba hata kama haijaandikwa haimzuii mtu kwenda kwenye Mahakama Kuu ku-*challenge* uamuzi wa Waziri; lakini huwezi kuwaweka kwenye sehemu moja kwa sababu siyo *organ* moja yaani huwezi kuweka kwamba Mahakama Kuu ni *level* ya *appeal* ya Waziri, kwa sababu mwingine ni *executive* na mwingine ni *judiciary*.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge ajue tu kwamba hata isipoandikwa, sawa, bado kuna fursa ya kufanya kitu kinachoitwa *judicial review* au mapitio ya sheria. Kwa hiyo, mara nyingi imetumika tu na maamuzi ya Waziri yamebatilishwa na mahakama kama imekiuka, haijafuata sheria, imekiuka utaratibu na imevunja kanuni za asili za haki. Kwa hiyo, hata kama

haijaandikwa haimaanishi kwamba mtu hana nafasi ya kwenda Mahakama Kuu. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu na hicho kifungu kipya. Ana kifungu kipya anaomba kiingie.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hicho nasema kwamba pamoja na nia yake njema, lakini katika weledi wa kuandika sheria, hatuandiki hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siyo kweli, Mheshimiwa Naibu Waziri hakuwepo huku Bungeni, hata miswada iliyopita kuna mahali tulipitisha hivyo na ndiyo maana nika-*refer* hii. Siwezi nikakubaliana naye kwamba hii habari ya kwamba labda kama mtu hajaridhika anaweza akaenda mahakamani, hiyo inaweza isitajwe, haina shida; lakini hapa akasema mtu anaweza akaenda kwenye bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mtu hajaridhika na maamuzi ya bodi, basi anaweza akakata rufaa kwa Waziri. Sasa kama mtu atakuwa hajaridhika na Waziri akaenda mahakamani, ni jambo lingine; lakini miswada iliyopita tumeweka maneno haya haya na yalipitishwa na Bunge hili hili.

Kwa hiyo, tutaomba kama hatujakubaliana, basi angalau nipate fursa niwaombe Wabunge tupate kujadili katika hili.

**MWENYEKITI**: Ana-*pray* kuwa kama bodi ikishindwa, Mheshimiwa Waziri inakuja kwako au kwa Waziri, *that is what he want.*

**WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Sawa, hiyo tunakubali, isipokuwa mambo ya mahakamani…

**MWENYEKITI**: Kwa hiyo, ya sita ni *redundant* kwa sababu tayari inakuwa *accommodated* Kikatiba na nini. Mheshimiwa Waitara, umeridhika?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kama amechukua hiyo hoja ya Waziri kuwa rufaa, naunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Tuendelee.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 24

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na-*propose* kwamba baada ya neno *"institute",* tuweke *'comma' (,)* halafu tuongezee "*aknowledge the researcher in question."*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri 24(1).

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, anachopendeza Mheshimiwa Dkt. Sware ni kwamba sentensi au kifungu hicho kisomeke kwamba; *"where as a result of any research carried out by or on behalf of the Institute anything is discovered, the discovery shall become the property of the Institute"*, halafu *comma (,) "acknowledge the research in question."* Sioni*,* kama inaleta *flow* nzuri, labda kama mimi sijaelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware. Anataka mumtambue na yule. Mali hii inabaki ya chombo cha umma, sasa yule mtu naye awe *complimented* kisheria, ndiyo hoja yake. Je, naye atatambuliwa au mnao utaratibu wa ku-*acknowledge* watu kama hao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Sware ni mwanazuoni na mtafiti mbobezi, anafahamu kabisa kwamba katika utafiti, kawaida wale wote waliohusika na hasa kama kweli, yaani mtafiti mwenyewe kawaida atakuwa *acknowledged,* sasa kuandika tena kwenye sheria ni yale yale anayosema kwamba kwenye sheria huwezi ukaweka kila kitu. Huwezi kuweka kila *detail* iliyopo, lakini kawaida ndiyo *practice* duniani kote lazima kum-*acknowledge researcher.* Nashukuru sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 26

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa. Kifungu kipya kilichoandikwa na Serikali kina mtiririko mzuri kwa sababu ya ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kuanzisha mfuko na vyanzo vyake, lakini sasa unaposhuka kwenye hiyo Ibara ya 26, uende nayo mpaka Ibara ndogo ya (6) *"the board shall submit with Minister the report under sub-section (2),"* sasa ukienda juu *sub-section* (2) inasema: *"the objective of the fund shall be to facilitate and to support fisheries reseach and such other functions of the institute."* Sasa inatupoteza, lakini ukishuka unaona wanachotaka kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako, kwa sababu haya yanahusu hesabu za mfuko, ukaguzi wa hesabu hizo namna ya kuwasilishwa Bungeni kupitia kwa Waziri; haya unayakuta yameandikwa kuhusiana na *institute* shughuli za mwaka za *institute* vizuri tu katika vifungu vya 33 na 34 ya muswada tutakapofika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nashauri, kama Serikali, yaani mtoa hoja mwenye muswada, kwa kifupi, tunaandika hapa kuyachukua yote yaliyopo kwenye (6) na (7) na kama unaniruhusu nisome.

**MWENYEKITI:** Soma, soma!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuwa na kifungu kidogo cha (5) tu kinachosema hivi: *"the provisions of section 33 and section 34 of this act relating to the preparation and submission of the annual report and laying of audited account of the board before the National Assembly shall, mutatis mutandis, apply to the fund."* Utakuwa umekokotoa yote mazuri ambayo kwenye vifungu vya 33 na 34, lakini itahusu huu mfuko ambao unaanzishwa hapa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi anachopendekeza Mheshimiwa Chenge kinaleta maana zaidi na inatusaidia kuondoa huo mkanganyiko wa hicho kifungu alichosema. Tutamwomba tu baadaye atuletee sasa kimaandishi haya maneno kwa sababu alikuwa nazungumza haraka ili tuweze kuyachukua, lakini kimsingi tunakubali. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na marekebisho aliyokuwa anayasema mzee wetu *(senior citizen)*, kuna maneno madogo tu kwamba kwa sababu kutakuwa na zile *audited accounts* na bodi imepewa miezi mitatu na kalenda ya Serikali mahesabu yanafungwa tarehe 30 Septemba, kwa hiyo, hii miezi mitatu hatuwezi kuwa tayari Mkaguzi Mkuu wa Serikali ameshafanya kazi kutokana na kalenda. Kwa hiyo, napendekeza kutoka miezi mitatu iende mpaka miezi sita ili tuendane na kalenda ya kufunga mahesabau na

pia ratiba ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya na baadaye inawasilishwa kwa Waziri na Waziri anawasilisha kwenye Bunge.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na mapendekezo yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37
Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati yaBunge Zima bila mabadiko yoyote)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 2

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye jedwali hili ni pale ambapo unaangalia muundo wa bodi. Sasa nilikuwa napendekeza kwa sababu, bahati nzuri ukiangalia kazi za wajibu ule kwenye *section 16* imeeleza vitu vingi sana, lakini pia na haya mengine ambayo tumepitisha muda mfupi uliopita, inaongeza nguvu. Kama ni muhimu sasa na hii hapa kwamba lazima iwepo, iweze ku-*approve research* mbalimbali, nilipendekeza watu wafuatao waingie humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, niliyopendekeza ni kwamba kuwe na mwakilishi kama kuna *umbrella of fisheries researchers organization* au wawakilishi wawe humo ndani, na mimi nikaona ni jambo zuri kwa sababu kama wanahitaji kupata kibali na nini, itawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nikasema ni muhimu kwa sababu hapa kwenye ile *section 16* inaonesha kwamba watakuwa wanaangalia pia na chakula na ubora na namna ya kusafirisha. Kama ni muhimu sheria ikataja kwamba katika hii taasisi kutakuwa na uwakilishi wa hawa watu wa Mamlaka ya Chakula *(Food and Drug Authority)* hata kama mazao yanaenda nje ya nchi, tayari tuna udhibiti ndani ya nchi na tumepitia vizuri. Nikasema hapa kuna tafiti zinaweza kufanyika lakini, tumepitisha sheria ya kuwa na *Government Chemist Laboratory Authority,* lakini kuna wale *professionals* na wenyewe wanawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilisema liwepo ni hawa *Fish Processing Industries,* wawe na mwakilishi katika eneo hili.

La mwisho, tumetaja hapa kuna vyuo vikuu ambavyo tayari vinafanya kazi hizi kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *aquatic sciences* na *applied science* zipo pale. Sasa tukasema ni muhimu hawa watu, kama ni taasisi ya utafiti, kama kuna mtu ambaye amebobea akiwa mwakilishi wa taasisi ile, hata itasaidia kuimarisha *knowledge* na vitu vingine vya namna hiyo. Kwa hiyo, ni muhimu hawa watu wakaongezwa kama wawakilishi katika taasisi. Ndiyo mapendekezo yangu.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni taasisi yenye malengo mahususi kabisa na watu anaowataja Mheshimiwa Waitara msururu wake ni mrefu sana. Kwa sasa hivi anasema *TFDA*, sijui nani na *somewhere down the line* zinaweza pia zikapatikana taasisi nyingine ambazo ziko *somehow related* na mambo haya ya utafiti au hata ni watumiaji wa matokeo ya utafiti kama anavyosema viwanda vya samaki na kadhalika. Kwa hiyo, haiwezekani hii sheria tukaitengenezea bodi ambayo inajaribu eti ku-*accomodate* watafiti na watu wenye kuja kutumia hizo *product* za utafiti, wote tukawaweka kwenye bodi *at the same time*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza tuiache hivi hivi kwa sababu hawa angalau waliotajwa hapa wanatosha sana na kwa sababu wale watatu waliosemwa kwamba wenye ueledi maalum unaohusiana na habari za utafiti wa samaki wanaweza wakatoka kwenye hizi taasisi mbalimbali *interchangeably.* Kama inaonekana *this time* alikuwako mtu kutoka taasisi fulani bodi ikiisha wakateuliwa wengine, anaweza; lakini hatuwezi tuka-*accommodate group* lote la Watanzania wenye maarifa kuhusu mambo ya samaki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikakubali tu kwamba huu mlolongo wa hawa watu waliopendekezwa wakapunguzwa. Nikupe mfano, huwezi kuwa na taasisi ya utafiti wa mambo ya baharini na viumbe vingine halafu ukaacha kui-*include* chuo kikuu cha nchi ambacho kinafanya kazi hiyo kufundisha watu. Maana yake ile taaluma itasaidia hata katika kuboresha mitaala mbalimbali na wale wataalamu wenyewe watasaidia pia hata kuboresha utafiti wao. Kwa hiyo, nikadhani tungeweza kuona uwezekano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, huwezi kuwa unazungumza na taasisi ambayo inahusiana na mambo ya utafiti wa samaki na viumbe wengine baharini, lakini ukaacha kuhusisha kwa namna yoyote ile watu ambao wana-*deal* na viwanda vya ku-*process* hawa samaki kwa maana ya uwakilishi. Kwa sababu utafiti umesema ni kuboresha mazao ya samaki na wadudu wengine, lakini vile vile soko linaenda mpaka nje ya nchi. Kwa hiyo, nadhani hii ingeweza kusaidia. Nakubali kwamba tupunguze lakini angalau hivi vyuo vinavyohusika na taaluma hii moja kwa moja, hii ni taaluma, ni *professional,* wakawakilishwa; lakini pia na wao watakuwa wanahusika na haya mambo ya viwanda vya samaki. Kwa hiyo, ni jambo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu nime-*take and give,* naye angalau apunguze kuwe na wawakilishi, nasema ni muhimu sana tunapokuwa tunaanzisha taasisi ambazo hakuna uwakilishi wa vyombo tulivyonavyo; kama jana tulipojenga hoja ya ile Sheria ya Taasisi ya Kilimo, ni hilo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri a-*accommodate* hili kwa maana ya uwakilishi wa wataalamu wetu, lakini kama ataona haifai, basi naomba tupate fursa ya kupata mjadala mpana zaidi tupate maoni ya watu wengine ili kufanya *substitution* ya hiki ambacho nimewasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lililoletwa kwenye muswada linaendana na *practice* ya sasa iliyopo kuhusu bodi. Kimsingi unapopendekeza kwamba bodi iwe na Wajumbe 15 na kuendelea, nafikiri haiendani na dhana ambayo sasa Bunge hili limekuwa likizungumzia sana kuhusu kubana matumizi, lakini vilevile hata leo hii tayari Waheshimiwa Wabunge walisema tuondoe nafasi ya *Deputy Director General* kwa sababu ya mambo hayo hayo. Nafasi zile tatu ambazo hazijatajwa *specifically* ni ili kutoa fursa kwa Waziri kuweza kuteua kutokana na uhitaji wa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukianza kusema sasa tuwaweke hao ambao anawapendekeza Mheshimiwa Waitara, bado kuna wadau wengine muhimu ambao na wao wangependa kuwekwa kwenye bodi. Labda kama tukiamua na tunaweza tukakubali, sidhani kama kuna shida na hii haitakuwa tunaanza kwenye muswada huu, tunaweza tukasema kwamba, bodi inaweza ku-*co-opt any person for the purpose of assisting it on any matter or issue but such convenient person shall have no right to vote in such a meeting.* Maana yake, ili kutoa fursa hiyo ambayo anazungumzia, tunaweza tukaweka hicho kipengele kwenye kanuni ili kisiwe *permanent* ili iruhusu wadau mbalimbali waweze kuja kwenye bodi kama wanahitajika kufanya hivyo. Nafikiri itakuwa imekidhi matakwa au hoja anayotoa Mheshimiwa Waitara. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Je, mkiongezea kwenye kanuni? Mkiweka kwenye kanuni?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hiyo kwenye kanuni.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubali kwamba yeye ametoa hoja muhimu tu kwamba hiyo ya ku-*co-opt* iende kwenye kanuni kama ataona bodi

inahitaji, lakini pendekezo langu hiyo habari ya idadi ya 15 mimi leo sikuitaja nikaacha, nikasema tuwe *professional.* Hii ni taasisi ya kitaalam ya kisayansi ya utafiti, basi acha nyingine zote, hao anaosema Mheshimiwa Waziri, namba *roman (ii),* "Wajumbe wasiopungua watatu lazima wawe wataalam katika nyanja za uvuvi au kwenye viumbe kwenye maji." Hawa ni wataalam wameshamaliza vyuo, wapo mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza sasa angalau hii tuwe na uwakilishi wa vyuo vikuu ambavyo vina-*deal* na huu utafiti; yaani waingie uwakilishi moja kwa moja yaani kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu moja ni kwamba hii ni taasisi ambayo inashughulikia utafiti wa samaki na viumbe vingine baharini Tanzania; lakini vilevile hii moja, huyu mtaalamu atasaidia kuongeza utaalam katika taasisi hii.

Pili, kila kinachofanyika hapa, atasaidia kubadilisha mitaala kwenye vyuo vyetu vikuu ambavyo vina-*deal* na samaki na utafiti wake. Kwa hiyo, unapanua wigo wa uelewa, kuwe na uwakilishi; na hii ni *promotion.* Kwa vyovyote, nilikuwa naomba angalau liingie moja, mengine wacha, lakini angalau uwakilishi itajwe kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, si amesema itakuwa *complimented* kwenye kanuni.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba iingie kwenye sheria kwamba kuna uwakilishi.

**MWENYEKITI:** Kanuni ndizo zinazoendesha sheria. Mimi nafikiri hoja yako na Mheshimiwa Waziri ni njia hiyo hiyo moja tu, tofauti yake kila mtu anapita njia yake kufika huko.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anapendekeza wata-*co-opt,* maana yake itakuwa siyo lazima; lakini ikiingia hapo kwenye sheria kwamba hawa watawakilishwa, kama ambavyo *amendment* yetu imetaja, kwamba hii taasisi ni *professional.* Sasa mtu, yaani ili chuo kijue kwamba wanawajibika kuwepo huku, uwakilishi wao; siyo hiyari ya Mheshimiwa Waziri au bodi kuona kama inafaa au haifai; na ina maana pana kisheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno aliyoyasema Mheshimiwa Waitara hayafanani na yalivyoandikwa huku kwa sababu anasema hawa wabobezi watatu ambao wanatajwa hapa na sheria wako mitaani, hapana. Hawa watu hawako mitaani, ni watu wenye weledi ambao wamefanya utafiti kwenye uvuvi. Watu wa namna hii huwakuti mtaani, unawakuta kwenye hivyo vyuo ambavyo Mheshimiwa Waitara anasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa taabu sana hapa tukianza kutaja vyuo vikuu, sijui cha Dar es Salaam, sijui cha wapi wakati nchi yetu hii ina-*envolve and develop;* yaani mabadiliko haya ya kitaaluma yanaendelea tu. Kesho kutwa tutakuwa na vyuo kumi vinavyofanya *research* kwenye *marine life;* sasa tutaanza tena kusema tuongeze na hivi vyuo vilivyojitokeza na kadhalika.

Mheshimiwa Menyekiti, ilivyokaa hivi, inamwachia ile *flexibility* anayeteua bodi kusema leo aliyebobea vizuri zaidi yuko *Institute of Marine Science - University of Dar es Salaam,* anam-*pick* yule. Kesho kutwa atapatikana mtaalam wa kutoka *SUA*, atamchukua yule wakati anaunda bodi nyingine na kadhalika, lakini siyo kuweka kifungo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu, tunasema kwenye Kanuni tunaweza kutoa *provision* ya ku-*co-opt* wajumbe kwenye bodi, mradi tu wasipige kura, tunahitaji weledi wao, sasa atuache tukae hivi na tuweke hiyo *provision* ya ku-*co-opt* na huko kwenye kanuni kama ambavyo umemshauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru, lakini napendekeza tu kwamba nakubaliana na mawazo yake ya kwenda ku-*co-opt* lakini napenda basi hiki kifungu kisomeke; katika hawa watu watatu, angalau mmoja atoke kwenye Chuo Kikuu cha Tanzania ambacho kina-*deal* na mambo hayo, basi. Angalau mmoja, halafu ata-*specify*. Mimi hapa sina hoja, ili tusiendelee kubishana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, *members being experts in fisheries or aquaculture* watatoka kwenye vyuo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo vyuo, sasa si iingie kidogo hapo?

**MWENYEKITI:** Hawa hawawezi kutoka mitaani, watatoka kwenye vyuo. Sheria imeandika hivyo Mheshimiwa Waitara, wewe ni msomi, mtaalamu wa vitu hivi. Kubali tu yaishe shehe!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha miswada; hivyo unavyokizungumza siyo kitu kipya. Tumependekeza katika muswada wa *professional* hapa. Kama hivyo ni sawa, yeye kusema tu kwamba, hii unayosema hoja yake aingize itaje angalao mmoja, kuna shida gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaweza akachukua au asichukue. Ni hivi, wako watafiti wataalam, wamemaliza vyuo vyao, wana taasisi zao, wanafanya utafiti na wanaendelea, hawapo kwenye vyuo na wala hawafundishi. Hoja yangu ni kwamba kuwe na *link* kati ya taasisi hii na vyuo vikuu na wanafunzi ambao wanaingia pale; kinachopatikana kipya kiende kwenye mitaala, kuna uwakilishi, ndiyo hoja yangu. Nami sina lengo la kutaka kubishana bure hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri anasema, *this is a dynamic issue.* Ukitaka ku-*spare* hivyo vitu uki-*zero in* unavyotaka wewe, miaka sita ijayo turudi tena kuja kutengeneza sheria nyingine.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeingia kwenye mtandao, Uganda wanayo na wameuinganisha *professional* wanaitaja…

**MBUNGE FULANI:** Aah, sasa sisi siyo Uganda!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nairobi, Kenya wametaja *Nairobi University* kwenye *pharmacist!* Kwa hiyo, siyo jambo jipya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, nafikiri ulishakubali; na Serikali imekubali kuweka kwenye kanuni, mengine yatakuwa *complimented* namna sheria itakavyopitishwa. Nakushukuru sana, ahsante sana, karibu. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungwe mkono na Wajumbe wengine watoe maoni. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Haya, Wajumbe wangapi wanataka kumuunga mkono? Wamechoka wenzio hao, hakuna mtu wa kuunga mkono, kaa chini sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waitara kaa chini *please,* muda wako umekwisha.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. *AG!*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *further schedule of amendment* ya Serikali kwenye aya hii, kuna makosa ya *typing* kwenye *paragraph 1(b)(ii),(iii),(iv)* iliandikwa kimakosa *(iv)* ziko mbili, ukurasa wa 26 pale. Kwa hiyo, tunaomba kufanya marekebisho hapa kwamba ile ya mwisho iliyokuwa imeandikwa *(iv)* iwe *(v)*. Pia katika aya hiyo kuna neno limeandikwa "*economists,*" ni "*economics.*" Badala ya "*economists*" ni "*economics*" na lenyewe sasa tulifanyie marekebisho.

**MWENYEKITI:** Ahsante, pamoja na marekebisho hayo?

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea!

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Mtoa Hoja!

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(The Tanzania Fisheries Research Institute Act, 2016)* kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake na kuukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu pamoja na merekebisho yake sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda na kwa hatua ya Bunge, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kutunga Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Kuainisha Mamlaka na Utendaji wa Taasisi Kuhusiana na Uendeshaji wa Utafiti wa Uvuvi na Utafiti wa Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji na Kuainisha Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.

*[A Bill of an Act to Establish the Tanzania Fisheries Research Institute and to Provide for its Powers and Operations in Relation to the Conduct and Promotion of Research in Fisheries and Aquaculture and to Provide for Matters Incidental thereto]* Kusomwa Mara ya Tatu.

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sheria sasa imepitishwa rasmi na Bunge, inangoja hatua ya ngazi ya juu ya mamlaka ya Rais kwa mujibu wa Katiba.

Nachukua nafasi kukupongeza Mheshimiwa Waziri, umefanya kazi nzuri na *Attorney General.* Pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu na kazi nzuri ambayo mmeifanya na hatimaye tumemaliza miswada yote sita ambayo Serikali imeileta kwenye Bunge hili. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 3.33 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 16 Septemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*